Hedayah
countering violent extremism

# KUDHOOFISHA SIMULIZI ZA UFURUTU ADA AFRIKA MASHARIKI

## NAMNA YA KUONGOZA



SARA ZEIGER

AGOSTI 2018

*MUONGOZO HUU SIO WA KUGAWA KWA UMMA*

# KUDHOOFISHA SIMULIZI ZA UFURUTU ADA AFRIKA MASHARIKI

## NAMNA YA KUONGOZA

SARA ZEIGER

*MUONGOZO HUU SIO WA KUGAWA KWA UMMA*

# FAHARASA YA MANENO

**Kupambana na Ufurutu Ada**

Kupambana na ufurutu ada inamaanisha matendo yanayozuia ushawishi na ajira kwa makundi ya kigaidi au itikadi kwa kupitia njia zisizo na vurugu.

**Kuzuia Ufurutu Ada**

Kuzuia ufurutu ada ni kitendo cha kukinga matendo, itikadi na vurugu zitokanazo na kukiuka misingi ya jamii. Kukinga huku hufanyika kabla ya vurugu kuibuka.

**Simulizi Kinzani**

Ni hadithi zinazokataa au kuharibu simulizi au propaganda za wafurutu.

**Simulizi Mbadala**

Ni hadithi ama simulizi zenye kuonyesha utofauti wamatendo na itikadi ya wafurutu zikiwa na nia ya kuonyesha njia mbadala za matendo tofauti na vurugu.

**Ufurutu Ada**

Ni Kiswahili fasaha cha "msimamo mkali" ukimaanisha matendo ya vurugu, itikadi na vurugu zitokanazo na kukiuka misingi ya jamii. Hapa inamaanisha zaidi ya kuwa mhusika anakithiri sio tu kwa mtizamo na itikadi bali hualalisha imani yake na itikadi kwa matendo ya vurugu pia.

**Mfurutu**

Ni mtu mwenye itikadi na matendo ya vurugu zitokanazo na kukiuka misingi ya jamii na kutumia nguvu ili kupata suluhu haraka. Mtu huyu hujiona sahihi kuliko wengine na kusimamia itikadi anayoiamini na huwa tayari kutumia nguvu ili kuhalalisha imani yake kwa wengine.

*Tafsiri na faharasa katika kitabu hiki imefanywa na Modern Linguistics and African Culture Promotion Centre (MOLAC) chini ya wataalamu wake Jacob Mulikuza, Martin Mufungizi, Martino Mbangile na Faysal Ahmed Sheikh. MOLACinapatikana Arusha-Tanzania.*

Mawazo yaliyopo katika muongozo huu ni maoni ya mwandishi, na sio lazima yaakisi mawazo ya Hedayah au Idara ya Serikali ya Watu wa Marekani.

© Hedayah, 2018
Haki zote zimehifadhiwa.

Muonekano na chapisho hili umebuniwa na Iman Badwan.

**KUHUSU MUONGOZO HUU**

Muongozo huu ni muendelezo wa "Warsha ya Wataalamu kuhusu Afrika Mashariki na Pembe ya Afrika Kukusanya Simulizi Kinzani za Kupambana na Ufurutu Ada", uliofanyika tarehe 5-7 Februari 2018 mjini Kigali, Rwanda. Warsha na Namna ya Kuongoza hii imefadhiliwa na Idara ya Serikali ya Watu wa Marekani.

Muongozo huu na viambatanishi vya simulizi kinzani vinapatikana kupitia maktaba iliyopo ya Simulizi Kinzani ya Hedayah (www.cn-library.com). Kwa taarifa zaidi kuhusu mradi, tafadhali angalia kiambatanishi A. Kuingia kwenye maktaba ya Simulizi Kinzani, tafadhali wasiliana na cnlibrary.admin@hedayah.ae.

**KUHUSU WAANDISHI**

**Sara Zeiger** ni Meneja Mradi kwenye Idara ya Utafiti na Uchambuzi ya Hedayah na anaongoza kitengo kingine Hedayah kinachohusu Kuzuia na Kupambana na Ufurutu Ada na Elimu. Sara humsaidia Mkurugenzi usimamizi wa miradi ya Idara, ikijumuisha Maktaba ya Simulizi Kinzani, Mradi wa Ushirika wa watu wasio wakazi na Mkutano wa mwaka wa kimataifa wa Utafiti wa Kupambana na Ufurutu Ada. Amehusika pia kutengeneza mfumo wa kielectroniki wa Ufuatiliaji, Kupima na Kutathimini miradi ya Kuzuia na Kupambana na Ufurutu Ada ujulikanao kama MASAR. Machapisho yake ya hivi karibuni ni pamoja na Ushawishi wa Vurugu na Ufuru Ada Uliokithiri Ulaya na Kuzuia na Kupambana na Ufurutu Ada Afrika : Jukumu la Sekta ya Madini. Pia ameshiriki kwenye uandishi wa matoleo mawili yaliyopita ya "Namna ya Kuongoza" kwa Kusini Mashariki ya Asia na Afrika Mashariki ya kati na Kaskazini. Sara pia kwa sasa ni Mshirika Asiye Mkazi wa Uhusiano wa Kimataifa na Kupambana na Ugaidi wa shirika la TRENDS Research & Advisory.

Kabla ya kujiunga na Hedayah, Sara alifanya kazi kama Mtafiti Msaidizi katika Kituo cha Masomo Mashariki ya Kati Chuo Kikuu cha Harvard.Pia amewahi kuwa Mshirika Mkufunzi Mkuu wa Shule Shiriki ya Harvard na alikuwa Mkufunzi Msaidizi wa Chuo kikuu cha Boston. Sara ana Shahada ya Uzamili ya Mahusiano ya Kimataifa na Dini (Akijikita kwenye :Masomo ya Ulinzi na Uisilamu) kutoka Chuo Kikuu cha Boston, na alihitimu kwa alama za juu kabisa na Shahada ya Saikolojia na Dini kutoka Chuo Kikuu cha Kaskazini Ohio.

**WATAALAMU (KWA MPANGILIO WA ALPHABETI)**

Namna ya Kuongoza hii isingeliandaliwa bila mawazo na michango kutoka kwenye kundi la wataalamu waliohudhuria warsha mjini Kigali, Rwanda. Wataalamu waliochangia kwenye warsha kwa kufanya mawasilisho na mijadala ambayo ilitoa dira ya Muongozo huu na kuujaza kwa mifano ya kupambana ama kutoa simulizi mbadala. Wataalamu hawa ni:

Fauziya Abdi
*UN Development Program*

Fatma Ahmed
*Albany Associates*

Mahamoud Ahmed
*United Religious Initiative, Djibouti*

Rebecca Besant
*Search for Common Ground, Rwanda*

Abdi Billow
*WAJIR Peace and Development Agency, Kenya*

Chris Chant
*Adam Smith International*

Patricia Crosby
*Commonwealth Secretariat*

Jessie Francescon
*Hedayah*

Matthew Freear
*Royal United Services Institute*

Sami Gathii
*YADEN East Africa, Kenya*

Mugita Gesongo
*BRICS Implementation, Kenya*

Claudia Harley
*European Institute of Peace*

Ursula Iszler
*US Embassy, Kigali*

Nuwagaba Muhsin Kaduyu
*Allied Muslim Youth Uganda*

Chris Maitland
*Australian Embassy, Ethiopia*

Adam Matan
*Anti-Tribalism Movement, Somalia and UK*

Omar Mattar
*Organization for Community Empowerment, Tanzania*

Ayub Mohamud
*Community Development Initiative, Kenya*

Martha Nghambi
*Global Peace Foundation, Tanzania*

Joseph Nkurunziza
*Never Again Rwanda*

Simon Nyambura
*IGAD Center of Excellence*

May Salem
*Cairo International Center for Conflict Resolution, Peacekeeping and Peacebuilding*

Murat Uzunparmak
*Hedayah*

Emmanuel Wakana
*Youth Empowerment and Leadership Initiative, Burundi*

Yosa Wawa
*University of Juba, South Sudan*

Rebecca Wiles
*Breakthrough Media*

Elizabeth Young
*BRICS, Kenya*

**SHUKRANI**

Mwandishi angependa kuwashukuru Jessie Francescon, Mkurugenzi wa Hedayah idara ya Majadiliano na Mawasiliano, na Murat Uzunparmak, Mkurugenzi wa Hedayah idara ya Utafiti na Uchambuzi, kwa mchango wao kwenye warsha na muongozo. Mwandishi angependa pia kumshukuru Sara Pan Algarra kwa kusaidia kuandaa rasimu ya muongozo huu na viambatanisho.

# UTANGULIZI

Ugaidi na ufurutu ada[1] umekua tatizo Afrika Mashariki[2] katika kipindi cha miongo mingi iliyopita. Tatizo hili chimbuko lake ni migogoro ya ukabila, dini, jamii, uchumi, tamaduni na kikabila. Utofauti wa ukanda huu mara nyingine umechangia sababu za uharibifu zinazopelekea ushawishi na vurugu, ila kwa upande mwingine umesaidia kujenga ustahimilivu wa jamii na kukuza mabadiliko kutoka kwenye vurugu hadi amani.

Tishio la hivi karibuni na kubwa katika ukanda huu linaendelea kuwa Al-Shabaab, lenye makao yake makuu Somali ila kuna ushahidi kundi hilo linajiendesha huko Djibouti, Ethiopia, Kenya, Tanzania na Uganda. Baada ya bomu lililotegwa kwenye gari kulipuka huko Mogadishu Oktoba 2017 na kuuwa watu zaidi ya 350, ni dhahiri ya kuwa kundi la Al-Shabab lililo tishio halitotoweka katika siku za hivi karibuni (Hili halikuwa bomu lingine tu 2017). Kutoka kwenye jicho la kuzuia na kupambana na ufurutu ada, kudhoofisha ushawishi na simulizi za ajira za Al-Shabaab ni muhimu sana katika ukanda huu.

Wakati huo huo, kuna migogoro ya kienyeji ambayo inaweza kugeuka kuwa shughuli za ufurutu ada katika ukanda huu. Zaidi ya hayo, siasa za kitaifa zisizoridhisha na uhuru wa kutembea umeruhusu vikundi mbalimbali vya waasi na wafurutu ada kujitengeneza hata nje ya mipaka. Kwa mfano, kundi la waasi lililozaliwa Uganda, Vikosi vya Washirika Kidemokrasia (ADF) linajishughulisha nje ya Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na linaajiri watu kutoka mpaka wa Magharibi mwa Uganda. Kundi hili linachukuliwa kama kundi la kigaidi na Serikali ya Uganda, kundi la ADF lilianzishwa kwenye itikadi ya dini (Kiislamu) ila limeshageuka na kuongeza itikadi ya siasa kama sehemu yao ya jitihada za kuajiri. Bado kundi hili ni tishio kwa Serikali ya DRC na Uganda, kundi la ADF lilituhumiwa kufanya mashambulizi huko Semuliki, DRC, mwaka 2017 ("RDC : Mandats d'Arrêt," 2018).

Kwenye nchi nyingine, mabadiliko mepesi ya kisiasa yamechangia mazingira mapya ya vurugu kuibuka. Kwa mfano, Burundi mwaka 2015, Rais Pierre Nkurunziza alitangaza angegombea muhula mwingine wa Urais, kauli hii ilizua maandamano nchi nzima. Mwezi mmoja baadaye, mapinduzi yaliyoongozwa na Meja Jenerali Godefroid Niyombare yaliyolenga kumuondoa Rais hayakufanikiwa. Wakati mazungumzo ya kisiasa yakiendelea kubadili ukomo wa muda wa Urais yamepelekea mabadiliko ya kikatiba, vurugu zimekuwa wazi kwenye maandamano ya kisiasa nchi nzima, mashambulizi kadhaa yamejitokeza Bujumbura wakati wote wa majira ya joto 2017 (" Watatu waliuawa kwenye mashambuizi ya bomu la mkono Burundi," 2017).

Ukirejea historia, Afrika Mashariki imekuwa mhanga wa vurugu kadhaa na makundi ya wafurutu ada. Kwa mfano, kundi la Lord's Resistance Army (LRA) lilikuwa ni tishio kwa Uganda, Sudan Kusini, Jamhuri ya Afrika ya Kati, na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) katikati ya miaka ya 1990. Chini ya uongozi wa Joseph Kony, kundi la LRA lilitaka kuanzisha demokrasia iliyojikita chini ya Amri Kumi za Mungu. Hata hivyo, kundi la LRA kihistoria ni kabila la Kiacholi kutoka Kaskazini mwa Uganda, ikimaanisha kuna msukumo wa kikabila unaohusiana na malengo yake ya kisiasa. Tukio maarufu duniani, lilihusisha vurugu za mauaji ya halaiki yaliyofanywa na Serikali ya Wahutu dhidi ya Watutsi huko Rwanda katikati ya miaka ya 1990unakuwa mfano uliokithiri wa upotevu wa hali ya juu ya maisha na uwezekano wa hatari ya ufurutu ada. Mwisho, kati ya miaka ya 1970 jeshi lililosheheni vurugu lililotawala kwa mabavu, maarufu kama Derg, liliikumba Ethiopia na mauaji ya halaiki kwa kile kilichojulikana kama Qey Shibir au "Hofu

[1] Ufurutu Ada ni Kiswahili sanifu cha msimamo mkali
[2] Kwa madhumuni ya taarifa hii, ukanda huu unajumuisha Burundi, Djibouti, Ethiopia, Rwanda, Kenya, Sudan ya Kusini, Somalia, Tanzania na Uganda.

Nyekundu," ambapo wapinzani wa kisiasa wa kundi la mlengo wa Marx na Lenin waliokuwa madarakani waliuwawa kwa wingi sana ("Mengistu alifungwa kifungo cha maisha," 2007).

Kwa kuzingatia hali ya sasa na ya historia ya Afrika Mashariki na ugumu wake, ni vyema kupinga ujumbe wa chuki, vurugu, ufurutu ada na ugaidi kwenye ukanda mzima, badala yake ni kutumia mbinu mbadala kukabiliana na migogoro na mivutano kati ya makundi tofauti. Zaidi ya hayo, kwa karne hii ambayo intaneti na mitandao ya kijamii ina jukumu muhimu kwenye maisha ya vijana ambao ni wahanga wa ufurutu ada, ni muhimu kutambua ya kuwa, kwa muktadha wa Afrika Mashariki, ajira nyingi kwa ukanda huu hufanyika nje ya mtandao (UNDP, 2017). Hii inamaanisha simulizi kinzani na simulizi mbadala kwa juhudi ya kuzuia na kupambana na ufurutu ada inahitaji kujumuisha vipengele vinavyokidhi matakwa ya vyombo vya habari vya jadi au ifanyike ana kwa ana.

Lengo la hii Namna ya Kuongoza ni kuwapatia nyenzo ya kuwaongoza watendaji, Asasi Zisizo za Kiserikali, na watunga sera wanaojihusisha na ujumbe kinzani na simulizi mbadala kuongeza na kukuza ujumbe dhidi ya ufurutu ada Afrika Mashariki. Muongozo unajumuisha orodha ya kina ya vyanzo huru vya simulizi kinzani na simulizi mbadala ambazo zinaendana na mazingira tofauti ya kitamaduni na kijamii ya nchi za Afrika Mashariki(Tazama Kiambanisho B). Lugha ya simulizi katika mjumuisho huu ni pamoja na Kiarabu, Kiingereza, Kifaransa, Kisomali, Kirundi na Kiswahili.

Muongozo huu ulitengenezwa kwa kutumia mbinu mchanganyiko kwa kuzingatia vipengele vya msingi viwili. Kwanza, simulizi kinzani husika, mazoea mazuri na mifano dhahiri iliyokusanywa kupitia mapendekezo kutoka kwenye kundi la wataalamu lililokutana Kigali, Rwanda kutoka tarehe 5-7 Februari 2018 kwenye "Warsha ya Wataalamu kuhusu Afrika Mashariki na Pembe ya Afrika Kukusanya Simulizi Kinzani za Kupambana na Ufurutu Ada". Wenyeji wa warsha hii walikuwa Hedayah na Kituo cha Ubora IGAD cha Kuzuia na Kupambana na Ufurutu Ada (ICEPCVE). Pili, mwandishi wa taarifa hii alifanya utafiti dawati kuongeza muktadha, maudhui na nadharia katika muongozo huu. Ieleweke ya kuwa, Namna ya Kuongoza hii ya sasa inafuata mpangilio na muundo sawa sawa na taarifa mbili zilizopita zilizoandaliwa na Hedayah, Kudhoofisha Simulizi za Ufurutu Ada Kusini Mashariki mwa Asia : Namna ya Kuongoza (Zeiger, 2016), na Kudhoofisha Simulizi za Ufurutu Ada Mashariki ya Kati na Kaskazini Afrika : Namna ya Kuongoza (El Sayed, Faris & Zeiger, 2017). Mpangilio uliopita ulitegemea mchakato endelevu uliojumuisha maoni kutoka kwa wataalamu wa simulizi kinzani, wanazuoni na maafisa wa serikali, na ulipitia mchakato wa kurejea, na baada ya hapo kutoa msingi bora wa Namna ya Kuongoza hii ya ziada na mfululizo ujao.



## NINI MAANA YA “KUPAMBANA NA UFURUTU ADA” ?

Katika wigo wa mbinu za kupambana na ugaidi, mikakati “mepesi” au “ya kuzuia”, sera na miradi ya kutambua changamoto za sababu za “kusukuma” na “kuvuta” za ushawishi na ajira zinaelezewa kama “Kupambana na ufurutu ada” au mipango na sera za ufurutu ada.

Kwa nia ya Namna ya Kuongoza hii, kupambana na ufurutu ada inajumuisha mipango ya muda mrefu ya kuzuia sababu za jumla za kiuchumi-jamii na siasa, na mikakati mahususi iliyotengenezwa katikangazi ya jamii na mtu binafsi (kujumuisha ushauri nasihi wa kisaikoloji kwa watu walio katika hatari pamoja na wafungwa) (Nakala ya awali kutoka kwa Zeiger, 2016).

# KUTENGENEZA SIMULIZI KINZANI

Kutokana na mfululizo wa awali wa Hedayah wa "Namna ya Kuongoza," kuna hatua 9 za kutengeneza simulizi kinzani za kupambana na Ufurutu Ada (Zeiger, 2016):

1. ELEWA NA TATHIMINI SABABU HUSIKA ZA KUSUKUMA NA KUVUTA
2. TAMBUA WALENGWA KUSUDIWA
3. TAMBUA SIMULIZI ZA UFURUTU ADA ZILIZO WAZI AU ZISIZO WAZI ZINAZOPINGWA
4. WEKA LENGO NA SHABAHA MAHUSUSI YA SIMULIZI KINZANI
5. AMUA MJUMBE MFANISI
6. TENGENEZA MAUDHUI NA MANTIKI KWENYE UJUMBE
7. TAMBUA NJIA ZA KUSAMBAZA UJUMBE
8. TENGENEZA MKAKATI WA USAMBAZAJI
9. TATHIMINI NA PEMBUA MATOKEO YA SIMULIZI KINZANI

## 1 ELEWA NA TATHIMINI SABABU HUSIKA ZA KUSUKUMA NA KUVUTA

Mipango yeyote ya Kupambana na Kuzuia Ufurutu Ada, ikijumuisha ile iliyopo eneo la simulizi kinzani, hatua muhimu ya mwanzo ya mchakato ni kuelewa mazingira ya asili na vichocheo vya asili vya ushawishi. Hapa Afrika Mashariki, kuna sababu za kipekee sana zinazopelekea watu binafsi kwenye ufurutu ada, na kwa sababu ya mnyumbuliko wa jamii ni muhimu zaidi kutathimini vichocheo asili vya ushawishi kwenye jamii kabla ya kutengeneza kampeni zozote za simulizi kinzani.

Ili kuonesha dhana hii kwa ukanda wa Afrika Mashariki, Namna ya Kuongoza zilizopita zilitumia mfano wa USAID (2011) wa kutambua sababu za "kusukuma" na "Kuvuta". Ila, ni vyema ikatambulika ya kuwa, kuna machapisho ya hivi karibuni kutoka Royal United Services Institute (RUSI) ambapo yameelezea vichocheo hivi vya ushawishi kama "vichocheo muundo," "motisha binafsi," na "sababu wezeshi" (Khalil & Zeuthen, 2016, p. 10). Kwahiyo, kwenye mpangilio ufuatao hapo chini, makundi yote matatu yametumika ipasavyo kuweza kutofautisha sababu binafsi na za kisaikolojia za "kuvuta" kuelekea ugaidi ambavyo ni vivutio vya ndani ikilinganisha na sababu za nje zinazowezesha mchakato wa haraka wa ajira. Hii ni muhimu sana kwa muktadha wa Afrika Mashariki ambapo kihistoria, viongozi wenye karisma kama Joseph Kony wamekuwa wamuhimu sana kuajiri wafuasi wapya na kuendeleza imani ya kundi.

Jedwali lifuatalo hapa chini linaeleza kwa ufupi vichocheo muhimu vya ushawishi Afrika Mashariki. Ifahamike ya kuwa, kumekuwa na tafiti nyingi zinazochunguza vichocheo vya ushawishi kwenye muktadha wa nchi tofauti za Afrika Mashariki. Kwahiyo, jedwali linaundwa na taarifa kutoka vyanzo viwili: 1) majadiliano ya vichocheo vya ushawishi wakati wa warsha ya wataalamu Kigali; na 2) vichocheo muhimu vilivyoainishwa kutoka kwanye machapisho husika kutoka Afrika Mashariki. Orodha hii sio ya kina, ila inaonyesha mnyumbuliko wa aina za sababu zinazoweza kupelekea ushawishi na kuajiriwa kwenye makundi mbalimbali ya kigaidi na wapiganaji kwenye ukanda huu.

Nimuhimu kutambua sababu kuu au vichocheo vya ushawishi kwenye ukanda huu au sehemu husika kabla ya kutengeneza mikakati yeyote ya Kupambana na Ufurutu Ada, hususani kwa simulizi kinzani kwa sababu kuumbili : 1) kuzuia kutoa taarifa isiyo sahihi kwa kundi la watu kama "wenye mazingira magumu" bila kufanya tathimini yoyote ya kina;na 2) kuweza kuchagua kwa usahihi walengwa ambao wanaweza kushawishika na simulizi kinzani.

| SABABU ZA KUSUKUMA/ MOTISHA YA KIMFUMO | SABABU ZA KUVUTA/ MOTISHA YA MTU BINAFSI |
|---|---|
| Siasa<br>• Majeshi ya Umoja wa Afrika ya Kulinda Amani Somalia (AMISOM) na uwepo wao nchini Somalia;<br>• Serikali dhaifu, hasa hasa vijijini kwa Afrika Mashariki yote (Dualeh, 2015);<br>• Matendo ya hasira yanayofanywa na vyombo vya usalama au polisi yanazidisha malalamko (Africa Center for Strategic Studies, 2012); | Jamii/ Kisaikolijia<br>• Motisha ya kutafuta mchumba kutokana na ufahari wa kuwa kwenye shirika la kijeshi;<br>• Kisasi, kwa mfano kwa ukatili wa polisi au mauaji ya wanafamilia (Scofield Associates, 2017);<br>• Uwezo wa kuwa na ajira (Botha, 2016);<br>• Kupenda kupita kiasi wafurutu ada au magaidi kwa kukosa |

| SABABU ZA KUSUKUMA/ MOTISHA YA KIMFUMO | SABABU ZA KUVUTA/ MOTISHA YA MTU BINAFSI |
|---|---|
| • Kutokufurahishwa na mfumo wa kisiasa au kukosa ushawishi wa kisiasa;<br>• Polisi kukusanya taarifa ya watu wachache kama wahalifu na kuwataja hadharani hata kama hawana makosa.<br><br><u>Uchumi-Jamii</u><br><br>• Kubaguliwa makabila au ukoo (mf. Wasomali na Wakenya) (Botha, 2016; Strasser, 2016);<br>• Ukosefu wa ajira au umasikini (Russell, 2017);<br>• Ukosefu wa mahitaji muhimu na miundombinu;<br>• Ukosefu wa elimu au fursa ya elimu[3];<br>• Mategemeo kutoka kwenye jamii na kushindwa kuyafikia haya matarajio (Mf. Ajira, nyumba);<br>• Msukumo kutoka kwenye jamii kufanya mambo kwa aina Fulani;<br>• Ukosefu wa mitandao na mifumo ya vijana rika;<br>• Utofauti wa kipato na mabadiliko ya hali ya uchumi-jamii kwenye mitaa duni (Guha, 2017). | baba mzazi kama kiongozi wa familia (Botha, 2016);<br>• Kuvutiwa kuwa na fursa ya kupata bunduki, kama alama ya nguvu;<br>• Kuwa kwenye mazingira ya vurugu kwa muda mrefu (Small Arms Survey, 2017);<br>• Kuvutiwa kuwa na nguvu, fursa na cheo ndani ya kundi.<br><br><u>Itikadi ya Dini</u><br><br>• Zawadi baada ya kifo kwa kutenda jambo;<br>• Itikadi ya kisiasa, matamanio ya mabadiliko au mageuzi.<br><br><u>Motisha za Kiuchumi na Zilizojikita Kimatumizi</u><br><br>• Kupewa zawadi kama pikipiki au fursa ya silaha;<br>• Kupatiwa huduma za muhimu kama chakula, malazi, madawa na maji;<br>• Kupatiwa sehemu ya kujificha au kutoroka mamlaka;<br>• Kupata fursa ya mitandao ya dawa za kulevya na pombe (Le Sage, 2014). |

| SABABU WEZESHI |
|---|
| • Uwepo wa wahubiri wenye msimamo mkali kwenye Misikiti;[4]<br>• Mabadilishano ya kundi rika kunaongeza hali ya kijamii ;<br>• Viongozi wenye karisma (haiba) kama Joseph Kony wa Uganda. |

**Jedwali 1: Sababu Muhimu za Kuvuta na Kusukuma Afrika Mashariki.**

*<u>Kumbuka:</u> Jedwali hili ni kwa ajili ya mfano tu na sio orodha kamili. Sababu zinaweza kutofautiana kutoka nchi moja na nyingine na kati ya mikoa ndani ya nchi moja na malalamiko yanaweza kuwa ya ukweli au ya kusadikika.*

[3] Kwa mfano, nchini Uganda ambapo wafuasi wa LRA walikuwa na elimu ya shule ya msingi tu kwa (80%) (Botha, 2015).

[4] Kwa mfano, kumekuwa na mwito wa kujiunga na mapambano na wafuasi wa ndani wa Al-Shabaab kama vile msikiti wa Pumwani Riyadha na kituo cha Uisilamu cha Vijana karibu na Eastleigh (kuanzia 2008) nchini Kenya. Imearifiwa kuwa vituo hivi vya ajira havifanyi kazi tena kwa uwazi na ushawishi umepungua tangu mwaka 2012 (Odhiambo, E., Onkware, K., & Leshan, M, 2015).

## 2 TAMBUA WALENGWA KUSUDIWA

Hatua nyingine ya mchakato wa kutengeneza simulizi kinzani za ufurutu ada ni kutambua walengwa waliokusudiwa na kampeni yako. Kama ilivyotajwa hapo awali kwenye Namna ya Kuongoza ya Hedayah Kusini Mashariki mwa Asia na Afrika Mashariki ya Kati na Kuskazini, muongozo huu unachukua mbinu ya kimasoko unaofafanua walengwa waliokusudiwa kama sehemu muhimu na msingi wa kampeni (El Sayed, Faris & Zeiger, 2017). Mchanganuo wa walengwa husika ujumuishe umri, jinsi, kiwango cha elimu, eneo, maslahi ya kipaumbele, na shughuli za mtandaoni (Tuck & Silverman, 2016).

Kufafanua walengwa waliokusudiwa ni muhimu katika muktadha wa Afrika Mashariki, ambako ufurutu ada na simulizi zake umejidhihirisha kwa kupitia mambo mbalimbali ya ukabila, matabaka, dini na chimbuko la jamii. Zaidi ya yote, simulizi zinazotumiwa na wafurutu ada zinaenda sawa na lugha za asili za kila ukanda, nchi na wilaya ndani ya nchi. Kwa mfano, Al-Shabaab wanaweza kutumia sinema ya Kiarabu ili kupata uhalali wa kidini, ila wanaweza kubadili lugha Kiswahili au Kisomali kwa ajili ya ujumbe kwa walengwa wa ajira. Hata hivyo, mtengenezaji wa kampeni ya simulizi kinzani lazima pia azingatie lugha inayoendana na walengwa wanaojaribu kuwafikia.

Kuna tabia pia ya kusisitiza "vijana" kama walengwa waliokusudiwa na kampeni ya simulizi kinzani. Ila, kama wataalamu katika warsha iliyofanyika Kigali walivyosema, kundi la "vijana" sio walengwa waliotengenezwa. Hivyo basi, kampeni lazima izingatie akilini makundi maalumu ndani ya vijana wanaotaka kuwafikia na kutarajia mahitaji na maslahi yao wakati wa mchakato wa muundo. Mbinu hii hutumika mara kwa mara, kwa mfano, Taasisi ya Al-Kataib ya Utengenezaji Habari, mshirika wa habari wa Al-Shabaab hutengeneza ujumbe unaonendana na mahitaji na maslahi ya walengwa husika na manung'uniko ya jamii husika[5]. Baadhi ya mifano ya makundi ya "vijana" ndani ya kundi kubwa la vijana inajumuisha :

- Vijana walioko kwenye mfumo rasmi wa elimu
- Vijana walioacha shule
- Vijawa wa mjini dhidi ya vijana wa kijijini
- Vijana walioachiwa kutoka jela au waliojihusisha na mitandao ya kihalifu
- Vijana wenye familia bila vyanzo halali vya kipato
- Vijana wenye elimu na hawana ajira

Ilibainishwa kwenye warsha ya Kigali kuwa, vijana waliowahi kujihusisha na makundi au shughuli za kihalifu walikua katika hatari zaidi kuajiriwa na makundi kama Al-Shabaab. Kwa kuzingatia haya, Al-Shabaab mara nyingine hutumia uhalifu wa mtu kumlazimisha kujiunga na wakimuogopesha kumtaja kama hatajiusisha na ugaidi.

Kwa nyongeza, mtengeneza kampeni lazima azingatie kile jamii inachodhani ni "sawa " ndani ya jamii. Mtaalamu mmoja kwenye warsha alibainisha ya kuwa wafurutu hutumia kwa ufanisi propaganda yenye kuonyesha "Uasi sawa" kwa kuwa unaonyesha uasi na ukaidi dhidi ya serikali. Alitoa mfano wa malalamiko kutoka kwenye jamii ambapo polisi hawakabiliani na waandamaji kwasababu ni "sawa" kuonekana kama muasi.[6]

[5] Wasilisho la Matthew Freear kwenye Warsha ya Wataalamu juu ya "Simulizi Kinzani za Kupambana na Ufurutu Ada Afrika Mashariki na Pembe ya Afrika," Februari 2018, Kigali, Rwanda..

[6] Wasilisho la Sami Gathii kwenye Warsha ya Wataalamu juu ya "Simulizi Kinzani za Kupambana na Ufurutu Ada Afrika Mashariki na Pembe ya Afrika," Februari 2018, Kigali, Rwanda.

## Aina za Walengwa Waliokusudiwa

### WALENGWA WA JUMLA

Simulizi kinzani zinazolengwa kwa walengwa wa jumla zinaweza kusisitiza utamaduni wa pamoja au maadili ya kihistoria, yanaweza kuhimiza mada za kawaida za utu, au zinaweza kusisitiza amani, uvumilivu na mshikamano (Briggs & Feve, 2013). Katika muktadha wa Afrika Mashariki, kampeni zinazolengwa kwa walengwa wa jumla zinaweza kujumuisha sanaa shirikishi, matamasha ya wazi, midahalo na mazungumzo ya wazi. Ni muhimu kufahamu hapa kuwa, simulizi kinzani kwa ajili ya walengwa wa jumla ni muhimu ziwe mahususi kwa jamii husika kwa kadiri inavyowezekana, na zitengenezwe kuendana na mahitaji ya jamii. Malalamiko na changamoto jamii inazokumbana nazo zinatofautiana kutoka nchi moja hadi nyingine na mkoa mmoja hadi mwingine ndani ya nchi moja.

### WAHAMASISHAJI WAKUU

Aina hii ya walengwa inahusu watu mashuhuri kwenye jamii kama viongozi wa mila, waalimu, makundi rika, wanafamilia au maafisa ustawi wa jamii. Wahamasishaji wakuu ni watu wenye uwezo kuathiri watu "wenye mazingira magumu". Ila, wahamasishaji wakuu wanaweza kukosa maarifa ya kujihusisha na kupambana na ujumbe. Kwa mfano, mama wa wahanga wa shambulio la ugaidi wanaweza kuwa na hadithi nzuri sana, ila wanaweza kuwa hawajafundishwa namna ya kuwasilisha ujumbe wao. Hivyo basi, kampeni zinazolengwa kwa wahamasishaji wakuu zinaweza kuhusisha mambo ya kujenga maarifa na ujuzi wakuwasilisha.

### WAFUASI

Kundi hili linamaanisha watu ambao moja kwa moja kikamilifu au kwa uwazi/ sauti hawaonyeshi kukubali ufurutu ada ila wanaweza kuwa wafuasi wa baadhi ya hoja zinazoletwa na propaganda za ugaidi kwa sababu ya utamaduni, muktadha wa jamii na kihistoria wa ukanda husika. Wafuasi hawa sio hai sana kukubali ufurutu ada na wanaweza wasifanye chochote pindi watakapokutana na ujumbe wa ufurutu ada, ila kwa ukimya hukubaliana na ujumbe hizo. Kundi hili linajumuisha watu ambao wako katika "hatari" ya kushawishika au ni watizamaji wazuri wa propaganda za ugaidi mtandaoni (Briggs & Feve, 2013).

### WATETEZI

Kundi la "Watetezi" linajumuisha watu ambao kikamilifu na kwa uwazi hualalisha hoja na matendo ya makundi ya kigaidi. Hii inajumuisha, kwa mfano muhubiri ambaye kikamilifu huunga mkono matendo ya kijeshi dhidi ya serikali ya Somalia, ikiwemo matendo ya vurugu yanayofanywa na Al-Shabaab.

### WAHUSIKA NA MAGAIDI

NI walengwa wenye changamoto ya kuwafikia kwa simulizi kinzani kwani wamejumuisha watu waliojitolea kikamilifu kushiriki katika ugaidi na wanaotumia matendo ya vurugu kupata malengo yao ya kisiasa, itikadi au dini. Kwa mukatadha wa Afrika Mashariki, hii itajumuisha magaidi waliokamatwa na kufungwa jela na serikali au wale waliotiwa hatiani kwa makosa ya kigaidi.

## 3 TAMBUA SIMULIZI ZA UFURUTU ADA ZILIZO WAZI AU ZISIZO WAZI ZINAZOPINGWA

Hatua nyingine kwenye mchakato ni kutambua ujumbe muhimu wa propaganda za ufurutu ada ambao ujumbe kinzani utajikita. Simulizi inayopingwa inaweza kupingwa kwa uwazi au kwa kuficha ficha (ikimaanisha kutoa simulizi mbadala au suluhisho la malalamiko).

Kwa kuzingatia mada zilizowasilishwa kwenye Namna ya Kuongoza ziliyopita, simulizi za wafurutu ada zilizo sahihi kutoka Afrika Mashariki ni:

- SIMULIZI ZA SIASA NAKIJESHI
- SIMULIZI ZA JAMII NA BINAFSI
- SIMULIZI ZA KIKABILA NA KIMILA
- SIMULIZI ZA DINI NA ITIKADI
- SIMULIZI ZA UCHUMI

Ieleweke kwamba kwenye mifano ifuatayo hapa chini, baadhi ya makundi yaliyobainishwa hayachukuliwi kama yakigaidi kwa viwango vya kimataifa. Ila, simulizi za makundi ya wapiganaji au waasi ni sahihi sana kwa muktadha wa Afrika Mashariki, na kwa hiyo baadhi ya mipango ya propaganda ya mashirika haya ni sahihi na zimeelezwa ili kuelewa vyema muktadha wa aina ya simulizizinazotolewa.Ifahamike pia ya kuwa, simulizi za wafurutu ada Afrika Mashariki zinaendana na mazingira na zimebadilika kulingana na muda, hivyo ni muhimu kuzingatia simulizi za sasa na zinazobadilika.[7]

### Simulizi za Kisiasa na Kijeshi

Simulizi maarufu zinazotumika na wafurutu ada Afrika Mashariki kuajiri na kushawishi watu ni siasa na jeshi kuhalalisha matumizi ya vurugu. Mifano mbalimbali ya simulizi za kisiasa na kijeshi zimeelezwa kwa ufupi hapa chini. Ila, orodha hii sio ya kujitosheleza kwa kuwa simulizi za ufurutu ada ni za aina tofauti katika ukanda wa Afrika Mashariki.

1. **Kiwango cha Kutenda na Uwezo wa Kuongoza**
   Simulizi hii hutumia hoja za kisiasa kuonyesha uhalali wa makundi ya kigaidi kuwa na uwezo wa kuongoza kuliko serikali za Afrika Mashariki. Kwa mfano, kabla ya uchaguzi nchini Kenya mwezi wa sita mwaka 2017, Taasisi ya Habari ya Al-Kataib, chombo cha habari cha Al-Shabaab, kilitoa sinema ijulikanayo kama "Tathimini ya Matukio : Ujumbe kwa Waislamu Kenya " uliosisitiza kuwa Al-Shabaab ina uwezo wa kupata rasilimali, himaya na kulinda watu wao, ujumbe huu ukionyesha ya kuwa serikali ya Kenya haiwezi kuongoza vyema (MEMRI,2017). Hata hivyo, sinema iliyotengenezwa na Al-Shabaab baada ya shambulio la Januari 2016 lililoua zaidi ya vikosi 100, shabaha ya sinema hiyo ni kuonyesha udhaifu na kushindwa kwa vikosi katika shambulio hilo, na kwa upande mwingine kuonyesha mafanikio ya Al-Shabaab katika shambulio hilo (PBS, 2016). Mfano wa tatu wa mkakati huu wa simulizi unaweza kuonekana kwenye propaganda iliyotolewa kwenye redio ;Radio Andalus katikati ya Januari 2013 baada tukio la kumuokoa mateka wa Kifaransa Denis Allex kushindikana. Ujumbe uliotolewa mara tu baada ya jaribio hilo ulisema "ushindi unajidhihirisha kwenye shambulio"na kuonyesha uwezo wake na mamlaka ya kutenda (Sikorski, 2014).

   Mfano mwingine wa simulizi ya kisiasa ni ule wa tamko la Allied Democratic Forces ulioeleza nia ya kundi hilo ni kuipindua serikali ya Uganda, na ukaonya ya kuwa mtu yeyote anayemuunga mkono Rais Museveni atauwawa au ndugu wa familia yake. (Titeca & Vlassenroot, 2012). Hivyo hivyo, kundi la Lord's

[7] Kwa rejea nzuri ya mabadiliko ya mbinu za Al-Shabaab katika mikakati yao ya habari kwa muongo uliopita, tizama taarifa ya Hate Speech International (Anzalone, 2016a).

Resistance Army (LRA) lilidai ya kuwa kutokuwa na usawa wa kiuchumi na kijamii kwa watu wa Uganda Kaskazini, na udhaifu wa serikali kushindwa kutoa huduma za jamii, yalihalalisha uasi (Jackson, 2002). Nje ya Rwanda, kundi la waasi la "Forces démocratiques de liberation du Rwanda" (FDLR) linajaribu kuwashawishi wakibimbizi wa Kinyarwanda wanaoishi nchini DRC kuwa serikali ya Rwanda inawanyanyasa Wahutu, na inawapasa kuchukua silaha kupambana dhidi ya serikali ("Democratic Front for the Liberation of Rwanda," 2015).

**2. Vita dhidi ya Uislamu**

Simulizi kubwa inayotumiwa na Al-Shabaab ni kuhamasisha hamasa ya vurugu "jihad" dhidi ya serikali za Ulaya, Somali na Umoja wa Majeshi ya Kulinda Amani Somalia (AMISOM). Kama Timothy Sikorski (2014, uk. 10) anavyoeleza, aina hii ya simulizi inahusisha "Kuonyesha matendo ya mataifa ya Ulaya, serikali ya Somali, na AMISOM kuwa sehemu kubwa ya vita dhidi ya Uislamu, huku serikali za pembe ya Afrika zikiwa na maslahi na nchi za Ulaya." Ifahamike ya kuwa, vita vya porini vya Al-Shabaab na Ethiopia zimesaidia kuhalalisha usemi huu, ikidhihirisha ya kuwa Waethiopia "walikuwa wanafiki wa nchi za Ulaya 'maadui wa mbali' wenye nia ya kushambulia Uislamu" (Ibid). Hii inaonyeshwa zaidi na sinema za propaganda kwa muda wote wa uwepo wao ambapo imeshawishi mashambulio kufia dini dhidi ya walengwa wa Ulaya, Serikali ya Mpito ya Shirikisho (TFG), AMISOM, au Jeshi la Ethiopia (Anzalone, 2016a).  Kwa simulizi hili la kipekee, madhara ya kujitoa kwa majeshi la AMISOM yanaendelea kutizamwa kutokana na mbinu za propaganda zilizotumiwa na Al-Shabaab.

**3. Kuanzishwa kwa "Dola" la Kidini.**

Kipekee hutumiwa na Al-Shabaab, hoja hii husisitiza kuanzishwa kwa dola lililojikita kwenye kanuni za Kiislamu na "sharia". Kwa mujibu wa historia, Al-Shabaab huchukua itikadi yake mahususi kutoka kwenye Mahakama za Umoja wa Kiislamu (ICU), ambayo iliundwa kama "serikali isiyo ya halali ikiwa na baadhi ya mfanano wa sheria na kanuni kupitia utekelezaji mkali wa sharia kwa sehemu kubwa ya Somalia isiyotawaliwa " (Sikorski, 2014, u. 10). Kulingana na taarifa ya mwaka 2016, "simulizi kwenye sinema za Al-Shabaab pia zinakuza dhana ya serikali ya 'Uislamu' kamili yenye uwezo wa kuwakilisha na kutetea maslahi ya Waislamu kitaifa, kikanda na kiulimwengu " (Anzalone, 2016a, U. 10).

Majeshi ya Allied Democratic Forces (ADF) ya nchini Uganda yalianzishwa pia katika muktadha wa Wapigania Uhuru Mujahidin wa Uganda ambao waliamua kulipiza kisasi dhidi ya maamuzi ya mahakama ya Uganda ya mwaka 1992 na kuhitaji kuanzisha taifa la Kiislamu lililo huru dhidi ya ubaguzi kwa jamii ya Waislamu wa Uganda (Weeraran-te, 2017).

Ifahamike hapa ya kuwa propaganda za Daesh[8], ambazo zimejikita kwenye uundaji wa taifa la kiislamu huko Syria na Iraq, zimejaribu kuajiri watu wa Afrika Mashariki. Kwa mfano, sinema ya mwaka 2015 ilihusisha Wasomali wanne na Muethiopia mmoja ikiwataka Wasomali wajiunge na Daesh, wakirejea uonevu uliofanywa na "Wakristu wa Kiethiopia[9]." Hata hivyo, kumekuwa na mafanikio kidogo ya Daesh kuajiri watu kutoka Afrika Mashariki kujiunga na nia yao, licha ya kwamba, muhubiri mashuhuri wa Al-Shabaab alihama mwaka 2015 (Anzalone, 2016b).

Kwa hali kama hiyo, mizizi ya itikadi ya LRA inaweza kufuatiliwa kutoka kwenye Harakati za Roho Mtakatifu za Alice Lakwena, harakati za kiroho na kijeshi zilizolenga kutakasa watu na kuanzisha njia mbadala ya maisha. Kama Beevor (2017) alivyobainisha, dira ya baadaye ya LRA yenye imani ya kidini zaidi kuliko dira ya Al Qaeda au Daesh, ambayo ni ya utabiri mbaya wa mwisho wa dunia.

[8] Taarifa hii inamaanisha kundi la kigaidi kama Daesh, Kifupi cha Kiarabu ikimaanisha "ad-Dawlah al-Islamiyah fi 'l-Iraq wa-sh-Sham" (Dola ya Kiisilamu ya Iraq na Levant).

[9] Tizama "Ujumbe kwa Waisilamu Somalia," Ofisi ya Habari ya Wilayat al-Furat, ilitolewa mwezi Mei 21, 2015, huko Anzalone, 2016a.

Kwa maneno mengine, LRA wanaamini wao “Wamechaguliwa na Mungu, kuhakikisha kwamba njia ya wenye haki inaushinda uovu” (Rinehart, 2006, u. 23). Hivyo basi, simulizi za LRA sio za mtu wa kawaida ila ni za kundi mahususi la dini ambao ni wasafi kiroho.” Wanajamii hawa walitambulika kama “Acholi Manyen” au “Acholi wapya” (Titeca & Vlassenroot, 2012, uk. 65). Kulingana na wafuasi wa Joseph Kony, mamlaka ya uongozi wake yalipata uhalali kutokana na Amri Kumi za Mungu na chini ya uongozi wa “Roho Mtakatifu” ambapo kwa kadiri ya wafuasi wake, alikuwa ndani yake (Beevor, 2017).

## Simulizi za Jamii na Binafsi

1. **Kuajiriwa kwa nguvu na kulazimishwa**
   Kwa muktadha wa Afrika Mashariki, wazo la kulazimishwa kujiunga kwenye kundi la kigaidi sio la kupuuzwa. Al-Shabaab mara nyingi hutumia vitishio vya vurugu kuogopesha watu ila pia huajiri watu wapya kwa nguvu. Kwa mfano, mwaka 2017, inasemekana Al-Shabaab walikutana na wanaukoo kutoka Bay na Bakool Kusini Magharibi mwa Somalia kutambua na kukutana na kundi maalum la vijana lenye umri kati ya 9-18 kupewa elimu na mafunzo chini ya uongozi wa Al-Shabaab (Maruf, 2017). Hivi karibuni Umoja wa Mataifa umeeleza wasi wasi wao kutokana na kampeni kubwa ya Al-Shabaab ya kuajiri wanajeshi watoto kwenye barua ya mwaka 2017 iliyopelekwa kwa Rais wa Baraza la Ulinzi (UN Security Council, 2017). Hata hivyo, hilo sio jambo jipya, kwani inasemekana Al-Shabaab waliwateka nyara mabinti wadogo ili waolewe na wapiganaji wao tangu mwaka 2010 (Spillus, 2012).

   Kwa mujibu wa historia, kundi la LRA mara nyingi waliwateka nyara watoto wa Kiacholi na kuathiriwa na kundi kutokana na vitisho vya kisaikolojia na kimwili. Mazoea ya mara kwa mara yalikuwa ni kuteka nyara mateka wapya na kuua mwanachama wa kundi lao. Kama Beevor (2017, uk. 504) alivyoainisha, “Kuuwa rafiki inaogopesha kuwa na wazo la kurudi nyumbani. Kuna matokeo ya kiroho pia. Kwenye miiko ya Kiacholi, kuua humchafua muuaji na gharama ya mauaji, kutokewa na roho ya marehemu, na kumletea bahati mbaya mhusika.” Kutokana na mahojiano ya aliyewahi kuwa mwanajeshi mtoto, vipigo vilikuwa vya kawaida kwa mateka wa kundi la LRA ili kuleta uoga na kusimika nguvu ya mfumo (Veale & Stavrou, 2007). Zaidi ya hayo, makamanda wa LRA mara nyingi walitishia vurugu au kifo dhidi ya wanafamilia za waajiriwa kwa wale ambao hawakuzingatia amri ama matakwa ya kundi (Peel, 2015).

2. **Kivutio cha vurugu au nguvu.**
   Pale ambapo fursa za kijamii na kiuchumi ni chache, simulizi nyingine yenye nguvu ya magaidi au makundi ya waasi katika ukanda ni kivutio cha vurugu au kupata nguvu. Kwa mfano, wataalamu katika warsha ya Kigali walibainisha ya kuwa vijana wa Kikenya waliajiriwa na Al Shabaab baada ya kupatiwa pikipiki. Pikipiki ilionekana kama ishara ya nguvu, na ilimpatia kijana wa Kikenya hadhi fulani katika jamii.

   Maelezo kama hayo yalitolewa na taarifa ya utafiti na Taasisi ya Masomo ya Usalama (ISS), kwamba upatikanaji rahisi wa silaha ndicho kilichowavutia zaidi vijana kujiunga na ufurutu ada: “Silaha ndogo ndogo zinaweza kuwa ishara ya hadhi na njia ya kudhihirisha nguvu ambazo huwavutia vijana kwenye uhalifu na harakati za upinzani” (Ikelegbe & Okumu, 2010).

   Kwa kundi la LRA, mateka hatimaye walitoa taarifa ya kuridhika na heshima baada ya kupata uaminifu wao katika kikundi, na walivutiwa na nguvu ya kisiasa na kiroho ya kiongozi wao (Beevor, 2017). Wakati huo huo, kutokana na mahojiano na wanachama wa zamani wa LRA, wapiganaji wazuri walipandish-

wa vyeo, hivyo hata kama mtu aliajiriwa kwa nguvu na kundi la LRA, hatimaye wanapata maana kwenye matendo ya vurugu kama njia ya kupata nguvu na mamlaka ndani ya kundi (Peel, 2015).

### Simulizi za Kikabila na Kimila

Wafurutu ada na makundi ya wapiganaji ya Afrika Mashariki wanatumia udhaifu uliopo wa utengano wa muda mrefu wa makabila na makundi ya kimila ndani ya jamii kama njia ya kupata ufuasi.Mfano wa wazi unaweza kutoka kwenye mauaji ya Rwanda yaliyowatenga Wahutu wengi kutoka kwa Watutsi wachache ambapo wahusika wa mauaji walihalalisha mauaji ya Watutsi kulingana ukabila na viashiria vya mwili. Mtangulizi wa mauaji, Wakoloni wa Kibelgiji waliwagawa watu wa Rwanda kama Wahutu, Watutsi au Watwa kwa kuwapima urefu na ukubwa wa pua na umbo la macho (Fornace, 2009).Ubaguzi kati ya makabila tofauti uliotokea takribani miaka 60 iliyopita na kudumu kwa muda mrefu, na licha ya kwamba mauaji hayakutokana moja kwa moja na sababu za kikabila, simulizi za kikabila zilivumilika kwa kipindi chote cha historia na zilitumika kuhalalisha mauaji makubwa ya Watutsi (na wale waliowasaidia) yaliyofanywa na Wahutu kwa kipindi chote cha mauaji kati ya miaka ya 1990.

Al-Shabaab pia wanatumia udhaifu uliopo wa utofauti wa makabila kuwafikishia ujumbe wa propaganda watazamaji wa sinema zao. Kwa mfano, Al-Shabaab huonyesha utengano wa kihistoria uliofanywa na nchi za Ulaya kwa kuigawa Somalia katika ukanda wa Ogaden uliopo Ethiopia na mkoa wa Kaskazini Magharibi nchini Kenya, na hujumuisha yote haya na ubaguzi wa Waislamu uliopo katika nchi zote hizi mbili, kama namna ya kuonyesha malalamiko yanayowalenga jamii husika (Anzalone, 2016a).

Kwa kiwango hicho, kundi la ADF la Magharibi Uganda waliwahamisha wanaharakati waliobaki wa Rwenzururu na Jeshi la Taifa la Ukombozi wa Uganda (NALU),ambao walitumia mvutano uliopo kwenye utawala wa ndani na kukataa utawala wa serikali ya Uganda unaopingwa na utawala wa Rwenzururu (Titeca& Vlassenroot, 2012). Baadae, kundi la ADF waliyachukua malalamiko ya nchi mwenyeji (sasa Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo) na kupata walau ufuasi kidogo kutoka kwa Wakongo ili kuendelea kuwepo.

### Simulizi za Kidini na Kiitikadi

Wakati makundi mengi Afrika Mashariki wanatumia simulizi za kidini na itikadi kuhalalisha malengo yao ya kisiasa na matendo yao ya vurugu, hoja za kidini zilizojikita kwenye theolojia hazina ushawishi kwa kiasi kikubwa kwa waajiriwa Afrika Mashariki. Utafiti uliofanywa na Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP) umetambua ya kwamba, kwa wale waliohojiwa (ikijumuisha baadhi ya washirika wa zamani wa Al-Shabaab na Boko Haram), wengi wa walioshiriki kwenye ufurutu ada walikuwa na kiwango kidogo sana cha elimu ya dini na maarifa machache ya Qur'an kuliko kundi la viongozi (UNDP, 2017, uk. 49-50). Kwa kuzingatia hili, utafiti huu unaeleza ya kwamba, "Imani isiyobadilika kuwa ni ukweli mtupu na kuwafundisha watu kukubali imani bila kuhoji, kuliko elimu ya kina ya dini, inaweza kushawishi kuajiriwa" (Ibid, uk. 50). Hoja yamsingi hapa inaweza kuwa, simulizi za kidini na kiitikadi zinazotumiwa na Al-Shabaab, kwa mfano, mara nyingi hazifuati mpangilio wa hoja za theolojia kushawishi watu, ila hutengeneza mazingira yanayoruhusu vurugu zilizojikita kwenye ushawishi wa hisia na kiroho. Mifano mbalimbali ya hoja ya dini na itikadi imeainishwa hapa chini:

1. **Mamlaka yenye Haki na Kundi lenye uwezo wa Kidini.**
   Dhima ya kuwa kundi lenye uelewa mpana juu ya dini kuliko watu wengine ni

tabia iliyopo kwa makundi yote ya ufurutu ada kwenye ukanda huu. Kwa kuzingatia hili, Al-Shabaab huwaona wale wasiokubaliana nao kama "makafiri" au "walioasi imani" hii huwafanya watu waliokuwa katika mazingira magumu kutokuwa na imani juu ya mafundisho ya dini zao (UNSOM, 2017). Kwa kudai wanamamlaka ya kimaadili ya dini, kwa kuzingatia ukosefu wa maarifa ya dini (kama ilivyoelezwa hapo juu), Al-Shabaab wanaweza kudai ya kuwa matendo yao yanamaadili makubwa zaidi "yenye uhalali zaidi." Hili linaweza kuonekana pia kwa kukuza imani kali sana za dini, zinazotekelezwa kwa kupitia adhabu za kidini au "adhabu kali za kuuwawa kwa kupigwa mawe au kukata viungo vya mwili" (Anzalone, 2016a).

Kwa hali kama hii, wafuasi wa Kony kwenye kundi la LRA walihusisha vurugu za mauaji na uharibifu sawa na haki. Sambamba na hili, mateso yaliruhusiwa kwa sababu lengo ilikuwa ni "kutakasa" utamaduni na watu kutoka dini na tamaduni "chafu"[10]. Dini na tamaduni za mila zilitekelezwa kwa ukali sana, na walioenda kinyume walipatiwa adhabu kali sana, mara nyingi ikiwemo kifo.

2. **Vurugu za Kuchukiza "Jihad".**
   Kulingana na taarifa ya mwaka 2016 iliyotolewa na Hate Speech International, mizizi ya itikadi ya Al-Shabaab ya "jihad" inapatikana kwenye kampeni yao ya mwaka 2008 "Hakuna Amani Bila ya Uislamu" inayotoa tafsiri dhaifu kwenye aya ya al-Anfal,inayoruhusu vurugu dhidi ya 'maadui wa Mungu' wakati wowote na mahali popote (Anzalone, 2016).

   Hoja nyingine inatafsiri dhana ya "jihad" kama njia ya kumsaidia Muislamu mwenzako kwa kuingia vitani. Kwa mfano, kwa maelezo ya Mkenya aliyewaki kuwa mshirika wa Al-Shabaab, waajiri wa Al-Shabaab walimfanya mtu ajihisi kuwa sio Muislamu kamili kwa sababu hawakuwa wakipigana dhidi ya adui aliyekuwa akiwashambulia Waislamu duniani kote (Meleagrou-Hitchens, 2012). Vile vile,sinema iliyoelezea shambulio la Maduka ya Westgate ilionyesha ubaguzi wa Waislamu uliofanywa na serikali ya Kenya kama moja ya sababu ya shambulio la Westgate(Anzalone, 2016a).

3. **Kuhama ili Kuanzisha Dola la Kiislamu**
   Mahususi kwa Al-Shabaab, kundi linakuza dhana ya kufanya "Hijrah"(kuhama) kujiunga na kundi lao Somalia. Wakati hoja hii inaweza kuwa na mashiko kidogo kwa wale waajiriwa wa Al-Shabaab kutoka nchi za Magharibi, kama vile kutoka Marekani na Ulaya, dhana hii bado inatumika kuwaajiri watu kutoka Kenya, Tanzania, Ethiopia au Uganda. Kwa mfano, wapiganaji wengi kutoka Afrika Mashariki wakiwamo Wakenya na Watanzania wamehusishwa na sinema za propaganda hizi huku sinema hizi zikiwa na tasfiri ya maneno kwa Kiswahili, Kiarabu na Kiingereza, na kumekuwako na ongezeko la propaganda za Kiswahili zilizotolewa na Al-Shabaab tangu mwaka 2013 (Anzalone, 2016b). Kwa mujibu wa Sikorski(2014), dhana ya Al-Shabaab "Hijrah"chimbuko lake ni itikadi ya Al Qaeda na ni moja ya sababu kwanini Al-Qaeda wameidhinisha Al-Shabaab kujihusisha kwenye mapambano yakidunia ya jihad.

## Simulizi za Kiuchumi

Simulizi za kiuchumi zinaweza kuonekana katika sehemu mbalimbali ikijumuisha ahadi za zawadi ya fedha, upatikanaji wa vitu au vitu vya kula, au fursa za kazi au ajira. Mbinu zote hizi zimetumika na Al-Shabaab kama njia ya kuajiri vijana kwenye kikundi chao. Kwa mfano, taarifa ya Kituo cha Kimataifa cha Masomo ya Ushawishi na Vurugu za Siasa (ICSR) kilieleza kuwa Al-Shabaab iliahidi pesa za Kenya 40,000 (500 Dola za Kimarekani) kwa mwezi kama mshahara wa washirika,

[10] Kutokana na majadiliano na Kenneth Bana, Kamanda mkuu wa zamani wa LRA, huko Beevor (2017).

ambayo ni mara nne ya kiwango cha mshahara wa kitaifa kwa wakati ule (Meleagrou-Hitchens, 2012). Al-Shabaab imeelezwa pia kutoa simu bure kama njia ya kushawishi waajiriwa wapya, ambazo walitumia kuajiri wahusika (UNSOM, 2017). Zaidi ya hayo, washiriki katika warsha ya Kigali walitoa mifano kutoka Kenya ambapo Al-Shabaab waliahidi kutoa pikipiki kwa wale ambao wangekuwa tayari kujiunga na kundi lao. Zaidi ya hayo, utafiti wa Ujumbe wa Msaada wa Umoja wa Mataifa nchini Somalia (UNSOM) umeeleza ya kuwa, ukosefu wa ajira ni kichocheo muhimu cha kuajiriwa na Al-Shabaab kwa sababu inatengeneza " hitaji la uchumi na muda wa kutosha wa mapumziko " (UNSOM, 2017, u. 15).

## 4 WEKA LENGO NA SHABAHA MAHUSUSI YA SIMULIZI KINZANI

Baada ya kutathimini mazingira husika na mambo muhimu ambayo simulizi kinzani itahusika nayo, hatua nyingine ni kutambua malengo na nia ya simulizi kinzani na kampeni yake. Malengo na nia yanapaswa kuelezea kwa uwazi mabadiliko ya tabia au mtazamo ambao unategemewa kutoka kwa walengwa waliotarajiwa. Walengwa hawa kusudiwa walitambuliwa katika hatua ya pili. Mfumo ufuatao hapo chini unaelezea nia na malengo ya ukanda wa Afrika Mashariki (Zeiger, 2016, u. 12; El Sayed, Faris & Zeiger, 2017, u. 14).

### KUJIONDOA

Lengo hili linajikita kubadilisha tabia pale ambapo mhusika atapunguza ama kuacha kujihusisha na shughuli za ufurutu ada. Vipimo vya kujiondoa vinaweza kuonekana kwenye mazingira ambayo simulizi kinzani zinatolewa ana kwa ana, kuliko mtandaoni. Kama kazi ya simulizi kinzani Afrika Mashariki ni vyema zaidi ikafanyika ana kwa ana, lengo hili linaweza kuwa na uhalisia zaidi katika ukanda huu kuliko ukanda mwingine.

### KUEPA

Lengo hili linajikita kuzuia watu mwanzo kabisa kutokuwa na nia ya ufurutu ada, na badala yake kuwageuza kwenye njia nyingine mbadala za kueleza mawazo na malalamiko yao.

### UHAMASISHAJI

Lengo hili linahitaji kutoa taarifa zinazohusiana na baadhi ya mambo ya ufurutu ada. Hii inajumuisha taarifa kuhusu vichocheo na michakato ya ushawishi. Lengo hili linaweza kutumika zaidi walengwa waliokusudiwa wakiwa "washawishiwakuu."

### KUZUIA ATHARI

Lengo hili linajikita kutenga simulizi au propaganda za wafurutu ada kupunguza athari kwa watu au makundi madogo. Hii inaweza kuwa sahihi pindi ujumbe wa wafurutu ada unaweza kuwa na mvuto kwa walengwa wengi.

### KUDHOOFISHA MVUTO

Lengo hili linajikita kuondokana na mvuto kwa watu wanaoishi kwenye mazingira magumu, ikiwamo kuharibu simulizi au ujumbe wa wafurutu ada ili usiwe na mvuto.

## KUPIMA MATOKEO YA SIMULIZI KINZANI

Kuanisha malengo mahususi kwa ajili ya simulizi kinzani ni muhimu kwa ajili ya kupima ufanisi wake. Ni muhimu kuainisha malengo kuwa madogo au vijilengo vidogo zaidi ambavyo yanaweza kupimika na yenye uhalisia. Ni muhimu pia kuzingatia viashiria mahususi ambavyo vinaweza kutathiminiwa na kupimwa kwa muda mrefu. Kwa taarifa zaidi juu ya kupima matokea ya simulizi kinzani na kampeni, tizama hatua ya 9.



### Kisa Mkasa kwa Malengo na Nia

Sinema ya Watatu, Kenya

Maelezo:

Watatu ni sinema iliyoigiziwa Mombasa, Kenya inayotoa simulizi la vijana watatu waliojihusisha na ufurutu ada : vijana hao ni Yusuf, Salim, na Jack. Yusuf anashawishiwa na kundi la wafurutu ada, na mjomba wake Salim anahangaika kumfanya akatae itikadi la kundi hilo. Jack, ambaye ni askari polisi, anajaribu kujenga uaminifu na Yusuf ili kumzuia kufanya shambulio. Sinema hii inabadilika na kuwa igizo la jukwaani, ambapo waigizaji wanaigiza mubashara simulizi iliyobaki, huku wakipata maoni kutoka kwa watazamaji. Waigizaji wanapewa fursa ya kufanya maamuzi ya wahusika wakuu kubadilisha matokeo ya hadithi.

Kwa taarifa zaidi kuhusu Watatu, tizama SAFE Tovuti ya Kenya :

http://safekenya.org/watatu/

**HATUA 1**

TATHIMINI SABABU ZA KUSUKUMA NA KUVUTA

Sababu za Kusukuma:
Kukosa ajira, mahusiano dhaifu kati ya huduma za usalama na jamii, mauaji yasiyofuata sheria yanatendwa na askari polisi.

Sababu za Kuvuta:
Itikadi, hali ya utambulisho na madhumini

**HATUA 2**

KUTAMBUA WALENGWA WALIOKUSUDIWA

Walengwa wa Jumla:

Walengwa waliokusudiwa ni Jamii ya Mombasa, ikiwalenga zaidi vijana.

**HATUA 3**

KUTAMBUA SIMULIZI ZA UFURUTU ADA ZINAZOPINGWA

Kulingana na sinema hii, simulizi inayotumiwa na wafurutu ada ni kwamba askari polisi na vyombo vya usalama vimeshindwa kulinda jamii yao, na serikali imeshindwa kutoa fursa za ajira kwa vijana wazawa kutoka Mombasa na fursa hizo wanapewa kipaumbele Wakenya kutoka "vijijini".

**HATUA 4**

KUWEKA MALENGO NA NIA DHAHIRI

LENGO 1

Kuhamasisha juu ya matatizo na simulizi za wafurutu ada kwenye jamii ya Mombasa kati ya walengwa wa jumla.

LENGO 2

Kudhoofisha mvuto wa simulizi za wafurutu ada kwa kuonyesha ya kwamba vyombo vya dola na usalama vinaweza kufanya kazi pamoja kwenye jamiii ya Mombasa.

LENGO 3

Kuzuia athari za simulizi za wafurutu ada kwa kuonyesha madhara hasi ya familia za wale wanaojiunga na ugaidi.

## 5 AMUA MJUMBE MFANISI

Baada ya kuweka malengo na nia ya simulizi kinzani, ni muhimu kuamua mjumbe au wajumbe ambao watafikisha ujumbe. Wataalamu walioshiriki warsha mjini Kigali walisisitiza ya kwamba, wakati wa kuzingatia mjumbe, sifa na tabia za mtu kama vile tamaduni, kabila na dini ni muhimu kuzingatia.

**MASWALI YA KUAMUA MJUMBE SAHIHI**

- Nini mahusiano baina ya mjumbe na walengwa waliokusudiwa ?
- Nini uhalali wa mjumbe na walengwa waliokusudiwa ?
- Nini uwezekano wa mjumbe kubadilisha mtazamo ?
- Nini uwezekano wa mjumbe kubadili tabia ?
- Ni athari zipi au hatari zinazohusika kwa kumchagua mjumbe mahususi ?

*Nakala ya mwanzo kutoka kwa El Sayed, Faris & Zeiger, 2017*

### Vijana (Rika-kwa-Rika)

Kwa muktadha wa Afrika Mashariki, vijana wanamchango mkubwa sana kwa jamii na wanajumuisha idadi kubwa ya watu. Kulingana na taarifa ya Umoja wa Afrika, zaidi ya asilimia 60 ya watu wa Afrika Mashariki wako chini ya miaka 30 (Ababa, 2017). Kwa kweli, "Harakati al-Shabaab al-Mujahideen" (jina rasmi la Al-Shabaab) linamaanisha "harakati za vijana wanaojitahidi au kupambana," ikieleza ya kuwa, Al-Shabaab inalenga vijana kutimiza malengo yao. Kwa kuongezea, rika na mitandao ya jamii inajukumu kubwa sana kutengeneza utambulisho na kuleta hali ya umoja, taratibu muhimu za kuimarisha katika muktadha wa kuzuia kuajiriwa na makundi ya wafurutu ada. Hata hivyo, viongozi vijana wanaweza kuwa wachochezi muhimu wa mabadiliko chanya na kuwazuia vijana wenzao kujiunga na makundi ya kigaidi.

Mfano wa ujumbe wa rika-kwa-rika unatoka katika muktadha wa Burundi unapatikana kupitia www.ivomo.net. Katika tovuti hii, vijana wanaweza kuanzisha mazungumzo baina yao wenyewe kuhusu mada zenye umuhimu kwenye jamii yao. Mfano kama huo ni kupitia YADEN Jukwaa La Fursa kwa Vijana Afrika Mashariki. Katika jukwaa hili la ana kwa ana, vijana nchini Kenya wanaweza kujenga jamii, kujenga hali ya umoja na utambulisho wa pamoja, na kujenga mfumo wa kupata fursa sahihi kwa mabadiliko yenye maana katika jamii yao, na kutengeneza nafasi ya kutengeneza na kubadilishana ujumbe wa mabadiliko baina yao.

Mfano wa tatu wa kijana kama mjumbe ni kwa kupitia Kampeni ya Harakati Dhidi ya Ukabila "Acha waisikie Sauti Yako"[11]. Kampeni hii ilihamasisha vijana wa Kisomali kuelezea hisia zao kuhusu mgawanyo wa makabila katika jamii zao ambao ungeweza kuoneka kwa wagombea urais wakati wa uchaguzi. Matokeo yalipelekea vijana wa Kisomali kutengeneza sinema ya sekunde 30 wakitoa maoni ya suluhisho ya malalamiko ya jamii yao.

### Wahanga na Majeruhi

Wahanga na majeruhi wa mashambulio ya ugaidi, au wanafamilia wa wahanga wa ugaidi wanaweza kuwa wajumbe imara sana wanaoweza kugusa hisia za wa-

[11] Sinema ya "Acha wasikie sauti yako" kampeni inaweza kutazamwa kwenye You Tube hapa: https://www.youtube.com/watch?v=rh1jAucXv0Q



## KUMJARIBU MJUMBE NA KUNDI LENGWA

Kama kuna fursa ya kufanya hivyo, inashauriwa kumjaribu mjumbe na kundi la walengwa kabla ya kufanya kampeni. Hii inaweza kufanywa kwa kupita majadiliano ya kundi. Kujaribu namna mjumbe anavyodhaniwa na walengwa tarajiwa inaweza kuzuia matokeo yasiyotarajiwa kwenye kampeni au kudhihirisha tabia za mjumbe ambazo zinaweza kusaidia kwenye kampeni.

husika tarajiwa kwa kuonyesha madhara ya ugaidi. Mfano wa kuunganisha hadithi za wahanga na wajeruhiwa unatumika Rwanda na Burundi kwenye eneo la kuzuia mauaji ya halaiki na elimu. Kwa mfano, kwenye sanaa ya kubadili mtizamo iliyobuniwa na Pieter Hugo, picha za majeruhi wa mauaji ya Rwanda ziliunganishwa na wahusika wa vurugu kwa pamoja zikihusisha simulizi zao binafsi zikionyesha maridhiano na msamaha wa jumuia (Ruby & Taylor, 2014). Vivyo hivyo, Makumbusho ya Mauaji iliyopo Kigali inajumuisha chumba chenye nguo za baadhi ya wahanga wa mauaji, na sinema fupi ya baadhi ya wajeruhiwa na uzoefu wao. Mfano mwingine ni mpango wa Never Again Rwanda, ambapo "nafasi ya amani" huleta pamoja wajeruhiwa na wahusika wa zamani kujadili uzoefu wao na kuelewana hali zao. Nafasi hizo ni kwa vikundi vilivyofungwa, ila uzoefu na hadithi zao husambazwa kwa watu mbalimbali bila kutaja majina kama mfano wa maridhiano ili kuzuia mauji mengine hapo mbeleni (Kezio-Musoke, 2017).

## Viongozi wa Dini

Viongozi wa dini wanauwezo wa kushawishi walengwa husika hususani wakati ambapo maudhui yamelengwa zaidi kwenye hoja za dini ua itikadi. Mfano nje ya Afrika Mashariki ni mradi unaoendeshwa na Kituo cha Kimataifa cha Cairo cha Utatuzi wa Migogoro, Kulinda na Kujenga Amani (CCCPA) kinachofundisha wanawake, vijana na viongozi wa dini juu ya maudhui ya simulizi kinzani. Kwenye mafunzo haya, washiriki hujifunza kuhusu ujumbe gani wa dini ni madhubuti zaidi kukizana na hoja za dini za Al-Shabaab, hasa ukijikita kwenye tafsiri ya "jihad," "takfir," "Jahiliyyah"[12] na dhana nyinginezo za Kiislamu pamoja na madai ya kwamba Al-Shabaab inatokana na heshima kwa nabii na wafuasi wake.

Kwa kuongeza, viongozi wa dini wanaweza kuwa vielelezo vya mwingiliano kati ya madhehebu au dini kama njia ya uvumilivu na amani. Kwa mfano, kundi la wakuu wa dini ya Sufi300 walikutana Afrika Mashariki mwaka 2015 kujadili ufurutu ada na kutoa tamko dhidi ya ugaidi (Abdi, 2015). Kwenye ukanda ambao maadili ya Sufi yanaendana pia na tamaduni za jamii na makabila, uongozi wa wahubiri wa dini ya Sufi kwenye suala hili huleta matokeo chanya muhimu kwenye jamii.

Wataalamu waliokutana kwenye warsha mjini Kigali walitafakari changamoto za kufanya kazi na viongozi wa dini kwenye ujumbe kinzani. Kwa kuzingatia hili, ilielezwa ya kwamba mara nyingine viongozi wa dini hawajaunganishwa sana na kundi la vijana Afrika Mashariki, kwani wengi wa wahubiri hawa ni wa kizazi cha zamani. Kutatua changamoto hii, shirika la Muungano wa Vijana wa Kiislamu Uganda linajikita kwenye mafunzo na kuwashauri viongozi vijana, ikiwamo kuandaa mikusanyiko ya dini mbalimbali na vizazi tofauti ya wanafunzi na viongozi wa dini (Allied Muslim Youth Uganda, 2017). Njia nyingine inayoweza kutatua changamoto hii ni kujenga maarifa na uwezo wa viongozi vijana wa dini ambao wanaweza kuwa wameonganishwa zaidi na vijana.

## Wasaliti na Washirika wa Zamani

Watu waliowahi kushiriki kwenye ufurutu ada na ugaidi na walioondoka kwenye makundi hayo wanauwezo wa kuwa wajumbe imara sana kuzuia wengine wasijiunge na makundi hayo (Ashour, 2010). Taarifa ya Neumann (2015) inaeleza ya

[12] "Jihad" ni dhana ya kiislamu inayomaanisha "Mapambano." "Takfir" ni dhana ya Kiislamu inayomaanisha kumtangaza mtu asiye na imani. "Jahiliyyah ni dhana ya Kiislamu inayomaanisha muda Fulani kabla ya Uisilamu, wakati ulimwengu ulivyokuwa na "ujinga."

kuwa wasaliti kutoka Daesh wanaweza kutoa ujumbe muhimu wa aina nne ambayo unaweza pia kutumia kwa muktadha wa Al-Shabaab: 1) kuonyesha utengano na mapigano ya ndani ya kundi; 2) kudhihirisha ukatili dhidi ya Waiislamu; 3) kuanika rushwa na matendo yasiyo ya Kiislamu ya kundi; na 4) kudhihirisha ugumu wa maisha (Neumann, 2015). Kwa muktadha wa Afrika Mashariki, wasichana kadhaa wa Kikenya waliokolewa na jeshi la Kisomali mwaka 2017 na kuwaeleza namna viongozi wa kundi walivyowadhalilisha kingono na kuwashikilia kifungoni. Wasichana ambao mwanzoni walijiunga kwa utashi wao wenyewe, kwa haraka walijifunza ya kuwa kundi halikuwa kama vile walivyotarajia. Kulingana na maelezo ya Halima mwenye miaka 16, "Al-Shabaab ni kundi la wauwaji tu na si vinginevyo. Hakuna Jihad Somalia, ninajuta kuwaunga mkono na kuiacha familia yangu kwa ajili yao" ("Wanaume wa Al-Shabaab wawageuza wasichana wa shule wa Kikenya kuwa watumwa wa ngono," 2017).

Kwa muktadha wa Rwanda, wapiganaji wa zamani wa kundi la FDLR wamejumuishwa kwenye simulizi zinazotumika na kambi ya Mutobo Kusambaratisha na kuunganisha kuwasiliana na wapiganaji wa sasa wa FDLR kama njia ya kuwarejesha kwenye jamii ya Wanyarwanda. Kwa maelezo ya mpiganaji mkuu wa zamani wa FDLR, Brigedia Jenerali Semugeshi Comes, wanachama wa zamani walikuwa sehemu muhimu kwake kurudi nyumbani ambao "walimuhakikishia ya kwamba Rwanda ilikuwa salama na hakuna kitu kingemkuta" (Mugabi, 2017).

### Watendaji wa Jamii na Ngazi ya Chini

Mashirika ya ngazi ya chini na watendaji wa jamii wanaweza kuwa wajumbe wazuri sana kwa sababu ni sehemu ya mahitaji ya jamii na malalamiko, na mara nyingi kama sehemu kubwa ya shughuli zao huyatatua matatizo haya. Kwa Tanzania, mikakati ya Shirika la Global Peace Foundation ni kuendesha kampeni zinazohamasisha jamii kutokuwa na vurugu, kuwa wavumilivu na watu wa amani. Kwa mfano, kampeni ya #VijanaNaAmani ililenga migogoro ya utambulisho kwenye jamii kwa kukuza hadithi za vijana wachapakazi katika jamii zao.

Hata hivyo, kutokana na utafiti uliofanywa na shirika la Search for Common Ground juu ya wahamasishaji muhimu na mitandao Tanzania na Kenya, ilidhihirika ya kwamba makundi ya asasi za kiraia walikuwa wahamasishaji wa chini kabisa ukilinganisha na wajumbe wengine muhimu, ambao ilijumuisha viongozi wa siasa, polisi, viongozi wa dini, walimu na wanafunzi, wafanyakazi, familia na wanarika (Russell, 2017). Kwa mantiki hii, makundi ya asasi za kiraia wananafasi kubwa ya kuwafundisha na kuwapatia taarifa wajumbe ambao wanahamasa kubwa kwa walengwa husika ila hawawezi kuwa wajumbe madhubuti.

### Wanasiasa

Wanasiasa wanajukumu muhimu sana kuishawishi jamii kuwa serikali za Afrika Mashariki zinaongoza vyema nchi zao na kupambana na rushwa, kinyume na hoja zinazojengwa na makundi ya wafurutu ada. Kwa mfano, simulizi ya sinema iliyoandaliwa na Breakthrough Media yenye kichwa cha habari "Meya wa Mogadishu" inaonyesha mfululizo wa maisha ya kila siku ya Meya, ikionyesha chaguzi anazozifanya na namna anavyoongoza mji (Breakthrough, 2016). Simulizi hii ya sinema inasaidia kusisitiza ujumbe wa kuwa serikali ya Somalia ilikuwa inafanya mageuzi makubwa ya nchi na imejitolea kufanya mabadiliko ya kweli kwenye jamii na nchi.

Hata hivyo, ifahamike ya kwamba wataalamu katika warsha ya mjini Kigali walijadili utata wa kuwatumia viongozi wa siasa kupambana na ufurutu ada Afrika Mashariki. Mosi, simulizi za kisiasa zinazoletwa na makundi ya wafurutu ada zikituhumu viongozi wa siasa kwa rushwa na/au kutokuwa na uwezo wa kuongoza kunaweza kuwa na chembechembe za ukweli, ikimaanisha ya kwamba kiongozi wa siasa anayetoa ujumbe wa aina hiyo anakosa uhalali kwa walengwa husika. Pili, maoni ya jamii na mtizamo wa viongozi wa siasa unaweza kubadilika kila siku—ikimaanisha ya kwamba ujumbe unaotolewa na kiongozi wa siasa unaweza kupuuzwa kama mtizamo wa jamii ukiwa hasi. Wakati ujumbe ni muhimu kama kupambana na simulizi za ufurutu ada, ni muhimu kuchagua mjumbe ambaye hataharibu kampeni mbele ya safari.

## 6 TENGENEZA MAUDHUI NA MANTIKI KWENYE UJUMBE

Hatua nyingine ni kutambua maudhui ya ujumbe kinzani unaotolewa. Wataalamu kwenye warsha iliyofanyika mjini Kigali pia walijadili kutumia mbinu ya hatua wakati wa ketengeneza maudhui, ikimaanisha kuwaonesha walengwa kusudiwa maudhui tofauti katika majukwaa tofauti. Kwa taarifa zaidi kuhusu mbinu hii, tizama Hatua ya 7. Aina tofauti za simulizi kinzani zimeelezwa kwa kina hapa chini:

### SIMULIZI CHANYA NA MABADALA

Simulizi kinzani ni ujumbe makini na mbadala wenye kuvutia kuliko ugaidi. Simulizi chanya na mbadala hufanya kazi vyema wakati zikitoa matendo mbadala kuondoa malalamiko. Baadhi ya mifano hii hapa chini:

#### AMANI KWANZA

Amani Kwanza (#AmaniKwanza), ni kampeni iliyokuwa ikiendeshwa na Global Peace Foundation iliyolenga kuweka amani kama kipaumbele namba moja kwa vijana. Kampeni ilihimiza jamii kuongea namna ya kutunza amani wakati wa uchaguzi Tanzania.

Nchi: Tanzania

https://bit.ly/2sal5ec

#### KUNDUBURUNDI

Kampeni hii iliyojulikana kama "Kunduburundi" au "Burundi ya Kuheshimika" iliyoandaliwa na Alkeza.net iliwataka vijana wa Burundi kupenda na kuthamini nchi yao. Kampeni hiyo ilijumisha ujumbe kwenye fulana kuhimiza vijana kupenda nchi yao, kuijenga, kuisaidia, na sio kuiharibu.

Nchi: Burundi

https://bit.ly/2MBWQzV

### SIMULIZI KIZANI ZA KIJAMII

Aina hii ya simulizi kinzani inafaa kwenye sababu za "kuvuta" ambazo zinaweza kumuathiri mtu katika hatua ya hisia au saikolojia. Hii imewahi kuainishwa kama "hisia na kikabila " kwenye NAMNA YA KUONGOZA iliyopita. Ifuatayo ni baadhi ya mifano:

#### MAISHA YALIYOHARIBIWA

Kampeni ya "Maisha yaliyoharibika" inaelezea hadithi za wamama wa wahanga wa mashambulio ya Al-Shabaab. Sinema ya Anti-Tribalism Movement, inataka kujidhihirisha kwenye hisia za watu ambao wanaweza kuwa wanataka kujiunga na makundi ya kigaidi kwa kuonyesha madhara kwa wamama –ambao wanathaminika sana kwenye jamii.

Nchi: Somalia

https://bit.ly/1B1vSK9

#### #KWAMSHIKAMANO

Sinema hii kupitia kampeni ya YADEN #kwa mshikamano, wanawake vijana wawili kutoka kata ya Kwale wanaelezea hadithi zao na uzoefu wao wa ugaidi. Wanaongelea namna vijana walivyoajiriwa na makundi ya kigaidi na hatari zinazoikumba jamii zao kutokana na ufurutu ada.

Nchi: Kenya

https://bit.ly/2t4Yge3

## SIMULIZI KINZANI ZA KIKABILA NA KIMILA

Simulizi hizi zinalenga kuondoa utofauti uliopo wa kikabila na kimila kwa kutafuta suluhisho la pamoja au maslahi ya pamoja. Mfano unafuata hapa chini:

### SUDANI YA KUSINI: MAKABILA MAWILI YAJENGA VURUGU ILICHOBOMOA

Sinema hii ijulikanayo kama "Sudani ya Kusini: makabila mawili yajenga vurugu ilichobomoa," Shirika la Search for Common Ground lilianzisha mpango wa maridhiano kati ya makabila ya Madi na Acholi, ikijumuisha vipindi vya redio na mijadala ya jamii. Sinema inaeleza namna mradi ulivyoleta kwa pamoja wahusika mbalimbali wa jamii kutafuta suluhu ya pamoja kutokana na mvutano wa jamii.

Nchi: Sudani Kusini

https://bit.ly/2lWiikm

## SIMULIZI KINZANI ZA KISIASA

Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya simulizi kinzani inayotatua malalamiko ya kisiasa na itikadi:

### MEYA WA MOGADISHU

Sinema ya "Meya wa Mogadishu" inaangazia maisha ya kila siku ya Meya ikionyesha namna ilivyo kuwa na majukumu ya kuongoza mji. Inasisitiza mawazo ya kwamba serikali ya Mogadishu ina uwezo wa kufanya maamuzi na utawala bora.

Nchi: Somalia

https://bit.ly/2GUsdSf

### HUGUETTE LABELLE

Mwenyekiti wa Bodi ya Uwazi ya Kimataifa, Huguette Labelle, anaiongelea Rwanda kuwa nchi iliyoshika nafasi ya chini yenye kiwango kidogo cha rushwa Afrika mwaka 2013. Kuonyesha ukweli huu wa kisiasa unapunguza uwezekano wa makundi ya ufurutu ada kutumia rushwa kama sababu ya kujiunga nao nchini Rwanda.

Nchi: Rwanda

https://bit.ly/2t4LA78

## SIMULIZI KINZANI ZA KIDINI NA KIITIKADI

Aina hii ya simulizi kinzani inapinga hoja potofu za kidini na kutoa tafsiri sahihi ya maandiko ya dini yasiyokubali vurugu. Ifuatayo ni baadhi ya mifano:

### KUKOSA UVUMILUVU WA KIDINI MOMBASA NA NAIROBI

Mashirika ya Hanns Seidel Foundation na Well Told Story yalichunguza sababu za kukosa uvumilivu wa kidini mjini Mombasa na Nairobi. Waligundua ya kuwa migogoro kati ya Waislamu na Waikristu mara nyingi inachochewa na walio nje. Hii huathiri ujumbe wa wafurutu ada unaotumika kutenga jamii kwa kigezo cha imani. Matokeo ya utafiti na mahojiano yalibadilishwa kuwa maigizo.

Nchi: Kenya

https://bit.ly/2HXmThH

### MAISHA NDANI YA UISLAMU

Imetungwa na Sheikh wa Kiganda Nuwagaba Muhsin Kaduyu, ujumbe wa sinema hii ni sehemu ya 'Maisha ndani ya Uislamu' mfululizo unalenga kuwataarifu Waisilamu wa Uganda namna chanya ya kubadilisha jamii yao. Sinema hii kwa mahususi inalenga ukuaji bora wa watoto kutoka kwenye mtazamo wa Kiislilamu.

Nchi: Uganda

https://bit.ly/2KWQGsz

### MATEMBEZI YA AMANI YA MADHEHEBU KITAIFA

Matembezi ya amani ya madhehebu kitaifa kila mwaka ni tukio kubwa linaloandaliwa na vijana waAllied Muslim Youth Uganda kila Februari wakati wa maadhimisho ya juma la amani la madhehebu la Umoja wa Mataifa. Linaleta kwa pamoja vijana, hususani wanafunzi, kwenye shughuli zinazojenga uaminifu na kukuza maelewano kuelekea lengo moja la ushirika wa madhehebu.

Shughuli zinahusisha : hotuba za hadhara, majadiliano ya baina ya vizazi, Matembezi ya Amani, kuchangia damu, huduma za jamii, michezo ya madhehebu, maongezi ya kuhamasisha majadiliano na ushauri.

Nchi: Uganda

https://bit.ly/2LwJUe4

## SIMULIZI KIZANI ZA UCHUMI NA UFUNDI

Aina hii ya simulizi kinzani inahalalisha sababu za kiuchumi za kutokujiunga na makundi ya kigaidi au uchumi mbadala kama ajira au mafunzo ya kazi. Ufuatao ni mfano:

### KITUO CHA MIGOGORO, UTAWALA NA KUJENGA AMANI

Mfuko wa Uimara ulioanzishwa na Kituoa cha Migogoro, Utawala na Kujenga Amani katika Chuo Kikuu cha Mogadishu. Kituo kinatoa ajira za muda zenye malipo kamili na hutoa pia mafunzo ya kuwaanda vizazi vijavyo vya viongozi nchini Somalia.

Nchi: Somalia

https://bit.ly/2thS3ep
https://bit.ly/2IQRfqr

## 7 TAMBUA NJIA ZA KUSAMBAZA UJUMBE

Utaratibu wa usambazaji wa simulizi kinzani au kampeni ni muhimu sana kuhakikisha ufanisi wa kampeni husika. Njia ya kufikisha ujumbe lazima iwe ile inayowafikia walengwa tarajiwa katika njia rahisi na asili zaidi iwe ile amabayo walengwa tarajiwa hutumia mara kwa mara. Kwa Afrika Mashariki, njia za mawasiliano za mitandaoni sio maarufu ukilinganisha na sehemu zingine duniani, na hivyo njia za mawasiliano nje ya mtandao zinaweza kuwa na ufanisi zaidi inapokuja swala la kupambana na simulizi za wafurutu ada. Kutokana na utafiti uliofanywa na We are Social and Hootsuite, intaneti imepenya Afrika Mashariki kwa 27% na mitandao ya kijamii imepenya kwa 7% (We are Social and Hootsuite, 2018). Kiwango hiki ni cha chini ukilinganisha na kupenya kwa intaneti kimataifa ambayo ni (53%) na matumizi ya mitandao ya kijamii ni (42%), pamoja na kupenya kwa intaneti Afrika (34%) na kupenya kwa mitandao ya kijamii Afrika ni (15%) (Ibid.). Hata hivyo, uwezekano wa ukuaji wa intaneti na matumizi ya mitandao ya kijamii Afrika Mashariki ni mkubwa, hasa kutokana na uwekezaji mkubwa wa miundombinu na biashara kutoka kwenye nchi kama vile China (Kiprop, 2017; Pilling, 2017). Kwa mantiki hii, kampeni za simulizi kinzani lazima zitathimini ukweli wa njia sahihi za mawasiliano za Afrika Mashariki kwa sasa, lakini pia ni muhimu kutizama matumizi ya teknolojia yajayo yenye uwezekano wa kukua katika ukanda huu. Njia sahihi za mawasiliano kwa muktadha wa Afrika Mashariki ni pamoja na:

### USHIRIKI WA ANA KWA ANA

*Kwa Afrika Mashariki, ushawishi na ajira za wafurutu ada mara nyingi hufanyika nje ya mitandao, hasa kwa majadiliano ya ana kwa ana (UNDP, 2017). Tukiliweka hili akilini, ujumbe unaweza kuwasilishwa moja kwa moja kwa mtu muhusika, hii ikimaanisha washawishi wakuu kwenye ukanda huu (kama vile viongozi vijana, waalimu, wazazi nk.) wanahitaji kupewa maarifa na ujuzi kukataa ujumbe wa ufurutu ada katika mazungumzo ya kila siku.*

*Kwa kuongezea mazungumozo ya kila siku, majadiliano ya ana kwa ana yanaweza pia kufanyika katika mazingira yasiyo rasmi sana. Kwa mfano, baadhi ya nchi za Afrika Mashariki, "maskani" ni sehemu ya mkusanyiko isiyo rasmi ambapo watu huchangia mawazo, ni kama sehemu ya mkusanyiko wa majirani "ambapo watu wazima hukutana baada ya saa za kazi kupiga umbea, kunywa kahawa na kucheza bao" (Bakari, 2001, u. 179). Kwa muktadha wa Tanzania, "maskani" zinaweza kuwa za kisiasa, hasa hasa Zanzibar, ila pia zinahusika na makundi au dawa ya kulevya (Russell, 2017). Huko Kenya, "maskani" zinahusika pia na matumizi ya dawa za kulevya (kama vile shisha au kutafuna miraa[13]), ila pia zinaweza kuwa maduka ya chai au vinjwaji baridi. Kwa Tanzania, kuna tabia ya "maskani" kutumika na wazee. Kwa upande mwingine, huko Kenya kuna mchanganyiko wa vijana na wazee ambao hukusanyika "maskani" (Russell, 2017). Pia ifahamike ya kwamba, washiriki wa mikusanyiko ya "maskani" mara nyingi ni wanaume kuliko wanawake (Russell, 2017).*



### RUNINGA, FILAMU NA SINEMA

*Njia nyingine ya muhimu ya kufikisha ujumbe katika ukanda wa Afrika Mashariki inajumuisha runinga, filamu na sinema. Ambapo njia nyingine za kufikisha ujumbe wa mtandaoni hazijafanikiwa, kuonyesha filamu kwenye jamii zikijumuisha ushiriki wa watazamaji au kuandaa mijadala zinaweza kuchangia kupunguza simulizi za wafurutu ada. Kwa mfano, filamu ya Watatu inaelezea hadithi ya watu watatu waliojihusisha na ufurutu ada: Yusuf, Salim, na Jack. Kituo cha Msaada cha Jamii Kenya (KECOSC) kilitengeneza filamu kwa vikao vya vijana 200 Mombasa, ikifuatiwa na mijadala au mijadala iliyoandaliwa kuhusu matokeo ya filamu.*



[13] Kulingana na Russell (2017), Miraa ni jina la asili la Khat, mmea wa kusisimua unaotumika kwenye barala Afrika.

## VIPINDI VYA REDIO

*Redio ni njia muhimu sana ya mawasiliano kwa Afrika Mashariki (Rus-sell, 2017; Sika et al., 2015). Vipindi vya redio ni njia ya awali ya mawasiliano kuhusu mambo muhimu ya jamii na kutoa fursa kwa serikali na mashirika kutoa taarifa kuhusu mu-suala muhimu kama unyanyasaji wa kijinsia, ubaguzi au mambo ya kiafaya. Vipindi vya runinga vya mijadala ni muhimu sana kukuza ushiriki wa wananchi na kuwafikia watu hasa hasa vijijini ambako kuna robo tatu ya watu wa Afrika Mashariki (Sika et. al., 2015, u. 23). Kampeni za ujumbe kinzani zenye mafanikio zinazofanyika kwa kupitia redio ni muhimu zikajumuisha baadhi ya mijadala endelevu moja kwa moja kwenye jamii. Kwa mfano, chini ya usimamizi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake nchini Kenya, wanawake nchini Kenya hukusanyika kwa pamoja katika vikundi vidogo kusikiliza vipindi vya redio juu ya mada wanazozipenda na kujadili mawazo yaliyowasilishwa wakati wa kipindi baina yao wenyewe (Orlale, 2015).*

## MAJUKWAA YA MITANDAO YA JAMII

*Kama ilivyoelezwa hapo awali, majuk-waa ya mitandao ya jamii hayatumiki sana Afrika Mashariki ukilinganisha na kupenya kwa mitandao ya kijamii ulim-wenguni. Hata hivyo, kujumuisha mambo ya mitandao ya jamii kwenye kampeni za simulizi kinzani kutasaidia kuwafikia walengwa vijana au kuongezea kampeni kwa kuweka nyongeza nyingine ya ush-iriki. Kwa mfano, huko Kenya, kampeni ilitengenezwa na Afrika Moja kwa ush-irikiano na Kituo cha Ubora cha IGAD cha Kuzuia na Kupambana na Ufurutu Ada kuhamasisha juu ya vurugu kwenye jamii na kuhamasisha vijana kongelea kuhusu vurugu, kwa kutumia alama ya reli #inaniumiza. Mfano mwingine ni ku-toka Tanzania, ambako shirika la Global Peace Foundation linatumia kampeni za mitandao ya jamii kwenye matukio na miradi yao kama vile kampeni za #Aman-iKwanza au #VijanaNaAmani.*

## SANAA, MUZIKI NA MAIGIZO

*Kuna mifano mingi ya maigizo jumuishi ya jukwaani na sherehe mbalimbali za muzi-ki zinazohamasisha uvumilivu, ujumui-shi, amani, na mbinu za jamii za kuzuia vurugu. Kwa mfano, Umoja wa Anataban wa Sudan Kusini hutumia maigizo ya juk-waani na sanaa kuongea dhidi ya vurugu Sudan Kusini na kuhamasisha jamii kue-lezea "Nimechoka " vurugu (Campeanu, 2017). Huko Burundi, sherehe za muziki wa Pamoja, zinazofanyika kila mwaka kwenye ukanda huu, zinahimiza amani na ushirikiano wa pamoja kwa kupitia muziki wa dini wa Burundi (Pamoja Festival, 2018). Hata hivyo, ifahamike ya kwamba wataalamu katika warsha iliyofanyika mjini Kigali walieleza kuwa sherehe za muziki na maigizo ya jukwaani zimeko-solewa kama ni burudani ya jamii tu na zimeshindwa kuonyesha kama ujumbe wake unaleta matokeo chanya yeyote.*

## MAJUKWAA YA MIJADALA NA TOVUTI

*Wakati majukwaa ya mijadala na tovuti bado sio maarufu sana Afrika mashariki, ku-nauwezekano mkubwa wa kuyatumia hapo baadae kama kiwango cha intaneti kupe-nyeza kitaongezeka kwenye ukanda huu. Hata hivyo, kwenye utafiti wa Tecknohama kwa Afrika Mashariki, ilielezwa kuwa taarifa inayopatikana kwenye tovuti za serikali na mashirika yasio ya kiserikali zimepitwa na wakati au zinaweza kupatikana kupitia njia nyinginezo za mawasiliano (Sika et al., 2015). Kwa mantiki hii, tovuti na majukwaa ya mijadala sio sehemu ya awali ya mawasiliano Afrika Mashariki, na labda yanaweza kutumika kama majukwaa ya ziada. Mfano mmoja wa Afrika Mashariki wa jukwaa la mtandaoni ni www.ivomo.net ambapo vijana huwa na mijadala ya uwazi kuhusu mambo muhimu na malalamiko kwenye jamii yao.*

### UJUMBE, MFUMO WA UJUMBE, NA NAMBA ZA BURE ZA SIMU



*Ujumbe wa simu ni sehemu muhimu ya mawasiliano kwa Afrika Mashariki, hasa hasa kama njia ya kukusanya taarifa juu ya maswala ya utawala na kuhimiza ushiriki wa wananchi (Sika et al., 2015). Uunganishwaji wa simu za mkononi kwa Afrika Mashariki ni 61%, na WhatsApp ndio mfumo maarufu wa kutuma ujumbe unaotumika Afrika Mashariki, ingawa mfumo wa Telegram na Facebook ni maarufu pia (We Are Social and Hootsuite, 2018). Hii inamaanisha ya kuwa picha, ujumbe na sinema ambazo zinaweza kusambazwa kwa kutumia ujumbe au WhatsApp inaweza kuwa sehemu sahihi ya mawasiliano kwa ukanda huu. Pia ifahamike ya kwamba namba za simu za bure ni njia maarufu kuruhusu ushiriki wa umma na mijadala kuhusu jambo au kutoa "namba ya simu ya bure" kwa taarifa zaidi (Sika et al., 2015). Kwa muktadha wa Afrika Mashariki, Kikundi cha habari cha SaSaa, mpango wa chini wa wanahabari unaolenga kutoa simulizi mbadala na chanya nchini Kenya, mara nyingi hutumia mfumo wa ujumbe kama vila WhatsApp kubadilishana maudhui yao kwa aina ya rika kwa rika.*

## 8 TENGENEZA MKAKATI WA USAMBAZAJI

Kifuatacho, simulizi kinzani inahitaji kuhusisha kampeni ili kusaidia kusambaza ujumbe. Baadhi ya mapendekezo ya mikakati ya usambazaji wa ujumbe ni ifuatayo hapa chini:



**Tambua lugha sahihi ya kampeni na hakikisha ujumbe utaakisi lugha ya asili ya sehemu husika.** Ujumbe wa awali ni vyema ukatolewa katika lugha mama ya sehemu husika kwa kadiri iwezekanavyo ila tafsiri itolewe kwa ajili ya jamii pana zaidi.

**Zingatia kampeni za simulizi kinzani zinahusisha ushiriki wa walengwa na mawasiliano pande zote mbili kati ya mjumbe na washiriki** wa kampeni kukiwa na fursa ya mrejesho au fursa ya kujadili au mjadala wa ujumbe unaweza kuwa na tija zaidi kwenye jamii na walengwa tarajiwa.





**Tumia ujumbe mfupi na kina utakaoweza kuwavutia walengwa tarajiwa kama sehemu ya kuanzia.** Endelea na ujumbe mrefu kidogo na toa taarifa za ziada na jukwaa la ushiriki pindi walengwa tarajiwa wanapozidi kuvutiwa.

**Husisha muda wa kampeni na matukio yanayoendelea kwenye jamii kwa wakati huo.**





**Ongeza kampeni za mtandaoni na zile za nje ya mtandao ili kutoa taarifa ya ziada.** Zingatia kutumia alama ya reli kama sehemu kubwa ya kampeni na ihusishe na tovuti sahihi na njia zingine za mitandaoni.

## 9 TATHIMINI NA PEMBUA MATOKEO YA SIMULIZI KINZANI

Kutathimini matokeo ya simulizi kinzani huanzia kwa kuhusisha malengo na madhumuni yaliyowekwa katika hatua ya 4, na kueleza mabadiliko tegemewa ya kampeni. Tathimini nzuri ya matokeo inaweza kuhusisha tathimini endelevu na upembuzi wa kampeni wakati wote wa hatua zilizochagulia kabla ya muda wa kampeni. Kufuatilia, Kutathimini na kupembua kampeni za simulizi kinzani ni muhimu kwa sababu kadhaa zifuatazo:

**KWANINI KUFUATILIA, KUPIMA NA KUTATHIMINI MATOKEO YA SIMULIZI KINZANI**

- ✓ Hakikisha ujumbe unapokelewa na walengwa tarajiwa kwa njia iliyotarajiwa.
- ✓ Hakikisha ujumbe unafikia lengo au madhumuni yanayopelekea matokeo tarajiwa.
- ✓ Hutoa nafasi ya kubadili ujumbe ili kuendana na mazingira.
- ✓ Hutoa taarifa ya namna bora ya kutengeneza ujumbe wa kampeni za baadae.
- ✓ Hutoa mrejesho kwa wafadhili wa mradi kwa ajili ya uwajibikaji.

Hedayah imetengeneza mfumo wa kufuatilia, kupima na kutathimini (KK na K) miradi ya Kuzuia na Kupambana na Ufurutu Ada ambayo pia inaweza kutumika kwenye simulizi kinzani ndani ya Afrika Mashariki (Mattei & Zeiger, 2018). Siyo vyema sana kuuelezea mfumo mzima kwani uko nje ya wigo wa muongozo huu, ila hatua muhimu za kutengeneza mfumo mzuri wa KK na K unaweza kuelezwa kama ifuatavyo hapa chini:




Sehemu zifuatazo hapa chini zitaonyesha baadhi ya mambo muhimu ya hatua hii ya kutengeneza simulizi kinzani kwa undani. Huu usichukuliwe kama mfumo wa kina sana, ila ni muongozo wa namna bora ya kutathimini simulizi kinzani.

### Tambua Viashiria

Ufuatiliaji mzuri, upimaji na tathmini unahusisha kuelezea kipimo cha mabadiliko kwa kupitia viashiria vilivyoelezwa vizuri ambavyo vinaweza kufuatiliwa na kutathiminiwa kwa muda mrefu. Kama ilivyoelezwa kwenye toleo lililopita la Hedayah Namna ya Kuongoza Afrika Mashariki ya Kati na Kaskazini, kuna namna tatu ambazo unaweza kupima simulizi kinzani: ufahamu, ushiriki na matokeo (El Sayed, Faris na Zeiger, 2017; Silverman, et. al, 2016). Baadhi ya mifano ya viashiria vinavyohusishwa na malengo mahususi inaelezwa kwenye kisa mkasa ufuatao.

### Kisa Mkasa Kuhusu Uundwaji wa Kiashiria

Katika nchi X, kuna tatizo la ushawishi wa vijana kati ya umri wa miaka 13-18 kujiunga na kundi la wafurutu ada, kundi G, ambalo huvamia kijiji Y, huiba mazao na rasilimali, na huua raia wasio na hatia kwa kupitia taratibu za kujitoa mhanga. Kundi G lina lengo la kuichukua nchi X na kuweka mfumo wao wa siasa ambapo wateule wa kundi lao watakuwa viongozi, wenye mamlaka kwa muongozo wa imani yao.Kundi G huajiri vijana kwa kuwalazimisha kutenda makosa madogo madogo dhidi ya mama zao, na kuwatisha kuwatangaza kwa watu kama watashindwa kutimiza matakwa ya kundi G. Nchi X pia ina mitandao mingi ya kijamii ambapo Facebook na Twitter zinapatikana kwa urahisi kwa kutumia simujanja. Vipindi vya redio husikilizwa mara nying na nchi X, hasa hasa na wanawake kweny kijiji Y.

**MRADI WA SIMULIZI KINZANI**

Watengeneza simulizi kinzani wanaamua kutengeneza kampeni ya kuhamasisha kuhusu mbinu za ajira za Kundi G katika Kijiji Y kwenye Nchi X miongoni mwa akina mama katika jamii. Hii itafanyika kwa kupitia njia tatu:

1. Majadiliano ya umma kwenye jamii sehemu ambazo mara nyingi wanawake hupatikana kwa wingi.
2. Kampeni za sinema za mitandao ya kijamii zinazotumia alama ya reli #PambanadhidiyaKundiG
3. Matangazo ya umma na majukwaa ya majadiliano kupitia redio za jamii

**LENGO: Kuongeza idadi ya akina mama ambao wanafahamu kuhusu mbinu za ajira za Kundi G.**

### VIASHIRIA VYA UFAHAMU

- Idadi ya watu waliopokea vipeperushi vya matukio ya umma
- Idadi ya "Hisia" kwenye Twitter kutoka kwenye kundi la walengwa tarajiwa
- "Ufuatiliaji" kwenye Facebook
- Idadi iliyotarajiwa ya wasikilizaji wa matangazo ya umma kupitia redio za jamii

### VIASHIRIA VYA USHIRIKI

- Idadi ya "Upendeleo" kwenye sinema zilizowekwa kwenye Facebook
- Kiungo kimebofya mara ngapi, kurudia kutuma ujumbe kwenye twitter, au sinema imesambazwa mara ngapi kwenye Twitter na Facebook
- Idadi ya washiriki wanaohudhuria majadiliano ya umma kwenye jamii
- Idadi ya simu zilizopigwa wakati wa majadiliano kwenye redio

### VIASHIRIA VYA MATOKEO

- Ongezeko la maarifa juu ya mbinu za ajira kwa walengwa tarajiwa (akina mama) kulingana na tathimini ya mrejesho kwenye Twitter
- Ongezeko la maarifa ya mbinu za ajira kwa walengwa tarajiwa (akina mama) kulingana na tathimini ya maoni ya sinema kwenye You Tube au Facebook
- Ongezeko la maarifa ya mbinu za ajira kwa walengwa tarajiwa (akina mama) kulingana na tathimini ya majadiliano kwenye matukio ya umma na kwenye redio

## Ukusanyaji wa Taarifa

Baadhi ya njia sahihi za ukusanyaji wa taarifa za simulizi kinzani kwenye ukanda huu zinajumuisha:

- Mahojiano ya ana kwa ana au majadiliano ya kundi
- Dodoso zinazogawiwa kwa kupitia ujumbe mfupi wa maneno au majukwaa ya mitandao
- Tathimini ya maoni ya maneno muhimu kwenye mitandao au maudhui
- Tathimini ya hisia za maoni ya mitandao au maudhui

## Rasilimali kwa Ajili ya Tathimini

Ni muhimu pia kutathimini rasilimali zilizopo kwa ajili ya ukusanyaji wa taarifa na tathimini. Hii inaweza kujumuisha muda uliopo kwa ajili ya tathimini, fedha, maarifa ya mtathimini na mafunzo ya mazingira husika, njia za ukusanyaji taarifa, na mfumo wa KK naK ; na zana za kiteknolojia za uchambuzi.

# SIMULIZI KINZANI NA MBADALA ZA VISA MKASA KUTOKA AFRIKA



## KISA MKASA #1 : "KIONGOZI WA BAADAE" KIPINDI CHA REDIO | Burundi

Kipindi cha redio cha "Kiongozi wa Baadaye" kinarushwa kwa kupitia kituo cha Redio kijulikanacho kama: Redio COLOMBE, inayohusiana na shirika lijulikanalo kama Centre Jeunes KAMENGE. Ni radio ya kwanza inayoongozwa na vijana nchini Burundi, na inafadhiliwa na UNFPA. Bonyeza hapa kuona.

### 1. SABABU ZA KUSUKUMA NA KUVUTA

**Sababu za Kusukuma:**

- Ukosefu wa elimu
- Ukosefu wa ajira
- Rushwa na fadhila za chama tawala
- Udanganyifu wa kikabila na historia ya migogoro
- Hali ya kukosa usalama
- Kukosa fursa ya sauti mbadala, uchunguzi wa mambo katika jamii, upinzani

**Sababu za Kuvuta:**

-Kisasi kwa kukosa haki
-Kuhitaji mamlaka, heshima
-Hisia ya kuwa sehemu ya kitu fulani
-Ajira na faida za kujiunga na kundi la waasi

**Mitandao ya Kijamii/Wezeshi:**

- "SISI dhidi YAO" simulizi inayotumiwa na wanaopinga serikali

### 2. WALENGWA KUSUDIWA

Walengwa kusudiwa ni wanaume na wanawake wa Bunjumbura na mazingira ya karibu wenye umri kati ya miaka 16-35.

### 3. SIMULIZI INAYOPINGWA

Simulizi ya wafurutu ada inayopingwa ni ile ya kwamba kuna ufinyu wa mifumo na nafasi za ajira pamoja na maamuzi ya maisha, na zaidi ya hapo hakuna suluhisho la matatizo zaidi ya matumizi ya nguvu dhidi ya dola.

### 4. LENGO LA SIMULIZI KINZANI

Kipindi kina malengo mbalimbali:

- Kutoa sauti mbadala ili kubadili mtizamo na tabia kwa kuhamisha mazungumzo kuhusu mambo muhimu kwa vijana. Kipindi kinalenga kutambulisha mawazo mapya na mbinu za kutatua matatizo yanayowakumba vijana. Kwa mfano, kipindi mara nyingi kinazungumzia ujasiriamali na fursa za ajira.
- Vijana wajiamini na kuwa na imani binafsi ya kuweza kubadili na kuendesha maisha yao wenyewe.

### 5. MJUMBE

Kuna wajumbe mbalimbalimuhimu kwa kipindi hiki:

- Vijana waliofanikiwa kimaisha
- Watangazaji vijana kwenye redio (Rika kwa Rika)
- Wataalamu wa masuala ya amani na usalama

Vijana waliofanikiwa kimaisha na watangazaji kwenye vipindi vya redio wanakuwa mfano wa wajumbe wa kuaminika kwa vijana wengine wa Burundi, ambao wanauwezo wa kujadili mada ngumu na kuongelea mambo muhimu kwa kuwa wanakumbwa na changamoto na hali zinazofanana kama vijana pia.

### 6. MANTIKI NA MAUDHUI

Ujumbe wa muhimu ni kwamba kama vijana wanajihisi kuwa na uwezo wa kujitegemea na kujijali wenyewe, watakuwa na uwezo wa kujizuia kutokujiunga na makundi ya vurugu ama kujihusisha na vurugu. Lengo ni kuongeza ufahamu, kujitegemea na maarifa kwa kupitia redio na ushiriki wa mitandao kwa kushirikiana na vijana waliofanikiwa kimaisha nawataalamu.

Baadhi ya mada za majadiliano kwenye kipindi zinajumuisha : haki za binadamu, ajira na shughuli za kuingiza kipato, kuandika Wasifu wa Ujuzi, utatuzi wa migogoro, namna yakuwa salama, namna ya kuzuia ufurutu ada.

### 7. NJIA ZA UWASILISHAJI

Njia kuu ya kuwasilisha ni kupitia kipindi cha redio. Maudhui husambazwa pia kwa kutumia mitandao ya kijamii, majukwaa ya mitandao na tovuti.

### 8. MIKAKATI YA UWASILISHAJI

Watangazaji wa redio wamefundishwa namna bora ya kuendesha mijadala, hata wakati watakapokutana na mada zenye changamoto na mijadala inayoletwa na vijana. Wahamasishaji wamefundishwa kuongoza mazungumzo ili kuonyesha mbadala sahihi wa vurugu au hasira.

Mbinu mbalimbali za usambazaji kwenye majukwaa tofauti zinahakikisha ya kwamba mafunzo muhimu yaliyopatikana kwenye kipindi cha redio yanasaidiwa na muendelezo wa majadiliano na ushirikiano kwenye mitandao ya jamii na majukwaa ya mitandaoni.

### 9. UFUATILIAJI NA TATHIMINI

Vipimo mara nyingi vimejikita kwenye kiwango na kupenya kwa majadiliano:

- Idadi ya watu walioshiriki kwa njia ya simu -Kwenye vipindi vya redio
- Idadi ya watu waliojihusisha kwenye mitandao– Tovuti na mitandao ya jamii.
- Idadi ya vipindi vya redio vilivyorushwa

Vipimo vinahusisha idadi na aina ya shuhuda, kiwango cha majadiliano, sauti na mitizamo iliyohusika, na kiwango cha ushiriki wa watu waliopiga simu kwenye kipindi cha redio.

ANTI-TRIBALISM MOVEMENT

## KISA MKASA #2: JUKWAA LA WAKINAMAMA | Somalia

Mradi huu wa Anti-Tribalism Movement umetengeneza mtandao wa akina mama huko Mogadishu kuzuia ufurutu ada kwa kujenga mahusiano bora na watoto wao. Mradi unahusisha wakina mama waliopoteza watoto wao kwa kupitia Al Shabaab na wanaweza kueleza hadithi yenye nguvu sana kuhusu hatari za ufurutu ada na ugaidi, na mateso wanayopitia ya kupoteza watoto kama mama. Kampeni inahusisha mbinu ya kitabaka kwa kuwalenga wajumbe muhimu kwa kupitia kampeni ya simulizi kinzani ya mama kwa mama na kampeni nyingine ya kuzuia ajira kupitia mama na mtoto. Dhana moja ya muhimu ni kwamba, wanawake hujihisi kuwa na uwezo wa kuongea zaidi dhidi ya Al Shabaab wakati wanawake wengine wenye uzoefu unaofanana na wao wakiwazunguka kwa msaada na ushauri.

### 1. SABABU ZA KUSUKUMA NA KUVUTA

**Sababu za Kusukuma:**

- Ukosefu wa ajira kwa vijana
- Kutengwa kiukoo ikiwamo kisiasa, kiuchumi na kijamii
- Ukosefu wa usalama wa mtu, familia au ukoo
- Mazingira ya msongo wa mawazo, vurugu na uzoefu wa mateso
- Ukosefu wa mifumo ya haki

**Sababu za Kuvuta:**

- Madai ya makundi ya wafurutu ada kuhusu utaifa wa Somalia
- Ulinzi wa Familia/Ukoo
- Fursa za ajira

**Mitandao ya Kijamii/Wezeshi:**

- Kulazimishwa kujiunga

### 2. WALENGWA KUSUDIWA

Walengwa kusudiwa wa mradi ni washawishi wakuu kwenye jamii, ambao ni wakina mama wa vijana walio kwenye hatari Somalia Kusini na Kati. Kundi lapili la walengwa kusudiwa ni wanaume walio kwenye hatari, wenye umiri wa miaka 14-30, ambao ni watoto wa akina mama hao.

### 3. SIMULIZI INAYOPINGWA

Simulizi kinzani ya wafurutu ada inayopingwa ni kwamba familia itapata kipato na ulinzi kutoka kwa Al Shabaab, na Al Shabaab italipiza kisasi au kutoa haki kwa malalamiko, hasa hasa matendo ya vurugu dhidi ya ukoo au familia.

### 4. LENGO LA SIMULIZI KINZANI

Jukwaa hili la kina mama linalenga kuhamasisha wakina mama wa Kisomalia dhidi ya ishara za hatari na kutoa mapendekezo ya namna kina mama wanaweza kuzuia watoto wao wa kiume kujiunga. Baadhi ya malengo madogo madogo yanajumuisha:

- Kuwafundisha wakina mama wengine hatari na matokeo ya watoto wao wa kiume kujiunga na Al Shabaab, hasa hasa matokeo ya kifo cha mtoto wa kiume.
- Kuwafundisha wakina mama kuhusu ishara za mtoto wa kiume anayeweza kujiunga na Al Shabaab
- Kujenga mtandao wa akina mama ambao unaweza kutoamuongozo, msaada na kujali kwa mambo kama haya
- Kuwaandaa wananchi wanaojaliambaowanafahamu kwa kina kuhusu madhara ya Al Shabaab na vurugu.

### 5. MJUMBE

Kwa simulizi kinzani hii, wajumbe wakuu ni wakina mama wa vijana walio katika hatari. Wakina mamahawa wanaaminika na walengwa kusudiwa (vijana wa kiume wa Kisomali) na wanaweza kuwapata na wanaushawishi kwa walengwa kusudiwa.

Ifahamike yakwamba, kuna hatari mbali mbali kwa wajumbe, ambao ni akina mama, ambao wakizungumza, wanageuka kuwa walengwa na kujiweka katika hatari kutoka kwa Al Shabaab. Kwa kuongezea, kuna hatari ya mama mwenyewe kushawishiwa na mawazo ya Al Shabaab na kushindwa kumzuia mtoto wake wa kiume kujiunga nao.

### 6. MANTIKI NA MAUDHUI

Mantiki ya ujumbe mkuu kwa wakina mama wengine ni kwamba, mama ni mshawishimkuu wa maisha ya mtoto wake wa kiume, na anauwezo wa kuingilia kati na kuongea kuzuia mtoto wake wa kiume kujiunga na kundi la magaidi. Mama anaushawishi wa kihisia kwa kuwa anajua namna bora ya kuhusiana na mtoto wake katika njia iliyo bora zaidi.

### 7. NJIA ZA UWASILISHAJI

Njia kuu ya usambazaji wa ujumbe huu ni moja kwa moja kwa kupitia mikutano ya vikundi vya akina mama na ana kwa ana kati ya akina mama na watoto wao wa kiume.

### 8. MIKAKATI YA UWASILISHAJI

Jukwaa la kina mama lina mtandao wa akina mama wengineambapowanaweza kuchangia mawazo na mfumo wa msaada unaweza kutengenezwa na kuwa endelevu. Mazungumzo hufanyika katika lugha ya asili (Kisomali), na mikutano hufanyika mara kwa mara.

### 9. UFUATILIAJI NA TATHIMINI

Shughuli hii ilifuatiliwa au kutathiminiwa kwa kupitia viashiria vifuatavyo kulingana na utafiti wa kabla na baada:

- Wakina mama wanauelewa zaidi kuhusu ishara za ajira au kushawishiwa
- Wakina mama wanauelewa zaidi kuhusu fursa mbadala za kiuchumi kwa watoto wao wa kiume.

Majukwaa yalipimwa pia kulingana na ukuwaji wa mtandao na ubora wa huduma walizotoa:

- Majukwaa ya kina mama yanakuwa kwa ukubwa (walau akina mama 500 wamefikiwa moja kwa moja kwa kupitia huduma hii baada ya miaka miwili na kwa sasa kuna mtando imara unaoendelea wa akina mama 40-50).
- Majukwaa yanaendelea na mikutano ya juma kwenye sehemu tatu kuu za Mogadishu zenye mitandao mikubwa kwenye jiji.
- Kuna baadhi ya mifano iliyofanikiwa ya kuzuia vijana kujiunga na Al Shabaab ambao walishawishiwa moja kwa moja



## KISA MKASA #3: MPANGO WA KUZUIA USHAWISHI NA UFURUTU ADA UNAOPELEKEA KWENYE UGAIDI (PRELT) | Somalia

Mradi huu umeandaliwa na Kituo cha Kimataifa cha Cairo cha Kutatua Migogoro, Kulinda na Kujenga Amani (CC-CPA) kama sehemu ya jitihada za kudhoofisha simulizi za wafurutu ada juu ya dini nchini Somalia. Mradi kama huu unafanyika pia kwenyemazingira ya Nigeria.

### 1. SABABU ZA KUSUKUMA NA KUVUTA

Sababu za Kusukuma:

- Muendelezo wa vurugu na migogoro nchini Somalia
- Ukosefu wa maarifa ya dini
- Ukosefu wa ajira
- Ujinga

Sababu za Kuvuta:

- Ahadi za uongo (Zawadi baada ya kifo, Utambulisho wa Kundi, Kuwaokoa Waislamu wa Ummah nk.)
- Kuokoka kutoka kwenye jamii/serikali isiyotenda haki na wala rushwa.

Mitandao ya Kijamii/Wezeshi:

- Mvuto wa simulizi za wafurutu na haiba ya viongozi wa kifurutu.

### 2. WALENGWA KUSUDIWA

Walengwa kusudiwa niwashawishi wakuu kwenye jamii, ambao ni wanawake, vijana na viongozi wa mila.

### 3. SIMULIZI INAYOPINGWA

Simulizi kinzani hii inapinga simulizi kubwa tatu za wafurutu ada (Al Shabaab):

- Tafsiri potofu ya Jihad
- Tafsiri isiyo sahihi ya dhana zingine za Kiislamu (Takfir, Hakimiya, Jahiliyya)
- Kutokuelewa vizuri kuhusu maisha ya Mtume na wafuasi wengine

### 4. LENGO LA SIMULIZI KINZANI

Jukwaa hili la kina mama linalenga kuhamasisha wakina mama wa Kisomalia dhidi ya ishara za hatari na kutoa mapendekezo ya namna kina mama wanaweza kuzuia watoto wao wa kiume kujiunga. Baadhi ya malengo madogo madogo yanajumuisha:

- Kutathimini mazingira ya asili na njia za watu binafsi zinazopelekea kushawishiwa,
- Kutambua majaribio ya kushawishiwa,
- Kutambua mambo yanayohusiana na simulizi za wakaidina wafurutu, na
- Kupata nyenzo sahihina ujuzi wa kutengeneza na kufikisha simulizi mbadala–kwa kutumia mafundisho ya wastani ya Kiislamu–ili jamii iweze kuchangia kuzuia ufurutu na ushawishi.

### 5. MJUMBE

Mjumbe mkuu (mkufunzi) ni utafiti na kituo cha mafunzo (CCCPA) chenye mamlaka ya kidini na mahusiano na Al Azhar.

Washawishi wakuu waliofundishwa kwenye mradi huu hatimaye wamekuwa wajumbe. Hapa wanajamii wanaaminika kwa sababu :

- Wanaelewa ugumu wa mazingira na njia sahihi za kutoa simulizi kinzani.
- Wanaaminika.
- Wanaweza kushawishi makundi yao na kusambaza ujumbe mbadala.

### 6. MANTIKI NA MAUDHUI

Maudhui ya mafunzo yanawapatika washiriki:

- Nyenzo za kuchunguza na kuelewa mazingira ya mgogoro, kuonyesha namna na kwanini ushawishihutokea na kutambua hatua ya utatuzi kwa washiriki.
- Uelewa wa Sheria ya Uislamu (Sharia), na kuelewa dhana kadhaa za Uislamu hususani Jihad, Takfir, Hakimiyya na Jahiliyia.
- Kuelewa namna simulizi na jumbe za kigaidi zinavyotengenezwa, ikujumuisha namna wanavyotengeneza mgogoro na jinsi wanavyohusisha dini ndani yake, kwa kupitia "tathimini ya maudhui" ya nyenzo za propaganda (sinema, machapisho na hotuba) za mashirika ya kigaidi.
- Nyenzo za kutengeneza ujumbe wao pekee mbadala, chanya na unaojumuisha amani na uvumilivu ambao umejikita kwenye uelewa wa jumla wa tamaduni za Uislamu, zilizojengeka kwenye tafsiri sahihi na za wastani za Sharia za Uislamu.
- Mfumo wa ujuzi wa kuweza kuwasilisha ujumbe huu jumuishi. Hii inajumuisha kusikiliza kwa makini, mawasiliano na ujuzi wa uongozi, kujadiliana na uwezo wa kutengeneza hoja za ushawishi na thabiti.

### 7. NJIA ZA UWASILISHAJI

Mafunzo haya hufanyika katika mazingira ya ana kwa ana. Maudhui ya mafunzo yanaweza kutumiwa na washiriki kwenye shule, mikutano ya hadhara na majukwaa mengine ya mitandaonina nje ya mitandao.

### 8. MIKAKATI YA UWASILISHAJI

Baadhi ya mikakati ya uwasilishaji zinajumuisha:

- Ujumbe mbadala na juimuishi unatengenezwa wakati wa mafunzo na baada
- Unasambazwa kupitia lugha ya asili ya washiriki na kulingana na mazingira yao.
- Zinasambazwa kwenye makundi ya ushawishi ya washiriki katika sehemu zao za kazi, majumbani na mazingira ya jamii.

### 9. UFUATILIAJI NA TATHIMINI

- Tathimini ya kabla na baada inafanyika wakati wa mafunzo kupima uelewa kabla na baada ya mafunzo.
- Majadiliano ya makundi hufanyika mara baada ya mafunzo ili kupata mrejesho kutoka kwa washiriki.
- Kufuatilia maendeleoyao na matokeo baada ya miezi 3, 6 na mwaka.




## KISA MKASA #4 : VIONGOZI VIJANA WA IMANI | Uganda

Mradi huu wa Allied Muslim Youth Uganda (AMYU) unatoa maarifa na ujuzi kwa viongozivijana wa imani kuzuia vurugu na kukuza uaminifu na kujenga mahusianokwa kuhimiza mjadala baina ya vijana wa imani tofauti nchini Uganda.

Ni sehemu kubwa ya miradi ya (AMYU) ya Kupambana na Ufurutu Ada inayolenga wanafunzi na wahubiri vijana ambao wanaweza kuwashawishi kujenga muungano wa madhehebu mbalimbali kwenye vyuo vya dini na visivyo vya dini na pia kutengeneza kampeni za mitandao ya kijamii au matukio ya kijamii yanayokuza uvumilivu na mijadala yamadhe-hebu.

### 1. SABABU ZA KUSUKUMA NA KUVUTA

**Sababu za Kusukuma:**

- Kukosa uzoefu wa madhehebu mbalimbali
- Kubaguliwa
- Kukosa maarifa ya dini
- Kukosa watu wa kuigwa au watu chanya

**Sababu za Kuvuta:**

- Hali ya uwepo
- Hali ya utambulisho na kujitathimini

**Mitandao ya Kijamii/Wezeshi:**

- Haiba ya viongozi wa Kifurutu na mvuto wa simulizi za mitandaoni

### 2. WALENGWA KUSUDIWA

Walengwa waliokusudiwa kwenyemradi huu ni washawishi wakubwa kwenye jamii kwa kupitia wahuburi vijana kutoka kwenye imani tofauti. Walengwa kusudiwa wa ujumbe ni kundi la vijana kwa ujumla kutoka Uganda (16-35)

### 3. SIMULIZI INAYOPINGWA

Simulizi kinzani hii inalenga maneno yasiyo na tija ya utengano ya "SISI " dhidi "YAO" kati ya Wakristu na Wais-lamu. Pia unalenga kudhoofisha ujumbe wa chuki au ku-tokuvumilia dhidi ya imani tofauti.

### 4. LENGO LA SIMULIZI KINZANI

Lengo ni kuwapatia nyenzo wahubiri vijana kukuza mijadala ya madhehebu mbalimbali, uvumi-luvu na ushirikiano baina yao na kutengeneza ustahimilivudhidi ya simulizi za wafurutu ada.

### 5. MJUMBE

Mjumbe wa mradi huu ni wafanyakazi wa AMYU na baadhi ya wahuburi vijana waliofundishwa na wanaoaminika kutoka dini tofauti tofauti. Mwanzilishi, Nuwagaba Muhsin Kaduyu, anaaminika sana baina ya vijana wa Kiislamu wa Uganda akiwa kama mmoja wa wahubiri vijana. Mara baada ya wahubiri vijana kufundishwa na kushauriwa kwenye vipengele muhimu vya majadiliano ya madhehebu na ushirikiano, mujumbe ni mhubiri kijana mwenye ujuzi wa kushawishi washiriki wengine wa imani yake kuwa na uvumilivu dhidi ya wengine, na kuwa watu wa kuigwa.

### 6. MANTIKI NA MAUDHUI

Ujumbe muhimu ni kwamba Waislamu na Wakristu wanaweza kuishi kwa pamoja, kushirikiana na kusaidiana kwenye jamii.

### 7. NJIA ZA UWASILISHAJI

Ujumbe unawasilishwa kwa kupitia njia kuu zifuatazo:

- Mitandao ya kijamii (Facebook na Twitter)
- Redio (vipindi vya majadilianovikifanywana wahubiri vijana)
- Runinga aumatangazo ya umma yakifanywa na wahubiri vijana
- Matukio au ushiriki wa ana kwa ana (Mf. Matembezi ya madhehebu)
  Sehemu ya mikutano

### 8. MIKAKATI YA UWASILISHAJI

Kampeni hii inawasilishwa kwa kupitia lugha za asili pamoja na Kiingereza. Ujumbe mbali mbali unasindikizwa na kujengewa uwezo na kushauriwa na AMYU mara kwa mara. Mtandao wa AMYU unatumia miradi mipya na iliyopo ya uhamasishaji kwenye jamii, na pia huwahimiza wahubiri vijana kusambaza ujumbe kwenye majukwaayao, kama vile nahubiri ya Ijumaa au Jumapili.

### 9. UFUATILIAJI NA TATHIMINI

Mradi huu umepimwa kwa kuangalia:

- Idadi ya shughuli zilizohusisha madhehebu mbalimbali zilizofanywa na washiriki
- Idadi ya simulizi zilizotengenezwa kwenye mitandao na nje ya mitandao na wahubiri kwa kutumia mitandao ya kijamii na majukwaa mengine.

## KISA MKASA #5: JITIHADA ZA MAENDELEO YA JAMII | Kenya

Mradi huu unaoendeshwa na Jitihada za Maendeleo ya Jamii huko Eastleigh, Kenya, unatizama namna sekta ya uchumi binafsi inaweza kuchangia kupambana na malalamiko yanayopatikana kwenye mchakato wa ushawishi.

### 1. SABABU ZA KUSUKUMA NA KUVUTA

Sababu za Kusukuma:

- Umasikini
- Ukosefu wa Ajira
- Mgawanyo wa rasilimali usio wa haki (kati ya jamii) na kukosa fursa za ajira

Sababu za Kuvuta:

- Hali ya utambulisho
- Uwezeshaji kiuchumi

### 2. WALENGWA KUSUDIWA

Walengwa waliokusudiwa kwenye mradi huu ilikuwa ni kwa faida ya vijana wa Eastleigh, Kenya waliokata tamaa miaka 14 – 25, wakike na wanaume.

### 3. SIMULIZI INAYOPINGWA

Simulizi kinzani za kifurutu zinazopingwa ziko pande mbili:

- Ubaguzi wa kikabila na chuki dhidi ya wageni– kitu ambacho kingeweza kutumiwa na Mashirika ya Wafurutu Ada au jamii zilizohatarini kwa kutengwa kutoka na shambulio la Westgate
- Ukosefu wa fursa za uchumi na ugawaji wa ajira usio na haki kwenye jamii ya Eastleigh

### 4. LENGO LA SIMULIZI KINZANI

Malengo ya simulizi kinzani ni:

- Kuzuia ubaguzi kati yamakundi ya makabila
- Kuzuia mgawanyo kati ya biashara na vijana walioshawishiwa (Ushirikiano wa jamii)
- Kutoa hatua mbadala kwa kuwashirikisha vijana kwenye majadiliano ya kitaifa
- Kutoa hatua mbadala kwa kuruhusu fursa za kiuchumi na ushirikiano kukua

### 5. MJUMBE

Mjumbe mkuu ni Eastleigh Business Community Assocation (EBCA) inayojihusisha na makundi ya vijana. Ni shirika linaloheshimika na kuaminika kwenyejamii, na wanauaminifu kwenye soko la ajira huko Eastleigh.

### 6. MANTIKI NA MAUDHUI

Ujumbe unasisitiza ya kuwa jamii ya wafanyabiashara Eastleigh inajali kuhusu hali ya baadaye ya vijana wao kwa kutoa fursa za ajira na kuwaunganisha kwenye kazi mpya. Ujumbe mwingine ni kwamba, vijana wanastahili kusikilizwa na jamii nzima, ikijumuisha sekta binafsi na viongozi wa serikali.

### 7. NJIA ZA UWASILISHAJI

Mradi huu unatekelezwa kwa Jitihada za Maendeleo ya Jamii kupitia:

- Mwingiliano wa ana kwa ana baina ya vijana na EBCA
- Runinga, redio na kampeniza mitandao ya kijamii kwenye maeneo yaliyojikita kwenye mpango kazi wa EBCA na mipango ya mapema.

## 8. MIKAKATI YA UWASILISHAJI

Mradi unahitaji ushirikiano mzuri kati ya jamii na sekta binafsi, inayoongozwa na EBCA. Ujumbe unawasilishwa kwa Kiingereza na Kiswahili kwa kupitia njia mbalimbali za uwasilishaji, ila zaidi hufanyika kwenye mazungumzo nje ya mtandao na maonyesho ya ajira.

## 9. UFUATILIAJI NA TATHIMINI

Mradi huu unapimwa kupitia viashiria vifuatavyo:

- Ushiriki wa vijana kwenye shughuli zilizopangwa.
- Ushiriki wa mitandao kukiwa na ujumbe kila kinachofanywa na EBCA.
- Vijana walikuwa wakitoa taarifa kwe viongozi wa ngazi ya chini juu ya kiwango ambacho vurugu ingeweza kutokea.
- Kiwango cha ushiriki cha jamii ya wafanyabiashara kwenyemikutano mingine.

Ifahamike hapa yakwamba, moja ya makundi ya asili 'yenye nguvu kubwa' lilishiriki kwenye shughuli hii kwa kuwa walivutiwa na kilichokuwa kinaendelea. Hii ilionekana kama mafanikio kwakuwa ujumbe uliwafikia walengwa kusudiwa ambao ni vijana wenye udhaifu wa kuonyesha tabia za vurugu.

## KISA MKASA #6 : KITUO CHA HABARI SASAA | Kenya

Kituo cha habari cha SaSaa ni mradi unaowasaidia vijana nchini Kenya kujihusisha na shughuli mbalimbali zaubunifu. Ni mradi unaoendeshwa na vijana wanahabari kutoka ngazi ya chini, na unasimamiwa na YADEN Afrika Mashariki. Mradi unahusisha warsha za mafunzo za kutengeneza maudhui pamoja na majukwaa ambayo watasambaza maudhui baada ya kutengenezwa.

### 1. SABABU ZA KUSUKUMA NA KUVUTA

Sababu za Kusukuma:

- Matarajio yasiyofikiwa
- Mamlaka kutokusikiliza vijana / Ukosefu wa 'nguvu ya kujieleza'

Sababu za Kuvuta:

- Matarajio yasiyofikiwa
- Mamlaka kutokusikiliza vijana / Ukosefu wa 'nguvu ya kujieleza'

### 2. WALENGWA KUSUDIWA

Walengwa kusudiwa wakuu kwenye kampeni hii ni vijana wa Kenya ambao wako kwenye umri wa njia panda kati ya 14-27, ikijumuisha wanawake na wanaume. Ila, sehemu kubwa ya mawasiliano ya mradi umefanya kazi pia na washawishi wakuu kwenye mitaa kwa mantiki ya viongozi vijana mbalimbali.

### 3. SIMULIZI INAYOPINGWA

Simulizi kinzani kubwa ya wafurutu ada inayopingwa ni swala la sauti ya vijana kutokusikilizwa na kwamba vijana 'hawana thamani' ("kuwaamini, na kufanya kila kijana kuwa mwenye thamani.") Mashirika ya wafurutu ada kama Al Shabaab yanatoa hali ya uwepo, maana na thamani kwa vijana wa Kenya, hivyo ujumbe huu unalenga kupinga hoja hiyo na kuonyesha mbadala.

### 4. LENGO LA SIMULIZI KINZANI

Lengo la kampeni hii ni kuwapatia walengwa kusudiwa maana, madhumuni na uwepo. Hii inajumuisha kutoa mambo mbadala kwa kupitia shughuli chanya na kukuza mahusiano kati ya vijana na viongozi wa serikali kuendeleza mabadiliko yenye tija.

### 5. MJUMBE

Mjumbe mkuu ni watu mashuhuri wa mitaa (vi-ongozi) kutoa simulizi kinzani. Wajumbe wana-aminika, wanahisia na wanamuunganiko wa moja kwa moja na jamii.

### 6. MANTIKI NA MAUDHUI

Kuna vipengele vingi kwenye mradi huu na kila kipengele kina ujumbe wake mkuu. Vipengele hivi vimeelezwa kwa kifupi hapa chini:

- Mchakato wa Ubunifu: shughuli za uandishi habari– zinaboresha kufikiri kwa kina baina ya viongozi vijana
- Mchakato wa Ubunifu: kutengeneza sinema– wanavifaa vya kuaminika
- Mchakato wa Ubunifu: utungaji wa muziki– njia za kibunifu kuelezea malalamiko
- Mchakato wa Ubunifu: malengo makuu ya kutoa maoni kwawahusika
- Sehemu zamakutano: zinakuza mwingiliano chanya kati ya vijana na mienendo ya makundi

https://bit.ly/2JcUr0t
https://bit.ly/2JcNPPK

### 7. NJIA ZA UWASILISHAJI

Kuna utaratibumbalimbaliwa kufikisha ujumbe:

- Nje ya mtando (sehemu za makutano, warsha za kutengeneza kinachohitajika)
- Kwenye mtandao, kupitia njia za mitandao (Face-book, You Tube)
- Uwasilishaji wa Rika kwa Rika (WhatsApp – inaji-penyeza kwenye mitandao iliyofungwa)

### 8. MIKAKATI YA UWASILISHAJI

Mradi unahusisha timu ya watengenezaji na watekelezaji waliosaidia kutengeneza maudhui pamoja na mahusiano ya majirani ambao ni muhimu kuhusisha maudhui na mazingira. Maudhui yanasambazwa kwa kutumia njia mbalimbali zinzaofaa (kwa mfano, CD kwa muziki uliotengenezwa). Lugha iliyotumika ni Kiswahili ambayo ni lugha ya asili.

### 9. UFUATILIAJI NA TATHIMINI

Ujumbe ulifuatiliwa kwa njia zifuatazo:

- Mara ngapi nyimbo na sinema zilisambazwa kwenye mitandao binafsi
- Ni watu wangapi walivutiwa na kutengeneza sinema zao na muziki bila kujihusisha moja kwa moja kwa kituo cha habari cha SaSaa
- Mahudhurio kwenye sehemu za makutano, na idadi ya sehemu za makutano zilizofanyika

## MAREJEO

Ababa, A. (2017, March 20-24). State of Africa's Population 2017. *African Union*. Retrieved from https://au.int/sites/default/files/newsevents/workingdocuments/32187-wd-state_of_africas_population_-_sa19093_-e.pdf.

Abdi, R. (2015, September 20). East Africa's Sufi Path to Countering Violent Extremism. *Strategic Thinking on East Africa*. Retrieved from http://www.strathink.net/ethiopia/east-africas-sufi-path-to-countering-violent-extremism/.

Africa Center for Strategic Studies. (2012, January 22-27). *Preventing Youth Radicalization in East Africa*. Retrieved from http://africacenter.org/wp-content/uploads/2016/01/Preventing-Youth-Radicalization-in-East-Africa-Program-Summary-ACSS.pdf.

Al Jazeera News Agencies (2017, August 18). Three killed in Burundi grenade attacks at bars. *Al Jazeera*. Retrieved from http://www.aljazeera.com/news/2017/08/killed-burundi-grenade-attacks-bars-170818140040303.html.

Allied Muslim Youth Uganda. (2017). *Interfaith Inter-Generational Retreats with Religious Leaders and Young Adults*. Retrieved from http://www.amyug.org/courses/interfaith-inter-generational-retreats/.

[Anti-Tribalism Movement (ATM)]. (2015, May 3). *Anti-Tribalism Movement - Preaching In Practice - Abdi Shire*. [Video File]. Retrieved from https://www.youtube.com/watch?v=zBtkunUuRrc.

Anzalone, C. (2016a). Continuity and Change, The Evolution and Resilience of Al-Shabaab's Media Insurgency, 2006-2016. *Hate Speech International*. Retrieved from https://www.hate-speech.org/wp-content/uploads/2016/11/shababreport.pdf.

Anzalone, C. (2016b). The Resilience of al-Shabaab. *CTC Sentinel*, *9*(4), 13-20. https://ctc.usma.edu/the-resilience-of-al-shabaab/.

Ashour, O. (2010). Online de-radicalisation? Countering violent extremist narratives: Message, messenger and media strategy. *Perspectives on Terrorism* *4*(6): 15-19. http://terrorismanalysts.com/pt/index.php/pot/article/view/128/html.

Avis, W. R. (2016). The role of online/social media in countering violent extremism in East Africa. GSDRC Helpdesk Research Report. http://www.gsdrc.org/wp-content/uploads/2016/06/HDQ1380.pdf.

Bakari, M. (2001). *The Democratisation Process in Zanzibar: A Retarded Transition*. Hamburg: Institute for African Affairs.

BBC News. (2007, January 11). Mengistu is handed life sentence. *BBC News*. Retrieved from http://news.bbc.co.uk/2/hi/africa/6251095.stm.

Beevor, E. (2017). Coercive Radicalization: Charismatic Authority and the Internal Strategies of ISIS and the Lord's Resistance Army, Studies in Conflict & Terrorism. *Studies in Conflict & Terrorism*, *40*(6), 496-521.

Botha, A. (2015). "Radicalisation to Terrorism in Kenya and Uganda: a Political Socialisation Perspective," *Perspectives on Terrorism*, *9*(5). http://www.terrorismanalysts.com/pt/index.php/pot/article/view/457/html.

Botha, A. (2016). Factors Facilitating Radicalization in Kenya and Somalia. In Zeiger, S. (Eds.). *Expanding Research on Countering Violent Extremism*. Retrieved from http://www.hedayahcenter.org/Admin/Content/File-410201685227.pdf.

Briggs, R. & Feve, S. (2013). Countering the Appeal of Extremism Online. Policy Brief. Institute for Strategic Dialogue. Retrieved from https://www.dhs.gov/sites/default/files/publications/Countering%20the%20Appeal%20of%20Extremism%20Online-ISD%20Report.pdf.

[Breakthrough]. (2016, August 22). *Mayor of Mogadishu*. [Video File]. Retrieved from https://www.youtube.com/watch?v=IPA9Pbxjqtc&feature=youtu.be.

Campeanu, A. (2017, July 12). Tired of war, South Sudanese youth turn to art to push for peace. Reuters. Retrieved from https://www.reuters.com/article/us-southsudan-art/tired-of-war-south-sudanese-youth-turn-to-art-to-push-for-peace-idUSKBN19X16Q.

Chinese investment in Africa: Beijing's testing ground. Financial Times. Retrieved from https://www.ft.com/content/0f534aa4-4549-11e7-8519-9f94ee97d996.

City University of Mogadishu. (2018). *The Center for Conflict, Governance & Peacebuilding.* Retrieved from http://www.cu.edu.so/center-for-conflict-governance--peacebuilding.html.

"Democratic Front for the Liberation of Rwanda (FDLR)." (May 2015). Washington D.C.: University of Maryland, START. Retrieved from http://www.start.umd.edu/baad/narratives/democratic-front-liberation-rwanda-fdlr.

Dualeh, R. (2015, October 19). Countering Violent Extremism in the Horn of Africa. *Georgetown Journal of International Affairs.* Retrieved from https://www.georgetownjournalofinternationalaffairs.org/online-edition/countering-violent-extremism-in-the-horn-of-africa.

Elsayed, L., Faris, T., & Zeiger, S. (2017, December). *Undermining Violent Extremist Narratives in the Middle East and North Africa A How-To Guide.* Retrieved from http://www.hedayahcenter.org/Admin/Content/File-10122017161331.pdf.

Fornace, K. (2009, April). The Rwandan Genocide. *Beyond Intractability.* Retrieved from https://www.beyondintractability.org/casestudy/fornace-rwandan.

The Global Peace Foundation. (2015). *Amani Kwanza Campaign.* Retrieved from http://www.globalpeace.org/project/amani-kwanza-campaign.

The Guardian. (2017, October 23). This was not 'just another bomb in Mogadishu'. It will destroy al-Shabaab Abdirahman Omar Osman 'Engineer Yarisow'. *The Guardian.* Retrieved from https://amp.theguardian.com/global-development/2017/oct/23/this-was-not-just-another-bomb-in-mogadishu-it-will-destroy-al-shabaab-somalia.

Guha, S. (2017). Violent Extremism in Kenya: Risk and resilience. *The Rift Valley Institute.* Retrieved from http://riftvalley.net/publication/violent-extremism-kenya#.WsTK75Nub-b.

Ikelegbe, A. & Okumu, W. (2010). Introduction: Towards conceptualization and understanding of the threats of armed non-state groups to human security and the state in Africa." In Militias, Rebels and Islamist Militants: Human Insecurity and State Crises in Africa." Edited by Okumu, W., and Ikelegbe, A. Retrieved from https://issafrica.org/research/books-and-other-publications/militias-rebels-and-islamist-militants-human-insecurity-and-state-crises-in-africa.

Jackson, P. (2002). The March of the Lord's Resistance Army: Greed or Grievance in Northern Uganda? *Small Wars & Insurgencies, 13*(3), 29-52. https://doi.org/10.1080/09592310208559196.

Kaduyu, N. M. [muhsin kaduyu]. (10 June 2016). Islam and Positive Youth Development. [Video File]. Retrieved from https://www.youtube.com/watch?v=xd08oK21Gek.

Kemp, S. (2018, January 30). Digital in 2018: World's Internet Users Pass the 4 Billion Mark. *We Are Social.* Retrieved from https://wearesocial.com/blog/2018/01/global-digital-report-2018.

Kezio-Musoke, D. (2017, March 25). "Spaces for Peace." Never Again Rwanda. Retrieved from http://neveragainrwanda.org/featured/spaces-peace.

Khalil, J, & Zeuthen, M. (2014). A Case Study of Counter Violent Extremism (CVE) Programming: Lessons from OTI's Kenya Transition Initiative. *Stability: International Journal of Security & Development, 3*(1), 1-12. http://dx.doi.org/10.5334/sta.ee.

Khalil, J., & Zeuthen, M. (2016, June 2-16). Countering Violent Extremism and Risk Reduction A Guide to Programme Design and Evaluation. Retrieved from https://rusi.org/sites/default/files/20160608_cve_and_rr.combined.online4.pdf.

Kiprop, V. (Retrieved from 2017, July 4). China most important African trade partner. *The East African.* Retrieved from http://www.theeastafrican.co.ke/business/China-most-important-African-trade-partner--/2560-3998956-a07dq1z/index.html.

Kwibuka, E. (2014, February 20). TI boss speaks about Rwanda's fight against corruption. *The New Times*. Retrieved from http://www.newtimes.co.rw/section/read/73263/.

Le Sage, A. (2014, September). The Rising Terrorist Threat in Tanzania: Domestic Islamist Militancy and Regional Threats. *Strategic Forum National Defense University*. Retrieved from http://ndupress.ndu.edu/Portals/68/Documents/stratforum/SF-288.pdf.

Mattei, C. & Zeiger, S. (2018). Evaluate Your CVE Results: Projecting Your Impact. Hedayah. Retrieved from http://www.hedayahcenter.org/Admin/Content/File-16720189339.pdf.

Maruf, H. (2017, September 27). Somali Teenagers Flee Al-Shabaab Recruitment Campaign. *VOA*. Retrieved from https://www.voanews.com/a/somali-teenagers-flee-al-shabab-recruitment-campaign/4046459.html.

Meleagrou-Hitchens, A. (2012, November 19). ICSR Insight – Al-Shabaab: Recruitment and Radicalisation in Kenya. *ICSR*. Retrieved from http://icsr.info/2012/11/icsr-insight-al-shabaab-recruitment-and-radicalisation-in-kenya/.

MEMRI. (2017, July 7). *Jihad and Terrorism Threat Monitor (JTTM) Weekend Summary*. Retrieved from https://www.memri.org/reports/jihad-and-terrorism-threat-monitor-jttm-weekend-summary-257.

MONUSCO. (2018, February 13). RDC: mandats d'arrêt contre 26 responsables présumés des ADF. *Radio Okapi*. Retrieved from https://www.radiookapi.net/2018/02/13/actualite/justice/rdc-mandats-darret-contre-26-responsables-presumes-des-adf.

Mugabi, I. (2017, June 16). "Rwanda: Fresh start for former FDLR fighters?" DW.com. Retrieved from http://www.dw.com/en/rwanda-fresh-start-for-former-fdlr-fighters/a-39147954.

Mugisha, L. (2015, September 19). Geoffrey Baluku: « utilisez ce que vous avez maintenant ». Akeza.net. Retrieved from http://akeza.net/geoffrey-baluku-utilisez-ce-que-vous-avez-maintenant/.

Neumann, P. (2015, September). Victims, Perpetrators, Assets: The Narratives of Islamic State Defectors. *ICSR*. Retrieved from http://icsr.info/wp-content/uploads/2015/09/ICSR-Report-Victims-Perpertrators-Assets-The-Narratives-of-Islamic-State-Defectors.pdf.

Odhiambo, E., Onkware, K., & Leshan, M. (2015, May-June). Domestic Radicalisation in Kenya. *Global Journal of Interdisciplinary Social Sciences, 4*(3), 48-56. http://gifre.org/library/upload/volume/48-56-Domestic-vol-4-3-15-gjiss.pdf.

Orlale, R. (2015, May 21). In rural Kenya, access to information is power. *Ford Foundation*. Retrieved from https://www.fordfoundation.org/ideas/equals-change-blog/posts/in-rural-kenya-access-to-information-is-power/.

Pamoja Festival [Facebook]. (2018). Pamoja Festiva [Facebook Page]. Retrieved from https://www.facebook.com/PamojaFest/.

PBS (Producer). (2016, April 22). Propaganda is effective weapon as Al-Shabaab makes resurgence. *PBS News Hours*. Podcast retrieved from https://www.pbs.org/newshour/show/propaganda-is-effective-weapon-as-al-shabab-makes-resurgence.

Peel, K. (2015). *Abduction, Rebellion and Reprieve: The Narratives of Former Members of the Lord's Resistance Army*. Retrieved from Simon Fraser University Doctoral Thesis.

Rinehart, J. (2006). *Apocalyptic Faith and Political Violence: Prophets of Terror*. New York: Palgrave Macmillan.

Ruby, M., & Taylor, R. (2014, April 6). Portraits of Reconciliation. *The New York Times*. Retrieved from https://www.nytimes.com/interactive/2014/04/06/magazine/06-pieter-hugo-rwanda-portraits.html?_r=0.

Russell, O. (June 2017). Meet Me at the Maskani: A Mapping of Influencers, Networks and Communication Channels in Kenya and Tanzania. Search for Common Ground. Retrieved from https://www.sfcg.org/wp-content/uploads/2017/07/SFCG-Meet-Me-at-the-Maskani-Final.pdf.

[Sasaa Media]. (2017, Oct 18). *Just A Minute Kwale Edition.* [Video File]. Retrieved from https://www.youtube.com/watch?time_continue=32&v=FoNEaFEf-h8.

Scofield's Associates. (2017, March 31). *Baseline Evaluation for Inuka Project.* Retrieved from https://www.sfcg.org/wp-content/uploads/2017/07/SFCG-BASELINE-EVALUATION-REPORT-FOR-INUKA-PROJECT-Final.pdf.

[Search for Common Ground]. (2016, July 21). *South Sudan: two tribes rebuild what violence demolished.* [Video File]. Retrieved from https://www.youtube.com/watch?time_continue=32&v=-FoNEaFEf-h8.

Shabaab men turn Kenyan schoolgirls into sex slaves. (2017, June 10). *Caasimada.net.* Retrieved from https://www.caasimada.net/shabaab-men-turn-kenyan-schoolgirls-into-sex-slaves/.

Sika, V. et al. (2014). ICT and Governance in East Africa: A Landscape Analysis in Kenya, Uganda and Tanzania 2014. **iHub_Research.* Retrieved from https://files.ihub.co.ke/downloads/ict_4_gov_report.pdf.

Sikorski, T. (2014). *Airwaves and microblogs: a statistical analysis of al-Shabaab's propaganda effectiveness.* Retrieved from Calhoun: The NPS Institutional Archive. Retrieved from http://hdl.handle.net/10945/44667

Silverman, T., Stewart, C., Amanullah, Z., & Birdwell, J. (2017). The Impact of Counter-Narratives. Institute for Strategic Dialogue. Retrieved from https://www.jugendundmedien.ch/fileadmin/user_upload/3_Medienkompetenz/Gegennarrative/Impact-of-Counter-Narratives_ONLINE_1.pdf

Small Arms Survey. (2017). National Small Arms Assessment in South Sudan. *UNDP.* Retrieved from http://www.ss.undp.org/content/dam/southsudan/library/Reports/South%20Sudan%20National%20Small%20Arms%20Assessment%20-%20Web%20Version.pdf?download.

Somalia Stability Fund. (2016, March). *Support to Higher Education in Conflict Resolution and Peacebuilding.* Retrieved from http://stabilityfund.so/support-to-higher-education-in-conflict-resolution-and-peacebuilding.

Spillius, A. (2012, February, 21). Al-Shabaab militia abducting teenage girls to marry fighters. *The Telegraph.* Retrieved from https://www.telegraph.co.uk/news/worldnews/africaandindianocean/somalia/9096315/Al-Shabaab-militia-abducting-teenage-girls-to-marry-fighters.html.

Strasser, F. (2016, December 15). South Sudan: Looming Genocide, Plans for Prevention Experts on World's Newest Country Lay Out Potential Strategies. *United States Institute of Peace.* Retrieved from https://www.usip.org/publications/2016/12/south-sudan-looming-genocide-plans-prevention.

Titeca, K., & Vlassenroot, K. (2012, January 26). Rebels without borders in the Rwenzori borderland? A biography of the Allied Democratic Forces. *Journal of Eastern African Studies, 6*(1), 154-176. Retrieved from https://www.tandfonline.com/doi/pdf/10.1080/17531055.2012.664708.

Tuck, H., & Silverman, T. (2016). The Counter-Narrative Handbook. Institute for Strategic Dialogue. Retrieved from http://www.isdglobal.org/wp-content/uploads/2016/06/Counter-narrative-Handbook_1.pdf.

UN Development Programme (UNDP). (2017). Journey to Extremism in Africa. Retrieved from http://journey-to-extremism.undp.org/content/downloads/UNDP-JourneyToExtremism-report-2017-english.pdf.

United Nations Security Council. (2017, November 2). *Letter dated 2 November 2017 from the Chair of the Security Council Committee pursuant to resolutions 751 (1992) and 1907 (2009) concerning Somalia and Eritrea addressed to the President of the Security Council.* Retrieved from http://www.un.org/ga/search/view_doc.asp?symbol=S/2017/924.

UNSOM. (2017, August 14). *Countering Al-Shabaab Propaganda and Recruitment Mechanisms in*

*South Central Somalia.* Retrieved from https://reliefweb.int/sites/reliefweb.int/files/resources/countering_al-shabaab_propaganda_and_recruitment_mechanisms_report_final_-_14_august_2017.pdf.

Veale, A., & Stavrou, A. (2007). Former Lord's Resistance Army Child Soldier Abductees: Explorations of Identity in Reintegration and Reconciliation. *Peace and Conflict Journal of Peace Psychology,* 13(3), 273-292. https://www.researchgate.net/publication/233165316_Former_Lord%27s_Resistance_Army_Child_Soldier_Abductees_Explorations_of_Identity_in_Reintegration_and_Reconciliation.

Weeraratne, S. (2017, June 27). Jihadists, Rebels or Bandits? The Threat of the Allied Democratic Forces. *Oxford Research Group.* Retrieved from https://sustainablesecurity.org/2017/06/27/jihadists-rebels-or-bandits-the-threat-of-the-allied-democratic-forces/.

Well Told Story. (2016, February 5). *"...It is not about Islam" -Young Kenyans Speak on Radicalisation.* Retrieved from http://www.welltoldstory.com/wp-content/uploads/2016/06/Report-Comic_WTS-HSF-Exploring-Religious-Tolerance-among-Kenyan-Youth_05.02.2016.pdf.

Zeiger, S. (2016, August). *Undermining Violent Extremist Narratives in South East Asia A How-To Guide.* Retrieved from http://www.hedayahcenter.org/Admin/Content/File-3182016115528.pdf.

# KIAMBATANISHO

## Kiambatanisho A

Kuhusu Mradi

## Kiambatanisho B

Taarifa za Simulizi Kinzani

# KIAMBATANISHO A: KUHUSU MRADI

Mradi huu unatumika kupanua Maktaba ya Simulizi Kinzani ya Hedayah kwa kuongeza mkusanyiko unaojikita Afrika Mashariki kama ukanda. Mradi huu unalenga kupangilia, kukusanya na kuchambua simulizi kinzani katika lugha mbalimbali. Mradi kwa ujumla, ikiwa ni pamoja na hatua zilizoainishwa hapa chini, unafadhiliwa na Idara ya Serikali ya Marekani.

Mradi ulihusisha hatua kuu kadhaa:

**Warsha ya Wataalamu kuhusu Simulizi Kinzani kwa ajili ya kukabiliana na ufurutu ada Afrika Mashariki na Pembe ya Afrika**

Ilifanyika tarehe 5-7 Februari mjini Kigali, Rwanda na Hedayah na IGAD Kituo cha Ubora cha Kuzuia na Kukabiliana na Ufurutu Ada (ICEPCVE).

**Utengenezaji wa "Namna ya Kuongoza" kwa ukanda huu inajumuisha:**

Mambo ya uzoefu na mifano ya kukabiliana/simulizi mbadala zinazoendana na ukanda huu

**Mkusanyiko wa simulizi kinzani katika ukanda huu kama kipengere muhimu cha simulizi kinzani mtandaoni kwenye maktaba ya Hedayah.**

<u>**Kuhusu Maktaba ya Simulizi Kinzani**</u>

Kama sehemu ya jitihada zake za kuendeleza desturi bora na mikakati kwa ajili ya simulizi kinzani, Hedayah ilizindua maktaba yake simulizi kinzani Oktoba 2016. Maktaba ni lango la kina ambapo serikali, watalaam na asasi za kiraia wanaweza kupata maudhui, vifaa na mifano bora ili kukabiliana na simulizi za aina zote za ufurutu ada. Maktaba inayolindwa na neno la siri inajumuisha sinema, maaonyesho ya runinga, katuni, vitabu, tovuti, magazeti, blogu, kampeni za mitandao ya kijamii, makala za habari na mifano mingine mingi ya simulizi kinzani.

Toleo la awali lililenga chanzo huru cha simulizi kinzani kwa Al Qaeda. Wakati huo, mradi uliungwa mkono na nchi 8, wakiongozwa na serikali ya Uholanzi, na kukabidhiwa kwa Hedayah mnamo Julai 2015. Kabla ya uzinduzi wa mkutano wa Afrika Mashariki, maktaba inaonyesha mikutano miwili ya kikanda (Asia Kusini Mashariki na MENA), na mada moja (Waasi wa Daesh).
Malengo makuu ya maktaba ya simulizi kinzani ni

- **Kuanzisha** rasilimali ya kina ambapo serikali, watalaamu na asasi za kiraia wanaweza kupata taarifa husika zilizotumika kukabiliana na simulizi aina zote za ufurutu ada.
- **Kuongelea zaidi** simulizi zilizopo dhidi ya wafurutu ada
- **Kukuza** desturi nzuri kushiriki na kuwapa wataalamu rasilimali husika na zana za kukabiliana na simulizi za wafurutu ada

Maktbata ya Hedayah ya simulizi kinzani inaweza kupatikana kupitia www.cn-library.com. Kwa taarifa zaidi kuhusu maktaba, wasiliana na CNLibrary.Admin@hedayah.ae.

# KIAMBATANISHO B: TAARIFA ZA SIMULIZI KINZANI

Kiambatanisho kifuatacho hapa chini ni mkusanyiko wa vyanzo huru vya simulizi kinzani kwa ukanda wa MENA. Maoni yaliyoelezwa kwenye maudhui ya nje hayajaidhinishwa au kuakisi maoni ya Hedayah au Idara ya Serikali ya Watu wa Marekani. Picha zilizotumika ni kwa hisani ya tovuti ya mashirika husika.

| | | |
|---|---|---|
| | **EAST AFRICA** | |
| 1 | PAMOJA FESTIVAL: TOGETHER | CHANYA/MBADALA<br>KIJAMII |
| 2 | COOPERATION CIRCLES | CHANYA/MBADALA |
| 3 | GOLDEN RULE TEACHING | KIDINI<br>KIITIKADI |
| 4 | EAST AFRICA'S SUFI PATH TO CVE | KIDINI<br>KIITIKADI<br>CHANYA/MBADALA |
| | **BURUNDI** | |
| 5 | AMAHORO EGO (YES PEACE) | CHANYA/MBADALA |
| 6 | KUNDUBURUNDI: ESTEEM BURUNDI | CHANYA/MBADALA<br>KIJAMII |
| 7 | ACCORD: SPEAK UP | CHANYA/MBADALA<br>KIJAMII |
| 8 | "WE ARE ACCOUNTABLE" - "FUTURE LEADER" RADIO SHOW | CHANYA/MBADALA<br>KIJAMII |
| 9 | KAZOZA KEZA: UN AVENIR MILLEUR | CHANYA/MBADALA<br>KIJAMII |
| 10 | "RWARUKA TURASHOBOYE": YOUTH WE CAN | CHANYA/MBADALA<br>KIJAMII |
| 11 | CITOYENS RESPONSABLES | CHANYA/MBADALA |
| 12 | IVOMO | CHANYA/MBADALA |
| | **KENYA** | |
| 13 | WATATU | KIJAMII |
| 14 | MENTORSHIP OF VULNERABLE YOUTH IN NAIROBI | CHANYA/MBADALA |
| 15 | RADIO PILOT PROJECT IN KENYA | KIJAMII |
| 16 | TEACHING ANTI-EXTREMISM IN KENYA | KIJAMII |
| 17 | AYUB MOHAMUD, THE TEACHER | KIJAMII |
| 18 | COMMEMORATION OF THE WESTGATE TERROR ATTACK | KIJAMII |
| 19 | TEACHING AGAINST VIOLENT EXTREMISM | KIJAMII |
| 20 | JUST A MINUTE: KWALE EDITION | KIJAMII |
| 21 | SURRENDERED TO EXTREMISTS | KIJAMII |
| 22 | REASON & PROGRESS WITH ME | KIDINI<br>KIITIKADI<br>KIJAMII |
| 23 | THE TARGET | KIJAMII |
| 24 | X KONVICT KONVERT | KIJAMII |
| 25 | #ITHURTSME | KIJAMII |
| 26 | FACE IT | CHANYA/MBADALA |
| 27 | WESTGATE | CHANYA/MBADALA |
| 28 | EXPLORING RELIGIOUS TOLERANCE AMONG YOUNG KENYANS IN NAIROBI & MOMBASA | KIDINI<br>KIITIKADI |
| 29 | THE ALTERNATIVE VOICES PROJECT | KIDINI<br>KIITIKADI<br>CHANYA/MBADALA |
| 30 | TAFAKARI (SHINARS ARTS) | KIDINI<br>KIITIKADI<br>KIKABILA<br>KIUCHUMI |
| | **RWANDA** | |
| 31 | PORTRAITS OF RECONCILIATION | MAADILI<br>KIJAMII |
| 32 | KUREMA, KUREBA, KWIGA | KISIASA<br>KIJAMII<br>KIUCHUMI |
| 33 | FIGHT AGAINST CORRUPTION | KISIASA |
| 34 | YOUTH PARTICIPATION IN RWANDA | KISIASA |
| 35 | PROVIDING EFFECTIVE SOCIO-ECONOMIC PROGRAMS IN RWANDA | KISIASA |
| | **SOMALIA** | |
| 36 | QURACA NABADDA | MAADILI |

| | | |
|---|---|---|
| 37 | LET THEM HEAR YOUR VOICE CAMPAIGN | CHANYA/MBADALA |
| 38 | PREACHING IN PRACTICE: ABDI SHIRE | MAADILI |
| 39 | BAR KULAN RADIO | KIHISTORIA<br>KISISA |
| 40 | SOMALI YOUTH ENTREPRENEURSHIP INITIATIVE | CHANYA/MBADALA<br>ECONOMIC |
| 41 | THE CENTER FOR CONFLICT, GOVERNANCE & PEACEBUILDING | KIHISTORIA<br>KISISA<br>KIUCHUMI |
| 42 | RECONSTRUCTION OF KISMAYO | CHANYA/MBADALA<br>ECONOMIC |
| 43 | DESTROYED LIVES | MAADILI<br>KIJAMII |
| 44 | LOST SOMALIA (STUDENT) ALSHABAB | KIJAMII<br>MAADILI |
| 45 | HUMANITY LOST: SOMALIA RAPPER | KIJAMII |
| 46 | HUMANITY LOST: SOMALIA MECHANIC-ALSHABAAB | KIJAMII<br>MAADILI |
| 47 | HUMANITY LOST: SOMALI JOURNALIST | KIJAMII<br>MAADILI |
| 48 | SOMALI YOUTH AND ELDERS UNITE AGAINST TRIBALISM AND EXTREMISM | KIDINI<br>KIITIKADI |
| 49 | CREDIBLE MESSENGERS | KIKABILA<br>KIDINI<br>KIITIKADI |
| 50 | SOMALI YOUTH DAY | KIKABILA<br>KIJAMII |
| 51 | TUBTA NABADDA | KISIASA<br>KIDINI<br>KIITIKADI |
| 52 | DIGITAL COUNTER-EXTREMISM CENTER: SOMALIA | KISIASA |
| 53 | SHABAAB MEN TURN KENYAN SCHOOLGIRLS INTO SEX SLAVES | KIJAMII |
| 54 | THE SEX SLAVES OF AL SHABAAB | KIJAMII |
| 55 | WHY I LEFT AL-SHABAAB | KIJAMII |
| 56 | STORIES OF SURVIVORS OF VIOLENT EXTREMISM: SOMALIA | KIJAMII |

| | | |
|---|---|---|
| 57 | RETURN TO SOMALIA: ALIYA'S STORY | MAADILI<br>KIHISTORIA<br>KISIASA |
| 58 | THIS WAS NOT 'JUST ANOTHER BOMB IN MOGADISHU.' | KIHISTORIA<br>KISIASA |
| 59 | DROP THE GUN, PICK UP THE PEN | KIJAMII<br>KIUCHUMI |
| 60 | IS THE REAL PROBLEM TO GROW BEARDS? | KIJAMII<br>KIDINI |
| 61 | THE POET NATION | KIJAMII |
| 62 | A BETTER LIFE THAN TODAY | CHANYA/MBADALA |
| 63 | MAYOR OF MOGADISHU | KIHISTORIA<br>KISIASA |
| **SUDANI KUSINI** | | |
| 64 | SOUTH SUDAN: TWO TRIBES REBUILD WHAT VIOLENCE DEMOLISHED | KIKABILA |
| 65 | REFORMING MIRACLES: SOUTH SUDAN REFUGEES FIND HOPE IN THEATER | CHANYA/MBADALA |
| 66 | ANA TABAN (I AM TIRED) | CHANYA/MBADALA |
| 67 | #ANATABAN OFFICIAL VIDEO: SOUTH SUDAN MUSIC | CHANYA/MBADALA |
| 68 | SOUTNA (OUR VOICE): SOUTH SUDAN MUSIC | CHANYA/MBADALA |
| 69 | MALESH (SORRY): SOUTH SUDAN MUSIC | CHANYA/MBADALA |
| 70 | #DEFYHATENOW | KIKABILA |
| **JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA** | | |
| 71 | VIJANA NA AMANI (YOUTH AND PEACE) CAMPAIGN | KIKABILA<br>CHANYA/MBADALA |
| 72 | STOP THE VIOLENCE | KIJAMII |
| 73 | 11 SHABAAB 'RECRUITS' ARRESTED AFTER REPORTS OF SECRET DRILLS | KIHISTORIA<br>KISIASA<br>KWELI |
| 74 | EXPLOSION IN NORTHERN TANZANIA BAR INJURES 15 | KIHISTORIA<br>KISIASA<br>KWELI |
| 75 | TWO BRITISH GIRLS ATTACKED BY MUSLIMS WITH ACID IN ZANZIBAR | KWELI<br>KIUCHUMI |

| | | |
|---|---|---|
| 76 | TANZANIA MOSQUE ATTACK | KWELI |
| 77 | RELIGIOUS CONFLICTS IN TANZANIA | KWELI |
| 78 | TERRORIST TRAINING IN TANZANIA | KIHISTORIA<br>KISIASA<br>KWELI |
| 79 | ONE FAMILY UNDER GOD | CHANYA/MBADALA |
| 80 | AMANI KWANZA (PEACE IS PRIORITY) | CHANYA/MBADALA |
| 81 | OKOA KITAA (STAND FOR COMMUNITY) | CHANYA/MBADALA |
| 82 | AMANI HUANZIA NYUMBANI (PEACE BEGINS IN THE HOME) | CHANYA/MBADALA |
| 83 | DINI MBALIMBALI UMOJA NA UPENDO (DIFFERENT RELIGIONS PEACE AND LOVE) | CHANYA/MBADALA<br>KIDINI<br>KIITIKADI |
| 84 | KIJANA BADILI MWENDO ACHANA NA TABIA HATARISHI (YOUTH ABANDON RISKY BEHAVIOR) | CHANYA/MBADALA |
| 85 | NAKUPENDA TANZANIA | CHANYA/MBADALA |
| **UGANDA** | | |
| 85 | ISLAM AND POSITIVE YOUTH DEVELOPMENT | CHANYA/MBADALA<br>MAADILI |
| 86 | STUDENT CONNECTORS | CHANYA/MBADALA |
| 87 | INTERFAITH YOUTH RETREAT | CHANYA/MBADALA<br>KITEOLOJIA<br>KIHISTORIA<br>KISIASA<br>KIJAMII<br>MAADILI |
| 88 | AMANI LEO | CHANYA/MBADALA |
| 89 | STORIES OF SURVIVORS OF VIOLENT EXTREMISM: UGANDA | KIJAMII |
| 90 | ANNUAL NATIONAL INTERFAITH HARMONY WALK | KIJAMII |
| 91 | KONY 2012: INVISIBLE CHILDREN | KISIASA<br>KIDINI<br>KIITIKADI |

**Chanya/Mbadala inamaanisha aina ya simulizi kinzani chanya au mbadala. Taarifa kwenye safu hii inaeleza aina ya kila simulizi kinzani.*

# KIAMBATANISHO 2 :TAARIFA ZA SIMULIZI KINZANI

## AFRIKA MASHARIKI




**SHEREHE YA PAMOJA**

| | |
|---|---|
| HADHIRA KUSUDIWA | Hadhira ya jumla |
| MASHIRIKA HUSIKA | PamojaFest |

**MJUMBE**
Viongozi wa jamii

**NJIA YA MAWASILISHO**
Ukurasa waMitandao ya ki-jamii, Tukio, Blogu

Swahili Kifaransa

Chanya/ mbadala Kijamii

**UJUMBE**

Ujumbe huu unatumika kwa ajili ya kukuza umoja na mshikamano wa kijamii kupitia muziki. Ujumbe mkuu unasambazwa kupitia tamasha la muziki. Jamii inatumia tamaduni za kusambaza ujumbe kwa mdomo ambayo hufanya muziki njia sahihi ya kufikisha ujumbe kwa mabadiliko ya kijamii. Tamasha ni la ngazi ya mkoa likishirikisha wasanii wa wilaya kwenye uimarishaji wa amani na uhamasishaji wa jamii shirikishi. Tamasha la muziki hufanyika mara kwa mara kila mwaka na linahusisha ushiriki wa wana-jamii. Ujumbe unaotolewa unalenga kureje-sha mahusiano ya watu yalivonjwa kwa migogoro ya vurugu na mitazamo ya chuki na kisasi ndani ya jamii. Mtindo wa muziki ni wa injili na unasherehesha utamaduni wa muziki wa kirundi kwa ajili ya eneo hilo.

http://bit.ly/2JZCxe3



**MAKUNDI YA USHIRIKIANO**

| | |
|---|---|
| HADHIRA KUSUDIWA | Hadhira ya jumla |
| MASHIRIKA HUSIKA | URI - Horn of Africa |

**MJUMBE**
Viongozi wa jamii

**NJIA YA MAWASILISHO**
Majadiliano ya wazi

Kifaransa

Chanya/ mbadala

**UJUMBE**

Jitiahada za Umoja wa Kidini (URI) huan-daa majadiliano ya mara kwa mara katika "Makundi ya Ushirikiano " na vijana juu ya kupambana na ufurutu ada, uendelezaji wa amani, na maendeleo katika jamii zao. URI hutoa nafasi kwa vijana kuchangia mawazo kuhusu kushawishiwa na ujumbe kinzani.

https://bit.ly/2M95dSP




**MAFUNDISHO YA KANUNI YA D HAHABU**

Kiingereza

Kidini Kiitikadi

| | |
|---|---|
| HADHIRA KUSUDIWA | Hadhira ya Jumla |
| MASHIRIKA HUSIKA | URI - Horn of Africa |

**MJUMBE**

Viongozi wa jamii

**NJIA YA MAWASILISHO**

Bango, Tukio

**UJUMBE**

Bango hili linaeleza taarifa muhimu kuhusu dini za ulimwengu kwenye maadhimisho ya “Siku ya kanuni ya dhahabu” tarehe 5 Aprili. Bango linahimiza pia maadhimisho ya umoja wa mataifa kwenye siku ya kimataifa ya amani na wiki ya maelewano baina ya dini ulimwenguni. Bango linasisitiza kutenda kulingana na “Kanuni ya dhahabu” na linatoa nukuu kutoka kila dini ili kumuunga mkono kuwatendea wengine kwa wema na upendo.



**SAFARI YA SUFI KUPAMBANA NA UFURUTU ADA AFRIKA MASHARIKI**

Kiingereza

Kidini Kiitikadi Chanya/ mbadala

| | |
|---|---|
| HADHIRA KUSUDIWA | Watu Wengi- Hadhira ya Waislamu, Watafutaji |
| MASHIRIKA HUSIKA | Pieter Hugo and Susan Dominus |

**MJUMBE**

Viongozi wa Jamii

**NJIA YA MAWASILISHO**

Makala za habari

**UJUMBE**

Kundi la maulamaa wa Kisufi walikutana katika mkutano wa siku tatu Agosti 2015 kujadili ufurutu ada Afrika Mashariki. Mkutano wa viongozi wa kidini wa Kisufi uliafiki kwamba Usufi Afrika Mashariki unapinga ugaidi, na wajumbe zaidi ya 300 walijadili njia za kidini ambazo zingeweza kupiga vita ufurutu katika kanda. Kwa mfano, washiriki kwenye mkutano walipendekeza kwamba usufi ni tiba ya ubaguzi na kutovumiliana.

https://bit.ly/2Lym7e7

## BURUNDI



### AMAHORO EGO (NDIO AMANI)

**HADHIRA KUSUDIWA**: Wenye imani isiyo Badilika (Wahusika)

**MASHIRIKA HUSIKA**: UNOHCHR

**MJUMBE**
Serikali

**NJIA YA MAWASILISHO**
Tovuti, blogu, Tukio

Kifaransa

Chanya/ Mbadala

**UJUMBE**

Simulizi kinzani hii inataka kudhoofisha utashi wa pamoja wa vurugu kutokana na uvivu, ukosefu wa ajira na malalamiko ya kisiasa nchini Burundi. Ili kuhamasisha uwajibikaji wa vijana kuchangia binafsi na kwa pamoja kwenyeamani, Ofisi ya Kamishna wa Umoja wa Mataifa ya haki za binadamu imeandaa kaulimbiu: ʼndio kwa amaniʼ kama sehemu ya kampeni. Marudio ya dhana hii, hasa wakati wa siku ya uhamasishaji, imeamsha uelewa wa pamoja wa vijana na Shirika la Umoja wa mataifa limealika vijana kuelekeza umakini wao kuelekea urudishaji na uimarishaji wa amani. Wanafunzi na vijana wanaalikwa kusema ʼndio kwa amaniʼ na hapana kwa njia za vurugu za kuonyesha kukata tamaa.

https://bit.ly/2ttEh8D



### KUNDU BURUNDI: BURUNDI YA HESHIMA

**HADHIRA KUSUDIWA**: Hadhira ya Jumla

**MASHIRIKA HUSIKA**: Christian Life Ministries Bujumbura

**MJUMBE**
Viongozi wa jamii

**NJIA YA MAWASILISHO**
Tukio, Blogu, Fulana

Kirundi

Chanya/ mbadala Kijamii

**UJUMBE**

Ujumbe KunduBurundi unawataka vijana kupenda nchi yao na kuijenga, kuiadilisha, badala ya kuiangamiza. Inatumia misingi ya kikristo iliyopo, lakini pia kuziwasilisha kwa njia ya utulivu kupitia kampeni kama vile wakati wa matukio na kwenye fulana ambazo zinasambazwa kwenye vyuo vyote nchini Burundi.

https://bit.ly/2MBWQzV



ACCORD: ZUNGUMZA

| | |
|---|---|
| HADHIRA KUSUDIWA | Hadhira ya Jumla |
| MASHIRIKA HUSIKA | TUBIYAGE Association |

MJUMBE
Viongozi wa jamii

NJIA YA MAWASILISHO
Vipande vya sinema, Tukio

Kifaransa

Chanya/ mbadala Kijamii

UJUMBE

Simulizi kinzani hii ni ujumbe uliokusudiwa kuvunja ukimya, kuwaleta wanajamii, kupitia maigizo na sanaa za maonyesho ndani ya jamii, kujieleza wenyewe katika hali halisi, changamoto na madhila ya kijamii yanayozuia maisha ya watu. Sanaa shirikishi hutoa fursa kwa wanajamii kujielezea kwa maneno na ishara zinazoonyesha tabia na mitazamo chanya ambavyo vinaweza kuchukuliwa ndani ya jamii.

https://bit.ly/2M5Ip67

Colombe FM 93.2

"TUNAWAJIBIKA" - "VIONGOZI WA KESHO"KIPINDI CHA REDIO

| | |
|---|---|
| HADHIRA KUSUDIWA | Hadhira ya Jumla |
| MASHIRIKA HUSIKA | Centre Jeunes KAMENGE |

MJUMBE
Community Leaders

NJIA YA MAWASILISHO
Redio

Kifaransa

Chanya/ mbadala Kijamii

UJUMBE

Kipindi cha redio "KIONGOZI WA KESHO" Kinaendeshwa kupitia kituo cha redio kinachoitwa COLOMBE. Ni redio ya kwanza ya vijana, inayoendeshwa na vijana nchini Burundi, inafadhiliwa na kusaidiwa na UNFPA. Inaongelea migogoro ya kijamii kama vile kutokuheshimu mali ya wengine au kutokuheshimu haki za binadamu wengine. Simulizi inakuza na inasisitiza uwajibikaji wa vijana kwa wanajamii na inahimiza kikamilifu watu kufikiria wengine kama wao wenyewe.

https://bit.ly/2ks980y



**KAZOZA KEZA: MAISHA BORA YA BAADAE**

| | |
|---|---|
| HADHIRA KUSUDIWA | General Audience |
| MASHIRIKA HUSIKA | Leo Burundi |

Kirundi

Chanya/ mbadala Kijamii

**MJUMBE**

Viongozi wa jamii

**NJIA YA MAWASILISHO**

Tukio, vipande vya sinema

**UJUMBE**

Ujumbe ulitumika kupandikiza kwenye ufahamu wa vijana na watu shupavu kwamba kuna matumaini ya maisha bora ya baadaye. Simulizi ya kupambana inataka kuonyesha kwamba vijana wanaweza kujihusisha na kuwekeza katika maisha bora ya baadaye wao wenyewe na jamii zao. Katika muktadha wa Burundi, maisha bora ya baadaye ni pamoja na amani, mshikamano wa kijamii na ustawi kwa ujumla (elimu, masuala ya uchumi).

https://bit.ly/2KaZmPc



**"RWARUKA TURASHOBOYE": VIJANA TUNAWEZA**

| | |
|---|---|
| HADHIRA KUSUDIWA | Hadhira ya Jumla, Watafutaji |

Kirundi

Chanya/ mbadala Kijamii

**MJUMBE**

Viongozi wa jamii

**NJIA YA MAWASILISHO**

Methali

**UJUMBE**

Kitamaduni, methali katika Kirundi zinaonyesha kwamba vijana ni nguvu ya mabadiliko katika siku zijazo, wanabaguliwa na kunyonywa hasa na watu hasidi ambao wanalenga maslahi yao wenyewe. Hali hii hufanya vijana kutenda chini ya amri ya watu waerevu zaidi wanaochukulia fursa ya kutokuwa na uwezo na kutokuwa na usalama kwao. Maelezo haya yanakusudia kuamsha vijana kuonyesha kwamba wanaweza leo. Umoja ni nguvu, lakini nguvu hii ya vijana mara nyingi imezoeleka kwa njia hasi ambapo hutumika kwa ajili ya maslahi ya wanasiasa na watu wanaofanya kazi kwa bidii. Ujumbe unataka kiasi kikubwa kubadilisha ukweli huu ili kuthibitisha kwamba vijana wako imara na wanajumuisha nguvu kazi kubwa ya taifa, muhimu hapa na sasa, kwa ajili ya mabadiliko chanya.



**WANANCHI WASIMAMIZI:** *mafunzo ya viongozi vijana ya vyama vya siasa na asasi za kiraia nchini Burundi*

Kifaransa

Chanya/ mbadala

**HADHIRA KUSUDIWA** General Audience

**MASHIRIKA HUSIKA** UNESCO

**MJUMBE**

Viongozi wa Jamii, Vijana

**NJIA YA MAWASILISHO**

Ripoti

**UJUMBE**

Mradi huu ulifanywa na UNESCO chini ya House of Culture and Peace Bujambura. Mradi huo ni pamoja na warsha ya mafunzo ya vijana kitaifa, na ujumbe ukitumika kwa ajili ya ushiriki bora wa makundi yote ya kijamii katika kutatua matatizo ya kijamii na kuijenga upya nchi katika Burundi. Baadhi ya masomo yaliofanywa na warsha hii ya mafunzo ya vijana kitaifa ni pamoja na: kukuza ulinzi wa pamoja na misaada ya pamoja, huruma katika uso wa uduni wa wengine na mchango wa wanajamii kusaidia wahitaji zaidi hasa wahanga wa mifumo ya kijamii na kisiasa ya vurugu kwa sababu kinachofanyika kwa wengine hakiwezi kupita bila matokeo katika mazingira yake.

https://bit.ly/2LDn8BA



**IVOMO**

Kirundi

Chanya/ mbadala

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya Jumla

**MJUMBE**

Viongozi wa jamii, Vijana

**NJIA YA MAWASILISHO**

Tovuti

**UJUMBE**

Katika tovuti hii, vijana wakirundi wanaweza kuanzisha mazungumzo baina yao kuhusu mada ambazo ni muhimu kwao kwenye jamii yao, wakibadilishana mawazo, na kupeana taarifa kuhusu fursa. Jukwaa hili linatoa nafasi mbadala kushughulikia malalamiko na masuala mengine.

www.ivomo.net

## KENYA



### WATATU

**HADHIRA KUSUDIWA:** Watafutaji, Hadhira Jumla & hadhira kubwa ya Waislamu

**MASHIRIKA HUSIKA:** S.A.F.E. Kenya

**MJUMBE:** Familia

**NJIA YA MAWASILISHO:** Vipande vya sinema, Makala

Swahili

Kijamii

**UJUMBE**

Hadithi ya Watatu inaelezea hadithi ya Yusuf na familia yake mjini Mombasa, Kenya. Yusuf anaanza kusoma magazeti kutoka Al-Shabaab na anataka kusafiri kwenda Somalia. Familia yake, inataabika na kufedheheshwa, ikijaribu kutafuta suluhisho la yeye kujiunga na kikundi cha kigaidi. Filamu iliwekwa kwa nia ya kuanza mazungumzo ya jamii, na maonyesho ya filamu ni pamoja na ufuatiliaji wa kufanyika kwa sanaa za maonyesho ambazo zinaruhusu hadhira kuchagua hitimisho la filamu wao wenyewe. Wahusika halisi wa igizo ni mama yakeYusuf, dada na mjomba kuamua mwisho mpya na kutoa sauti kwa wananchi wa Mombasa moja kwa moja.

http://bit.ly/2llXlSx

https://imdb.to/2loaiv0



### KUWAFUNDISHA VIJANA WALIO HATARINI NAIROBI

**HADHIRA KUSUDIWA:** Wathibitishaji, Wasikitikaji, Watafutaji

**MASHIRIKA HUSIKA:** STRIVE HoA

**MJUMBE:** Viongozi wa Jamii

**NJIA YA MAWASILISHO:** Taarifa

Kiingereza

Chanya/ Mbadala

**UJUMBE**

Kwa kushirikiana na asasi za kiraia wenyeji, STRIVE HoA, ilizindua mpango wa majaribio wa ushauri kwa vijana Eastleigh na Majengo mjini Nairobi. Mpango uliwatambua vijana 20 waliokuwakwenye hatari ya kushawishiwa kulingana na sababu mbalimbali. Kila kijana aliunganishwa na mshauri. Mpango ulionekana kuwa na mafanikio sana na endelevu kwa wenyewe, kwa tahadhari moja kwamba mara nyingi ni vigumu kupata mshauri ambaye yuko tayari na wa kuaminika. Washauri wenye mafanikio zaidi walikuwa wale waliokuwa wafurutu ada wa zamani, ambao wangeweza kuzungumzia hali halisi ya kushawishiwa.

http://bit.ly/2thTr1t



MRADI WA MAJARIBIO WA REDIO KENYA

HADHIRA KUSUDIWA: Watafutaji, Hadhira ya Jumla & Jumla-Wengi hadhira ya Waislamu

MASHIRIKA HUSIKA: STRIVE HoA

MJUMBE: Viongozi wa jamii

NJIA YA MAWASILISHO: Taarifa

Swahili

Kijamiii

**UJUMBE**

STRIVE HoA ilitangaza vipindi vinne redioni vya hadithi na mipango minne ya kidini (iliratibiwa na viongozi wa wadini walioelimika kwa wastani) ikilenga kwenye masuala yanayohusiana na kushawishiwa huko Mombasa. Vipindi vilijaribu kujenga uelewa kuhusu mbinu zinazotumiwa na waandikishaji wa ufurutu ada. Zaidi ya hayo, kushirikishana simulizi za waathirika na familia, vipindi vilitaka kuonyesha hali halisi hasi ya kushawishiwa.

http://bit.ly/2JZCxe3





KUFUNDISHA DHIDI YA UFURUTU KENYA

HADHIRA KUSUDIWA: Hadhira ya jumla

MASHIRIKA HUSIKA: The New Yorker

MJUMBE: Viongozi wa jamii, Vyombo vya habari

NJIA YA MAWASILISHO: Makala za habari

Kiingereza

Kijamii

**UJUMBE**

Makala hii ya habari ni mfano wa namna elimu ilivyo moja ya silaha yenye nguvu kupinga ujumbe wa ufurutu, ikitoa mfano wa muktadha wa Kenya. Elimu husaidia kuwezesha wavulana na wasichana kuhoji jumbe za kifurutu na kuzikataa. Pia inaweza kutengeneza majadiliano kuhusu vikundi vya kifurutu ada ambako uandikishaji unafanyika na kuwapa wanafunzi mikakati ya kuepuka simulizi zao.

http://bit.ly/2K4n8cq




**AYUB MOHAMUD, MWALIMU**

| | |
|---|---|
| HADHIRA KUSUDIWA | Vijana |
| MASHIRIKA HUSIKA | Eastleigh Community & CCTV Africa Story |
| MJUMBE | Viongozi wa Jamii |
| NJIA YA MAWASILISHO | Vipande vya sinema |

Kiingereza

Kijamii

**UJUMBE**

Ayub Mohamud ni mwalimu wa masomo ya biashara na elimu ya dini ya Kiislamu kwenye shule ya sekondari ya Eastleigh, Nairobi Kenya. Alikuwa miongoni mwa wahitimu 10 bora kwenye tuzo ya kimataifa ya mwalimu mwaka 2016. Kama mwalimu, amekabiliana na ufurutu ada katika jamii yake kupitia elimu, akichangia kutatua matatizo ndani ya jamii yake. Kipande cha sinema kinasimulia kisa chake.

http://bit.ly/2I4nH4g

http://bit.ly/2M3LQdA




**KUMBUKIZI YA SHAMBULIO LA WESTGATE**

| | |
|---|---|
| HADHIRA KUSUDIWA | Hadhira ya Jumla, Vijana hatarini |
| MASHIRIKA HUSIKA | Community Development Initiative |
| MJUMBE | Viongozi wa Jamii |
| NJIA YA MAWASILISHO | Vipande vya sinema, Tukio |

Kiingereza

Kijamii

**UJUMBE**

Sinema hii inaonyesha mfululizo wa hadithi za habari ya namna wanajamii wa Eastleigh walivyoadhimisha kumbukumbu ya shambulio la Westgate na kulaani ugaidi. Tukio hili lilifanywa na jamii linaonyesha kwamba jamii haikubali matumizi ya vurugu, na ishara wakati wa maandamano zinadhihirisha kwamba hawaamini kwamba Uislamu unaruhusu kushawishiwa na ugaidi. Tukio liliandaliwa na Community Development Initiative, asasi ya wenyeji ipo mstari wa mbele kupambana na ufurutu ada.

http://bit.ly/2llatqQ




KUFUNDISHA DHIDI YA UFURUTU ADA

Swahili

Kijamii

| | |
|---|---|
| HADHIRA KUSUDIWA | Hadhira ya Jumla, Vijana na Jamii hatarini |
| MASHIRIKA HUSIKA | Walimu dhdi ya Ufurutu Ada |

**MJUMBE**

Viongozi wa Jamii

**NJIA YA MAWASILISHO**

Vipande vya Sinema

**UJUMBE**

Chanzo hiki kinaelezea namna mwalimu mmoja, Ayub Mohamud, anavyopambana na ushawishi na ugaidi darasani. Video inaanika simulizi ya Al-Shabaab kwamba wanapambana na mataifa ya Afrika kwa sababu ya uvamizi wa magharibi, na inatoa baadhi ya mapendekezo ya namna ya kukabiliana na simulizi hizo kupitia maneno na matendo darasani.

http://bit.ly/2tm9nPm




NGOJA PUNDE: TOLEO LA KWALE

Swahili
Tafsiri ya Kiingereza

Kijami

| | |
|---|---|
| HADHIRA KUSUDIWA | Watafutaji, Hadhira ya Jumla |
| MASHIRIKA HUSIKA | #insolidarity, YADEN East Africa |

**MJUMBE**

Viongozi wa Jamii

**NJIA YA MAWASILISHO**

Vipande vya sinema

**UJUMBE**

Wanawake wawili kutoka Kaunti ya Kwale mjini Mombasa wanashirikishana hadithi zao na kukutana na ugaidi. Wanazungumzia juu ya namna vijana walivyokuwa wameajiriwa kwenye makundi ya kigaidi na hatari inayoikabili jamii yao kuhusiana na ufurutu ada.

http://bit.ly/2yty9Tq



KUJISALIMISHA KWA WAFURUTU

**HADHIRA KUSUDIWA** Wathibitishaji, Wasikitikaji, Watafutaji, Hadhira ya Jumla

**MASHIRIKA HUSIKA** The Guetto Marvellous

**MJUMBE**

Viongozi wa Jamii, (Familia)

**NJIA YA MAWASILISHO**

Vipande vya Sinema

Swahili
Tasfiri za Kiingereza

Kijamii

**UJUMBE**

Filamu hii fupi inaonyesha majadiliano katika familia. Mama na Baba wanalalamika kwa sababu kijana mkubwa hana ushirikiano kwenye nyumba. Familia inatoka kwnye makazi duni ya Mathare jijini Nairobi. Wazazi wote wawili wanamfukuza nyumbani. Hali kama hiyo inatokea katika familia nyingine, lakini awamu hii ni binti ambaye anafukuzwa nyumbani. Ufafanuzi wa hadithi hizi mbili uonyesha namna wanavyoweza kukumbana na ubaguzi katika mazingira mengine kwenye jamii zao na namna ubaguzi huanza. Watu hawa wawili wanaishia kujiunga na kundi la wafurutu.

http://bit.ly/2JZCxe3




SABABU NA ENDELEA NA MIMI

**HADHIRA KUSUDIWA** Watafutaji, Wathibitishaji, Wasikitikaji

**MASHIRIKA HUSIKA** Liberty Studios, Credible Local Voices

**MJUMBE**

Viongozi wa Jamii

**NJIA YA MAWASILISHO**

Vipande vya Sinema

Swahili
Tafsiri ya Kiingereza

Kidini
Kiitikadi

**UJUMBE**

Kwenye ujumbe huu, kijana anaondoka gerezani baada ya kuwa amerekebishwa. Wakati anarejea nyumbani, familia yake inamkataa. Kanisani pia anakataliwa. Kimsingi anakataliwa kokote aendako. Kundi la marafiki linamkubalia, na kumtambulisha katika kundi la kigaidi. Kwa sababu hii anaamua kuwa na hasira na jamii kwa kutekeleza mashambulizi ya kigaidi. Sinema hii inajaribu kulenga shughuli za kigaidi za vijana na jinsi vijana wanavyokabiliwa na hatari ya kujiunga na makundi kama hayo.

http://bit.ly/2M7LCCi




WALENGWA

**HADHIRA KUSUDIWA** Watafutaji, Wathibitishaji, Wasikitikaji

**MASHIRIKA HUSIKA** Liberty Studios

**MJUMBE**

Viongozi wa Jamii

**NJIA YA MAWASILISHO**

Vipande za Sinema

Kiingereza

Kijamii

**UJUMBE**

Sinema hii fupi inaonyesha hadithi ya kijana ambaye yupo njiapanda kati ya kufuata marafiki zake na kutafuta kazi ya uchezaji ngoma, au kujiunga na kikundi cha wafurutu. Mwishoni anaamua kufuata kikundi cha wafurutu, lakini pia inaonyesha madhila na huzuni ya yeye kujiunga.

http://bit.ly/2MDB6DU




X KONVICT KONVERT

**HADHIRA KUSUDIWA** Watafutaji, Wathibitishaji, Wasikitikaji

**MASHIRIKA HUSIKA** The Real Thespians

**MJUMBE**

Viongozi wa Jamii

**NJIA YA MAWASILISHO**

Vipande vya Sinema

Kiingereza

Kijamii

**UJUMBE**

Kwenye ujumbe huu, kijana anaondoka gerezani baada ya kuwa amerekebishwa. Wakati anarejea nyumbani, familia yake inamkataa. Kanisani pia anakataliwa. Kimsingi anakataliwa kokote aendako. Kundi la marafiki linamkubalia, na kumtambulisha katika kundi la kigaidi. Kwa sababu hii anaamua kuwa na hasira na jamii kwa kutekeleza mashambulizi ya kigaidi. Sinema hii inajaribu kulenga shughuli za kigaidi za vijana na jinsi vijana wanavyokabiliwa na hatari ya kujiunga na makundi kama hayo.

http://bit.ly/2ljqq0c




#INANIUMIZA

Swahili
Kiingereza

Kijamii

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla, Watafutaji

**MASHIRIKA HUSIKA** Afrika Moja

**MJUMBE**

Viongozi wa jamii, Vijana

**NJIA YA MAWASILISHO**

Kaulimbiu ya kampeni

**UJUMBE**

Kauli mbiu ya kampeni iliandaliwa pamoja na ICEPVE ili kuzuia vurugu nchini Kenya. Iliwekwa kwenye mitandao ya kijamii kwenye jukwaa la vijana kuongeza uelewa wa vurugu katika jamii na kuwahamasisha vijana kuzungumza kuhusu hilo.

http://bit.ly/2K28JNZ




ITIZAME

Swahili

Chanya/
Mbadala

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla, Watafutaji

**MASHIRIKA HUSIKA** Liberty Studios, YADEN East Africa

**MJUMBE**

Viongozi wa jamii

**NJIA YA MAWASILISHO**

Albamu ya muziki

**UJUMBE**

Albamu ya muziki ikijumuisha orodha ya nyimbo za wasanii mbalimbali waliotolewa kutoka mahali ambapo vijana mara nyingi huajiriwa nchini Kenya. Nyimbo za ujumbe wa kupinga kushawishiwa na za amani. Kwa ujumla, nyimbo ni za kusisimua na za kisasa.

http://bit.ly/2ta9qyf



**WESTGATE**

| | |
|---|---|
| HADHIRA KUSUDIWA | Hadhira ya jumla, Watafutaji |
| MASHIRIKA HUSIKA | Liberty Studios, YADEN East Africa |

**MJUMBE**

Viongozi wa jamii

**NJIA YA MAWASILISHO**

Albamu ya muziki

Swahili

Chanya/ Mbadala

**UJUMBE**

Albamu ya muziki ikijumuisha orodha ya nyimbo za wasanii mbalimbali waliotolewa kutoka mahali ambapo vijana mara nyingi huajiwa na wafurutu ada nchini Kenya. Nyimbo ni za ujumbe wa amani kupambana na ajira za vikundi vya kigaidi. Kwa ujumla nyimbo ni za kuleta uchangamfu na kufurahi.

http://bit.ly/2K5BlcA



**KUCHUNGUZA UVUMILIVU WA KIDINI KWA VIJANA WA KENYA NAIROBI NA MOMBASA**

| | |
|---|---|
| HADHIRA KUSUDIWA | Hadhira ya Jumla |
| MASHIRIKA HUSIKA | Well Told Story |

**MJUMBE**

Viongozi wa Jamii

**NJIA YA MAWASILISHO**

Ripoti ya vichekesho

Kiingereza

Kidini Kiitikadi

**UJUMBE**

Utafiti huu uliofanywa na Hanns Seidel Foundation na Well Told Story ulianga-lia uvumilivu wa kidini huko Mombasa na Nairobi. Utafiti uligundua kwamba kuna uvumilivu wa kidini kidogo, na migogoro kati ya Waislamu na Wakristo mara nyingi huletwa na watu wa nje. Hii hudhoofisha ujumbe ambao wafurutu ada hujaribu ku-utoa kwa lengo la kuigawanya jamii katika misingi ya imani. Matokeo ya utafiti na mahojiano yalifanywa kuwa katika ripoti ya vichekesho.

http://bit.ly/2MHukNu

http://bit.ly/2I3zm3m



MRADI WA SAUTI MBADALA

**HADHIRA KUSUDIWA** Watafutaji, Hadhira ya Jumla, Jumla ya Wengi-Hadhira ya

**MASHIRIKA HUSIKA** STRIVE HoA

**MJUMBE**
Viongozi wa Jamii

**NJIA YA MAWASILISHO**
Ripoti

English

Kidini Kiitikadi Chanya/ mbadala

**UJUMBE**

STRIVE HoA iliajiri maimamu kadhaa na ukhtis na kuwapatia mafunzo ya kuwajengea uwezo kuhusiana na mchakato wa ushawishi binafsi. Aidha, walipata mafunzo juu ya mada pendwa na vijana. STRIVE HoA pia ilitoa mafunzo kwa vijana ili waweze kutengeneza mbinu za ufuatiliaji kujifunza namna maimamu walivyoandaa mahubiri yao na namna jamii ilivyokuwa ikiyapokea.

http://bit.ly/2thTr1t



TAFAKARI (SANAA YA SHINARS)

**HADHIRA KUSUDIWA** Wathibitishaji, Wasikitikaji, Watafutaji, Hadhira ya Jumla

**MASHIRIKA HUSIKA** #insolidarity, Shinars Arts

**MJUMBE**
Viongozi wa Jamii, Vijana

**NJIA YA MAWASILISHO**
Vipande vya Sinema

Swahili
Tafsiri ya Kiingereza

Kidini Kiitikadi Kikabila Kiuchumi

**UJUMBE**

Hadithi hii inatumia Shairi (ushairi/wimbo) ili kufikisha ujumbe, na inawasilishwa kwa njia ya sinema kwa kupitia simu ya mkononi ya vijana kama sehemu ya YADEN #kwamshikamano Mradi wa kuzuia /kupambana na ufurutu ada.

Hadithi inaenda kama ifuatavyo: Kuna mhubiri mpya wa kidini kwenye mji. Analenga vijana wawili wanaofanya kazi kwenye machimbo na ujumbe wa utakaso wa kidini na kikabila. Mawazo yao ya msimamo mkali yaliwaongoza kuwalenga wale wanaotoka dini tofauti na asili ya kikabila. Pia wamesha ahidiwa pesa kwa ajili ya ushujaa wao. Baadaye mamlaka inaingilia kati baada ya vijana kufuatiliwa na jamii juu ya mipango yao miovu, kutoa taarfifa ya muandikishaji ambaye amekamatwa.

http://bit.ly/2JZCxe3

## RWANDA



**PICHA YA UPATANISHO**

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya Jumla, Hadhira ya Waisilamu wengi na wachache, Watafutaji

**MASHIRIKA HUSIKA** Pieter Hugo and Susan Dominus

**MJUMBE**
Wahanga, Manusura, Wasaliti, Wamwanzo

**NJIA YA MAWASILISHO**
Tovuti, Mtumizi ya sanaa

Kiingereza

Kikabila Kijamii

**UJUMBE**

Mfululizo huu wa picha na michoro unaonyeshwa kwenye New York Times, na unajumuisha simulizi na picha za wakosaji wote na waathirika wa mauaji ya kimbari ya Rwanda. Hadithi zinaonyesha matukio ya msamaha, upatanisho na hamu ya kuelekea jamii yenye amani zaidi. Baadhi ya washirika ni wakosaji moja kwa moja wa vurugu dhidi ya manusura. Kwa mfano, Godefroid Mudaheranwa inaonyesha ni jirani wa Evasta Mukanyandwi -Mudaheranwa moja kwa moja anajaribu kuchoma nyumba ya Mukanyandwi, lakini Mukanyandwi hatimaye alimsamehe Mudaheranwa baada ya kuachiwa kutoka jela.

https://nyti.ms/2of9U40



**KUREMA, KUREBA, KWIGA**

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya Jumla, Watafutaji

**MASHIRIKA HUSIKA** Kurema, Kureba, Kwiga

**MJUMBE**
Viongozi wa Jamii, Wasanii

**NJIA YA MAWASILISHO**
Facebook, Sanamu

Kiingereza

Kisiasa Kijamii Kiuchumi

**UJUMBE**

Kurema, Kureba, Kwiga (Kutengeneza, Kuangalia, Kujifunza) ni mradi wa sanaa wa jamii ambao unashughulikia masuala ya kijamii nchini Rwanda. Unafanya hivyo kuonyesha masuala haya katika sanamu zinazotengenezwa na wasanii wenyeji na kupakwa rangi na wanajamii. Pia ni jukwaa la mtandaoni kwenye Facebook na Tumblr ambayo inakuza aina mbalimbali za sanaa nchini Rwanda.

http://bit.ly/2M7dKFB

http://bit.ly/2ytDvhy



KUPIGANA DHIDI YA RUSHWA

HADHIRA KUSUDIWA General Audience

MASHIRIKA HUSIKA Eugene Kwibuka - The New Times

MJUMBE
Serikali

NJIA YA MAWASILISHO
Makala za habari

Kiingereza

Kisiasa

UJUMBE

Makala hii inaonyesha mahojiano ya Huguette Labelle, ambaye ni mwenyekiti wa Bodi ya Transparency International. Anazungumzia kuhusu Rwanda, tangu ilipotambulika mwaka 2013 kuwa nchi yenye rushwa kidogo Afrika. Hii ni muhimu ili kukabiliana na masimulizi ya makundi ya ufurutu ambayo yanaweza kuonyesha ufisadi wa serikali Afrika kama sababu ya kujiunga nao.

http://bit.ly/2t9LPxY

http://bit.ly/2JQp8Jo




USHIRIKI WA VIJANA RWANDA

HADHIRA KUSUDIWA Hadhira ya jumla

MASHIRIKA HUSIKA Serikali ya Rwanda

MJUMBE
Serikali

NJIA YA MAWASILISHO
Waraka

Kiingereza

Kisiasa

UJUMBE

Mpango Mkakati wa vijana wa Rwanda 2013-2018 unaonyesha jinsi Rwanda imekuwa ikijaribu kuwahusisha vijana katika kujenga mshikamano wa kijamii, kuhamasisha vijana kushiriki kwenye ulingo wa siasa kama viongozi wa baadaye kwenye nchi.

http://bit.ly/2I3JJUQ




KUTOA MIRADI BORA YA UCHUMI JAMIIRWANDA

HADHIRA KUSUDIWA Hadhira ya jumla

MASHIRIKA HUSIKA Serikali ya Rwanda

MJUMBE
Serikali

NJIA YA MAWASILISHO
Waraka

Kiingereza

Kisiasa

UJUMBE

Rwanda imeshatengeneza sera mbalimbali ili kupunguza ghasia nchini. Serikali inatoa kwa ufanisi miradi ya kijamii kiuchumi kama vile ya mutuelle de sante ambayo huchangia kwenye viwango vya maisha bora ili kuzuia watu kutojihusisha katika migogoro. Pia wameweka viwango kwa ajili ya elimu ya amani na mipango ya elimu ya kuzuia mauaji ya kimbari katika sekta zote za elimu rasmi na sekta isiyo rasmi kupitia makumbusho na miradi ya elimu.

http://www.rdb.rw/uploads/tx_sbdownloader/EDPRS_2_Main_Document.pdf

http://bit.ly/2JYr8LA

## SOMALIA



QURACA NABADDA

HADHIRA KUSUDIWA Hadhira ya jumla,Watafutaji, Jumla ya wengi- Hadhira

MASHIRIKA HUSIKA Center for Research & Dialogue

MJUMBE
Viongozi wa Jamii, Wasanii wenyeji

NJIA YA MAWASILISHO
Matukio, Mabango

Kisomali

Kikabila

UJUMBE

Quraca Nabadda ni mpango wa maridhiano ya kijamii unotekelezwa na Somali Youth Development Network (SOYDEN). Mradi wa wiki 12 uliolenga kuimarisha amani changa nchini Somalia kupitia warsha, ushauri nasaha na kuonesha mfano wa kujitoa kwenye mlolongo wa vurugu kwa wahanga wa mzozo wa kikabila, uhalifu, vurugu zenye misingi ya jinsia na ugaidi.

Sehemu ya mradi ilihusisha kutengeneza mabango. Mabango yanayotokea kwenye tovuti hii ni michoro ya wasanii wenyeji wa Somalia, iliyotengenezwa katika kituo cha utafiti na mijadala. Ilikuwa imewekwa kuzunguka Mogadishu kuchochea mjadala kuhusu masuala ya migogoro na jamii.

http://bit.ly/2yqFtz9

http://bit.ly/2to72Dh



KAMPENI ACHA WASIKIE SAUTI YAKO

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla, Watafutaji

**MASHIRIKA HUSIKA** Anti-Tribalism Movement (ATM)

**MJUMBE**
Vijana

**NJIA YA MAWASILISHO**
Vipande vya Sinema

Kisomali

Chanya/ mbadala

**UJUMBE**

Wito huu wa sinema kutoka kwa Anti-Tribalism Movement unawaalika vijana kutoa maoni yao dhidi ya chuki na ukabila kwenye jamii zao. Kampeni za "Acha Wasikie Sauiti Yako" ni utii kwa vijana wa Somalia ili kuitikia wito. "Acha Wasikie Sauti Yako" ilikuwa kampeni iliyowafanya vijana kusikilizwa na wagombea wa Urais ambapo vijana nchini Somalia walituma sinema ya sekunde 30 yenye ujumbe uliosema: "tutakuwa raia wa amani wenye kuheshimu serikali yetu na utawala wa sheria, na upande wa pili Serikali yetu inapaswa: (1) Kutoa nafasi za ajira, (2) Kutoa fursa bora ya elimu ya juu, (3) Kuwapa vijana sauti kwenye maamuzi ya sera, (4) Kupambana na rushwa, (5) Kumaliza ukabila, (6) "Kutokomeza Al-Shabaab".

http://bit.ly/2JTboh6

http://bit.ly/2tcg87b



KUHUBIRI KWA VITENDO: ABDI SHIRE

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla

**MASHIRIKA HUSIKA** Anti-Tribalism Movement (ATM)

**MJUMBE**
Viongozi wa Jamii

**NJIA YA MAWASILISHO**
Vipande vya Sinema, Tukio

Kisomali

Kikabila

**UJUMBE**

Kipande hichi chasinema kinaonyesha hadithi ya Abdi Shire, ambaye pia ni mshairi na mwanaharakati nchini Somalia. Abdi Shire anatumia hali yake ya mtu mashuhuri na mashairi kuongelea kikamilifu dhidi ya ugaidi na ufurutu ada, na kuimarisha ujumbe wa amani na kuonyesha matatizo ya ufurutu ada kwenye vyombo vya habari. Sinema inaonyesha picha halisi ya shambulio kwenye sherehe za mahafali nchini Somalia ambako watu 30 waliuawa. Shambulio hili si tu ilionekana kama kitendo cha ugaidi, lakini pia shambulio kwenye elimu. Sinema pia inaonyesha kikundi cha waimbaji, Qaylodhaan, ambacho kilifuatiliwa sana mjini Mogadishu, na kwenye Youtube, kwa ajili ya maonyesho yao na nyimbo kwa ajili ya amani. Hatimaye, Sinema pia inaonyesha mkutano uliofanywa na Anti-Tribalism Movement Istanbul, Uturuki kutafuta suluhisho kwa ugaidi nchini Somalia.

https://bit.ly/1B1vSK9

https://bit.ly/2IUj94N




**BAR KULAN RADIO**

**HADHIRA KUSUDIWA** Watafutaji, Hadhira ya jumla, Hadhira ya Waisilamu wengi na wachache

**MASHIRIKA HUSIKA** Radio Bar Kulan Website

**MJUMBE**
Viongozi wa Jamii, Vijana

**NJIA YA MAWASILISHO**
Tovuti Matangazo ya Redio

Kisomali

Kihistoria Kisiasa

**UJUMBE**

Redio Bar Kulan hutangaza habari na taarifa kwa mitandao inayozungumza kisomali nchini Somalia na Wasomali wanaoishi nje. Habari huonesha hadithi za hivi karibuni zinazohusiana na ugaidi kama vile taarifa kwenye vyombo vya kimataifa kama vile Umoja wa Mataifa na IGAD. Mradi pia unaendesha matukio kwa vijana na kuhusika zaidi na serikali na jamii zao.

www.bar-kulan.com

http://bit.ly/2yoGR5a

http://bit.ly/2JYt2Me




**MPANGO WA VIJANA WAJASIRIAMALI SOMALIA**

**HADHIRA KUSUDIWA** Watafutaji, Hadhira ya Jumla

**MASHIRIKA HUSIKA** Stability Fund

**MJUMBE**
Viongozi wa Jamii, Vijana

**NJIA YA MAWASILISHO**
Makala, Miradi

Kiingereza

Chanya/ mbadala Kiuchumi

**UJUMBE**

Kutokana na ukosefu wa fursa za fedha kwa ajili ya vijana wa Somalia, Stability Fund ilianzisha Mpango wa Vijana Wajasiriamali Somalia. Ukijumuisha taasisi mbili za kifedha na mashirika yasiyo ya kiserikali mawili, mpango unawezesha wajasiriamali vijana wa Somalia kuanzisha biashara zao wenyewe kwa kutoa mikopo ya ushindani na bidhaa zingine za kifedha.

https://bit.ly/1W86E5G



**KITUO CHA MIGOGORO, UTAWALA NA KUJENGA AMANI**

Kiingereza

Kihistoria Kisiasa Kiuchumi

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla

**MASHIRIKA HUSIKA** Stability Fund & City University

**MJUMBE**
Viongozi wa Jamii

**NJIA YA MAWASILISHO**
Makala

**UJUMBE**

Mnamo mwezi Oktoba 2015, Stability Fund ilizindua kituo kwa ajili ya Migogoro, utawala na utafutaji wa amani kwenye Chuo Kikuu cha City Mogadishu. Kituo hutoa programu ya shahada ya juu kwenye migogoro, utawala na utafutaji wa amani, na huchukua wanafunzi 12 kwa mwaka. Wanafunzi hunufaika kwa kulipwa kikamilifu wakati wa majira ya joto mafunzo ya vitendo nje ya nchi. Lengo la kituo ni kuandaa kizazi kijacho cha viongozi, walioelimika kikamilifu nchini Somalia.

https://bit.ly/2rTOcDi

https://bit.ly/2lQRfqr



**UKARABATI WA KISMAYO**

Kiingereza

Chanya/ mbadala Kiuchumi

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla, Watafutaji

**MASHIRIKA HUSIKA** Stability Fund Website

**MJUMBE**
Viongozi wa Jamii

**NJIA YA MAWASILISHO**
Makala

**UJUMBE**

Kwa kushirikiana na Dhasheeg Construction na Trading Comapany, Stability Fund ilianza mradi wa majaribio kwa lengo la kuboresha ajira ya vijana ; kwa vijana wa Kismayo. Mradi ulihushisha ujenzi wa barabara kuu ya Kismayo, ambayo inaunganisha wakaazi wa Farjano na Faanooles hadi soko kuu la Kismayo, hospitali na shule. Mradi huo uliajiri vijana 200 na kuwezesha usafiri kwenye mji.

https://bit.ly/2bcHZNJ

https://bit.ly/1KBPS5H




MAISHA YALIYOHARIBIKA

Somali Tafsiri ya Kiingereza

Kikabila Kijamii

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla, Watafutaji

**MASHIRIKA HUSIKA** Anti-Tribalism Movement (ATM)

**MJUMBE**
Viongozi wa jamii, Familia

**NJIA YA MAWASILISHO**
Vipande vya Sinema

**UJUMBE**

Lengo la sinema hii ni kuonyesha na kupaza sauti kwa akina mama ambao wanapata mateso ya itikadi ya Al-Shabaab. Mateso yao ni ya aina mbalimbali. Akina mama hawa wana watoto wakiume na au mabinti wanaoshiriki kwenye Al-Shabaab, na kilio chao ni kuwapoteza, kwa kuuawa na Al-Shabaab.

https://bit.ly/1B1vSK9




MSOMALI ALIYEPOTEA (MWANAFUNZI) ALSHABAB

Kisomali Tafsiri ya Kiingereza

Kijamii Kikabila

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla, Watafutaji, Wasikitikaji

**MASHIRIKA HUSIKA** Anti-Tribalism Movement (ATM)

**MJUMBE**
Viongozi wa jamii

**NJIA YA MAWASILISHO**
Vipande vya Sinema

**UJUMBE**

Hii ni taarifa ya mtu aliyetekwa nyara na mwanachama wa Al-Shabaab. Inaonyeshabaadhi ya hoja za Al - Shabaab wakidai kwamba kikundi hiki kinapigana kwa ajili ya ustawi wa watu wenye hali mbaya. Alipotoroka utekaji nyara, mtu huyu bado anapokea vitisho kutoka kwa magaidi mara kwa mara. Anaonyesha matokeo ya ugaidi, ikiwa ni pamoja na uathirika.

https://bit.ly/2wWT9Bk



UTU ULIOPOTEA: MWANAMUZIKI WA SOMALIA

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla, Watafutaji, Wathibitishaji

**MASHIRIKA HUSIKA** Anti-Tribalism Movement (ATM)

Kisomali Tafsiri ya Kiingereza

Kijamii

**MJUMBE**

Viongozi wa jamii, Vijana

**NJIA YA MAWASILISHO**

Vipande vya Sinema

**UJUMBE**

Mwanamuziki kijana wa Kisomali adhihirisha ukosefu wa uvumilivu miongoni mwa wafurutu kutokana na kushindwa kukubali muziki. Anashirikisha uzoefu wake kwenye ufurutu ada, ikiwa ni pamoja na vitisho juu ya maisha yake, kwa sababu ya muziki wake. Al-Shabaab wanadai kuwa wanapigana kwa ajili ya ustawi wa watu, lakini hawaruhusu kujielezea kupitia muziki.

https://bit.ly/2rVfcmZ



UTU ULIOPOTEA:FUNDI MAGARI SOMALIA AL-SHABAAB

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhiraya jumla, Watafutaji, Wasikitikaji

**MASHIRIKA HUSIKA** Anti-Tribalism Movement (ATM)

Kisomali Tafsiri ya Kiingereza

Kijamii Kikabila

**MJUMBE**

Viongozi wa jamii

**NJIA YA MAWASILISHO**

Vipande vya Sinema

**UJUMBE**

Huyu fundi magari kijana wa Kisomalia aliwekwa chini ya ulinzi na Al Shabaab. Kwa sasa amekimbilia Mogadishu, anaishi chini ya hatari za mara kwa mara na vitisho. Hadithi inaonyesha matokeo ya ugaidi, na kuishi chini ya hofu.

https://bit.ly/2ltgfE0



UTU ULIOPOTEA: MWANAHABARI WA SOMALI

Kisomali
Tafsiri ya Kiingereza

Social
Ethical

| | |
|---|---|
| HADHIRA KUSUDIWA | Hadhira ya jumla, Watafutaji, Wasikitikaji |
| MASHIRIKA HUSIKA | Anti-Tribalism Movement (ATM) |

**MJUMBE**

Viongozi wa jamii, Vyombo Vya habari

**NJIA YA MAWASILISHO**

Ukurasa wa mitandao ya kijamii

**UJUMBE**

Mwandishi wa habari hii anashirikisha hadithi yake ya kupokea vitisho vya kifo kila siku kwa ajili ya kutoa taarifa juu ya hadithi zao. Mwandishi wa habari anashirikisha makovu yake tangu alipotekwa nyara na kuteswa na Al Shabaab. Simulizi ina maana kubwa kwa sababu Al Shabaab wanadai wanaboresha ustawi wa Somalia, lakini hadithi za waathirika na mateso vinaashiria vinginevyo.

https://bit.ly/2IRT1HY



VIJANA NA WAZEE WA KISOMALIA WAMEUNGANA DHIDI YA UKABILA NA UFURUTU

Kisomali
Kiingereza

Kidini
Kiitikadi

| | |
|---|---|
| HADHIRA KUSUDIWA | Hadhira ya jumla, Wasikitikaji, Watafutaji & Hadhira ya Waisilamu wengi na wachache |
| MASHIRIKA HUSIKA | Anti-Tribalism Movement (ATM) |

**MJUMBE**

Viongozi wa Jamii (Maimamu)

**NJIA YA MAWASILISHO**

Vipande vya Sinema

**UJUMBE**

Mradi huu ukiwezeshwa na Anti-Tribalism Movement uliitisha mkutano wa maimamu wa Somalia huko Istanbul, Uturuki, kutoa fatwa dhidi ya Al-Shabaab. Katika mkutano huu, vijana na wazee waliungana dhidi ya ukabila na ugaidi ili kuzungumza pamoja kwa sauti moja.

https://bit.ly/2k8QlYt



**WAJUMBE WANAOAMINIKA**

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla, Wasikitikaji, Watafutaji na Hadhira ya Waisilamu wengi na wachache

**MASHIRIKA HUSIKA** Anti-Tribalism Movement

**MJUMBE**
Viongozi wa Jamii (Maimamu)

**NJIA YA MAWASILISHO**
Tovuti

Kisomali
Kiingereza

Kimaadili
Kidini
Kiitikadi

**UJUMBE**

Wajumbe Wanaoaminika ni mradi uliopo Kusini na katikati ya Somalia ambao unafanya kazi na kikundi cha maimamu kutoa simulizi kinzani kiteolojia kwa Al-Shabaab. Wajumbe wakuaminika huandaa matukio ya mara kwa mara kwenye miji yao na vijiji na kujadili masuala mbalimbali yanayohusiana na Al - Shabaab kama vile ya kujitoa muhanga na jinsi yalivyoharamu katika Uislamu.

https://bit.ly/2Gybjsk



**SIKU YA VIJANA SOMALIA**

**HADHIRA KUSUDIWA** Wathibitishaji, Wasikitikaji

**MASHIRIKA HUSIKA** Breakthrough Media, Anti-Tribalism Movement

**MJUMBE**
Viongozi wa jamii

**NJIA YA MAWASILISHO**
Tovuti

Kisomali
Kiingereza

Kikabila
Kijamii

**UJUMBE**

Kusherehekea siku ya vijana wa Somalia, ATM ilitengeneza jukwaa ambapo vijana wanaotoka koo tofauti wanaweza kuja pamoja na kujadili jinsi wangeweza kuchangia kwa mustakabali chanya wa Somalia. Jukwaa hilo lilitengenezwa kwa kuunganisha ukweli kwamba vijana wa Somalia wanaweza na wamefanya jukumu muhimu kwenye mafanikio ya hivi karibuni ya Somalia na kuhimiza Wasomali wengine vijana kutimiza majukumu yao kwenye maendeleo ya nchi. Pamoja na kuandaa jukwaa, Breakthrough Media iliandaa kampeni ya kufikisha ujumbe muhimu kwa hadhira pana Somalia yote. Kwa kufanya hivyo, Breakthrough Media iliandaa kampeni ya bango la matangazo ndani ya Mogadishu, kampeni ya mitandao ya kijamii ya taifa yenye maudhui ya maandishi, michoro na sinema na kampeni ya wiki nne ya Redio PSA. Breakthrough Media pia hutangaza mubashara jukwaa kwenye Redio ya taifa na kuanzisha huduma ya ujumbe mfupi na simu ili kuruhusuwasikilizaji wa redio kuchangia mjadala.

http://bit.ly/2K4nhg9




**TUBTA NAABADDA**

Kisomali

Kimaadili Kidini Kiitikadi

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla, Wathibitishaji, Wasikitikaji

**MASHIRIKA HUSIKA** UNSOM Somalia & Somalia National TV

**MJUMBE**

Serikali

**NJIA YA MAWASILISHO**

Mfululizo wa Sinema

**UJUMBE**

Tubta Nabadda ni jukwaa la serikali la Somalia, kupitia mfululizo wa sinema, ambalo mara kwa mara limealika Masheikh wa Somalia kutoa tafsiri sahihi wa Uislamu na limekuwa na mafanikio kwa kupambana na Al-Shabaab kwa kutumia marejeo ya maandiko na kupunguza mvuto wa kidini wa Al-Shabaab. Mfululizo pia umeambatana na alama ya reli ya, #TubtaNabadda.

https://bit.ly/2DVzZdi



**KITUO CHA KIDIGITALI CHA KUKABILIANA NA UFURUTU: SOMALIA**

Kiingereza

Kisiasa

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla, Wathibitishaji, Wasikitikaji

**MASHIRIKA HUSIKA** Serikali ya Somalia

**MJUMBE**

Serikali

**NJIA YA MAWASILISHO**

Makala za habari

**UJUMBE**

Kituo cha serikali ya Somalia cha kidigitali cha kukabiliana na ufurutu ada kinakusudia kuwazuia vijana wa Somalia kuunga mkono vikundi vya wanamgambo kama vile Al-Shabaab na dola ya Kiislamu. Kituo kinafanya kampeni kwenye Facebook, YouTube, Twitter, na vyombo vya habari vya serikali vilivyoundwa kukuza utulivu katika taifa ya pembe ya Afrika.

https://bit.ly/2D4Yj07



**WANAUME WA SHABAAB WAMEWAGEUZA WASICHANA WA SHULE WA KENYAKUWA WATUMWA WA NGONO**

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla, Watafutaji

**MJUMBE**

Waasi, Wamwanzo

**NJIA YA MAWASILISHO**

Makala Za Habari

Kiingereza

Kijamii Chanya/ mbadala

**UJUMBE**

Bango hili linaelezea taarifa muhimu kuhusu dini za ulimwengu kwenye maadhimisho ya "Siku ya kanuni ya dhahabu" tarehe 5 Aprili. Bango linahimiza pia maadhimisho ya umoja wa mataifa kwenye siku ya kimataifa ya amani na wiki ya maelewano baina ya dini ulimwenguni. Bango linasisitiza kutenda kwa kuzingatia "Kanuni ya dhahabu" na linatoa nukuu kutoka kila dini katika kumuunga mkono kuwatendea wengine kwa wema na upendo.

https://bit.ly/2ly7Pw7




**WATUMWA WA NGONO WA AL SHABAAB**

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla, Watafutaji

**MASHIRIKA HUSIKA** BBC

**MJUMBE**

Waasi, Wamwanzo, Waathirika wa ugaidi

**NJIA YA MAWASILISHO**

Maandishi, Vipande vya Sinema

Kiingereza

Kijamii

**UJUMBE**

Hadithi ya wasichana wanne wa Kenya ambao walijiunga na Al Shabaab inaonyesha uzandiki wa kikundi wanaowatendea wanawake. Simulizi ya Halima, mwenye miaka 16, inaonyesha jinsi wapiganaji na viongozai wa Al - Shabaab mara kwa mara walivyowabaka na kuwanyanyasa wasichana wadogo wakati wa muda wao kwenye kikundi. Pia walichukuliwa kama wake, lakini pia walilazimishwa kutoa mimba pale walipopata ujauzito.

https://bit.ly/2LhL4dw

https://bbc.in/2qgh0YM



KWANINI NILIONDOKA AL-SHABAAB

Kiingereza

Kijamii

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla, Watafutaji

**MASHIRIKA HUSIKA** BBC

**MJUMBE**

Waasi, Wamwanzo

**NJIA YA MAWASILISHO**

Makala za habari, Vipande vya Sinema

**UJUMBE**

Makala hii ya habari inaonyesha hadithi ya Zakariya Ahmed Ismali Hersi, kiongozi wa zamani wa Al Shabaab. Kwenye ushuhuda wake, anaonyesha awali alijiunga kuikomboa nchi, lakini hatimaye alitambua kwamba lengo la awali halikuweza kutekelezwa kupitia kundi hilo la kigaidi. Alihisi kwamba kundi hilo lilikiuka lengo halisi, na kwamba alitambua vikosi vya usalama viliua na kuwakamata wenzake wengi. Alijiondoa kutoka kwa Al Shabaab kuokoa maisha yake mwenyewe.

https://bbc.in/1K2nFVU



HADITHI ZA MANUSURA WA UFURUTU ADA: SOMALIA

Kiingereza

Kijamii

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla, Watafutaji, Wathibitishaji

**MASHIRIKA HUSIKA** UNDP

**MJUMBE**

Waathirika wa ugaidi

**NJIA YA MAWASILISHO**

Tovuti

**UJUMBE**

Tovuti hii ina hadithi fupi za manusura wa ufurutu ada nchini Somalia, ikiwa ni pamoja na mashambulizi yaliyofanywa na Al-Shabaab. Hadithi inafupisha madhila ya kimwili na kihisia waliopata kwa wahanga na manusura. Yaliyomo katika hadithi ni pamoja maelezo ya wanafamilia waliopoteza wapendwa wao katika mashambulizi ya Al-Shabaab.

https://bit.ly/2GxScig



## KURUDI SOMALIA: HADITHI YA ALIYA

Kiingereza

Kimaadili Kihistoria Kisiasa

| | |
|---|---|
| HADHIRA KUSUDIWA | Hadhira ya jumla, Hadhira ya Waislamu wachache na wengi |
| MASHIRIKA HUSIKA | Breakthrough Media |

**MJUMBE**
Waathirika, Manusura

**NJIA YA MAWASILISHO**
Vipande vya Sinema

**UJUMBE**

Sinema inaonyesha hadithi ya Aliya Durban, mhamasihsji wa muziki kutoka Atlanta na kwa asili ni mwanamke wa Kisomali. Sinema inaonyesha hadithi yake kama alivyorejea Somalia kugundua historia ya familia yake, mizizi na nchi ya mama yake na Baba. Ana shuhudia uharibifu wa vita, ikiwa ni pamoja na magofu ya nyumba yake ya zamani ya familia. Pia alishuhudia umaskini wa watu wanaoishi katika magofu ya nyumba ya kale ya familia yake -wakimbizi wa ndani. Uzoefu wa Aliya unaonyesha vipengele vyote chanya na hasi vya maisha nchini Somalia kutokana na mtazamo wa mtu ambaye amekulia katika nchi za Magharibi.

https://bit.ly/2lNr2dm



## HILI 'HALIKUWA BOMU JINGINE TU MOGADISHU.' ITAHARIBU AL-SHEBAAB

Kiingereza

Kihistoria Kisiasa

| | |
|---|---|
| HADHIRA KUSUDIWA | Wathibitishaji, Wasikitikaji, Watafutaji |
| MASHIRIKA HUSIKA | Abdirah Man Omar Osman (Engineer Yarisow |

**MJUMBE**
Waathirika, Manusura

**NJIA YA MAWASILISHO**
Makala ya Gazeti

**UJUMBE**

Baada ya bomu kubwa kulipuka huko Mogadishu tarehe 14 Oktoba 2017, jamii nchini Somalia iliharibika, lakini pia yenye ustahimiluvu zaidi dhidi ya Al-Shabaab. Mlipuko wa bomu uliua watu zaidi 350, na kwa mujibu wa mwandishi, umepoteza himaya ya Al-Shabaab nchini. Mwitikio wa jamii dhidi ya shambulio hilo ilikuwa ni kuchangia kiasi kikubwa cha damu. Juhudi ya uratibu wa asasi za kiraia (#Gurmad252) pia ilikuwa amilifu kusaidia waathirika wa shambulio hilo. Vifaa tiba vililetwa kwa ndege za ndani na za kimataifa ili kusaidia baadhi ya jitihada za misaada. Maandamano dhidi ya Al-Shabaab pia yalitokea siku 2 baada ya shambulio, kuonyesha ustahimilivu. Kiongozi wa zamani wa al-Shabaab, Abu Mansur Mukhtar Robow, alikuwa mmojawa waliojitolea damu, na kulaaani shirika lake la zamani kwa kushambulia "watoto wa taifa.

https://bit.ly/2KWESqc



ANGUSHA BUNDUKI OKOTA KALAMU

HADHIRA KUSUDIWA Wathibitishaji, Wakosaji

MASHIRIKA HUSIKA Elman Peace

Kiingereza

Kijamii Kiuchumi

MJUMBE
Viongozi wa Jamii

NJIA YA MAWASILISHO
Vipande vya Sinema

UJUMBE

Mpango huu unalenga kuweka silaha chini, ukarabati na kuwaunganisha vijana wanaume na wanawake ambao washiriki katika mapambano ya silaha nchini Somalia tangu miaka ya 1990. Lengo la mpango ni kuwaunganisha wanajeshi watoto na vijana. Mpango unatumia kazi za kijamii na ujuzi wa ajira kama sehemu ya mkakati wa kuwaunganisha.

https://bit.ly/2lylfag

https://bit.ly/2kcnyT1



JE TATIZO LA KWELI NI KUOTESHA NDEVU?

HADHIRA KUSUDIWA Wathibitishaji, Wasikitikaji

MASHIRIKA HUSIKA Al Awsat

Kiarabu

Kijamii Kidini

MJUMBE
Viongozi wa Jamii

NJIA YA MAWASILISHO
Makala

UJUMBE

Makala inajadili mgogoro wa muda mrefu nchini Somalia. Mwandishi akikashifu kiongozi wa Kiislamu wa Somalia kwenye chama cha Kiislamu, kwenye mkutano na vyombo vya habari, ambao licha ya mgogoro nchi inaopitia alidai kwamba watu wote lazima wafuge ndevu na kunyoa masharubu yao kama sharti la lazima la sheria ya dini yao.

https://bit.ly/2rYt0Mw




**TAIFA LA USHAIRI**

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla

**MASHIRIKA HUSIKA** Poet Nation

**MJUMBE**
Viongozi wa Jamii, Vijana

**NJIA YA MAWASILISHO**
Tovuti

Kiingereza

Kijamii

**UJUMBE**

Lengo la tovuti ni kuwahusisha vijana wa Somalia, ikiwa ni pamoja na ughaibuni kutoka duniani kote, kupitia mashairi, muziki na Simulizi za visa. Tovuti inakusudia kuwa jukwaa kwa ajili ya mazungumzo mazuri ambayo hukuza amani, maelewano na tunu jadi za Somalia kwa kizazi cha vijana.

http://thepoetnation.com/



**MAISHA BORA KULIKO LEO**

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla, Watafutaji

**MASHIRIKA HUSIKA** Stability Fund, BBC Media Action websites

**MJUMBE**
Vijana

**NJIA YA MAWASILISHO**
Makala

Kisomali

Chanya/mbadala

**UJUMBE**

Stability Fund, kwa kushirikiana na BBC Media Action Service, wameshirikiana kutengeneza mchezo wa redio shirikishi kwa vijana wa Somalia, ambao wasikilizaji wanaweza kupiga kura kuamua hatima ya wahusika. Onyesho linaitwa Maalmo Dhama Maanta (Maisha Bora Kuliko Leo). Msingi wa simulizi unajikita kwenye vijana wa Somalia wenye ndoto ya maisha bora ya baadaye. Mchezo wa kuigiza unagusia mada kama vile siasa, uhamiaji, uchumi na utawala. Onyesho linarushwa kwenye Redio Hargeisa, Redio Goobjoog na Redio Garowe.

https://bit.ly/2KFX4Ei

https://bbc.in/2oGxTZ8



**MEYA WA MOGADISHU**

Kiingereza

Kihistoria Kisiasa

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla, Watafutaji

**MASHIRIKA HUSIKA** Breakthrough Media

**MJUMBE**
Serikali

**NJIA YA MAWASILISHO**
Klipu Video

**UJUMBE**

Filamu "Meya wa Mogadishu" inahusu Meya kwenye majukumu yake ya kila siku serikalini kuonyesha namna ya kuongoza mji kulivyo. Sinema inaonyesha mahojiano na maelezo ya maamuzi ya serikali kupitia Meya. Pia inaonyesha sherehe mitaani iliyofanyika huko Mogadishu kusherehekea utamaduni, muziki na tamaduni za Somalia kama njia ya kuunganisha mji.

https://bit.ly/2GUsdSf

## SUDANI YA KUSINI



**SUDAN YA KUSINI:MAKABILA MAWILI YAJENGE KILICHOBOMOLEWA NA VURUGU**

Kiingereza

Kikabila

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla

**MASHIRIKA HUSIKA** Search for Common Ground

**MJUMBE**
Viongozi wa Jamii

**NJIA YA MAWASILISHO**
Klipu Video

**UJUMBE**

Sinema hii inaonyesha mpango uliofanywa na Search for Common Ground Sudan Kusini mnamo 2015. Mpango ulianza mchakato wa maridhiano kati ya makabila Madi na Acholi, na kipindi cha redio na mazungumzo ya jamii yameendeleza mchakato. Mpango uliwatambua Wazungumzaji waliokuwa na uwezo wa kuingilia kati katika mgogoro na kuwaleta pamoja ili kupata ufumbuzi wa pamoja kwenye jamii.

https://bit.ly/2lWiikm



### KUFANYA MIUJIZA: WAKIMBIZI WA SUDAN YA KUSINI WAMEPATATUMAINI KWENYE SANAA SHIRIKISHI

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla

**MASHIRIKA HUSIKA** Search for Common Ground

**MJUMBE**

Viongozi wa Jamii, Waigizaji

**NJIA YA MAWASILISHO**

Vipande vya Sinema

Kiingereza

Chanya/ mbadala

**UJUMBE**

Sinema hii inaelezea mradi kwenye makambi ya wakimbizi Sudan Kusini nchini Kenya ambapo watu wanatumia maonyesho shirikishi kueleza malalamiko na kuanza majadiliano kuhusu mada ngumu. Sanaa ya maonyesho pia inatoa fursa kwa watu binafsi kwenye makambi ili kupata ufumbuzi wa pamoja. Hadithi Sanaa zimejikita kwenye matukio ya kweli na kuruhusu hadhira kujibu kinachoendelea jukwaani, na hata kufanya maamuzi juu ya namna utendaji unavyoisha.

https://bit.ly/2d27rl1



### ANA TABAN (NIMECHOKA)

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla, Watafutaji

**MASHIRIKA HUSIKA** Anataban Collective

**MJUMBE**

Viongozi wa Jamii, Wasanii

**NJIA YA MAWASILISHO**

Makala habari, Picha, Kampeni Mitandao ya jamii

Kiingereza Kiarabu

Chanya/ mbadala

**UJUMBE**

Anataban Collective hutumia graffiti, maonesho, uchongaji na mashairi kueneza ujumbe wao wa amani. Michoro yao iliyotengezwa na wanachama wa kikundi huonekana kwenye kuta huko Juba, Sudan ya Kusini. Mradi ulianza Septemba 2016 wakati wasaniiwa Sudan ya Kusini na wanaharakati walipounganisha nguvu kumaliza vurugu ambazo zimekuwa zikisumbua nchi mpya duniani tangu 2013. Harakati ziliambata na alama ya reli sambamba, #Anataban, ambayo imekuwa maarufu miongoni mwa vijana Sudan Kusini.

https://reut.rs/2lZrCUm

https://reut.rs/2t9C5AG

https://bit.ly/2lU3vXm



#ANATA-BAN SINEMA RASMI:MUZIKI WA SUDAN KUSINI

HADHIRA KUSUDIWA General Audience, Seekers

MASHIRIKA HUSIKA Anataban Collective

MJUMBE

Viongozi wa Jamii, Wasanii

NJIA YA MAWASILISHO

Wimbo, Sinema ya Muziki

Kiarabu (Sudani kusini)

Kikabila

UJUMBE

Wimbo huu ulitengenezwa na Anataban collective unaonyesha nchi iliyoharibiwa na vita na yote ambayo ni muhimu kufanya mabadiliko kwa ajili ya hatima nzuri Sudan Kusini. Wimbo pia unaambatana na alama ya reli #Anataban.

https://bit.ly/2MhYNk1



SOUTNA (SAUTI YETU):MUZIKI WA SUDAN KUSINI

HADHIRA KUSUDIWA Hadhira ya jumla,Watafutaji

MASHIRIKA HUSIKA Anataban Collective

MJUMBE

Viongozi wa Jamii, Wasanii

NJIA YA MAWASILISHO

Wimbo, Sinema ya Muziki

Kiingereza Kiarabu (Sudani kusini))

Chanya/ mbadala

UJUMBE

Wimbo huu ulitengenezwa na Anataban Collective ukionyesha wito kutoka kwa vijana kwa ajili ya amani Sudan Kusini. Ujumbe unaolenga viongozi wa Sudan Kusini kumaliza vurugu, vita, dhuluma na umaskini. Wimbo pia unaambatana na alama za reli ya #Anataban na #Kumwaga Damu- Huru2017.

https://bit.ly/2LhotxG




**MALESH (SAMAHANI): MUZIKI WA SUDAN KUSINI**

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla, Watafutaji

**MASHIRIKA HUSIKA** Anataban Collective

**MJUMBE**
Viongozi wa Jamii, Wasanii

**NJIA YA MAWASILISHO**
Wimbo, Sinema ya Muziki

Kiingereza
Kiarabu (Sudani kusini))

Chanya/ mbadala

**UJUMBE**

Wimbo huu ulitengenezwa na Anataban unaangalia makosa ambayo Wasudan Kusini wametendeana, ikiwa ni pamoja na vurugu, vita na mauaji. Wimbo unakuza uponyaji, msamaha na upatanisho. Wimbo pia ni unaambatana na alama ya reli #Anataban.

https://bit.ly/2KeBK9i




**#DEFYHATENOW**

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla, Watafutaji

**MASHIRIKA HUSIKA** #defyhatenow

**MJUMBE**
Viongozi wa Jamii, Vijana

**NJIA YA MAWASILISHO**
Tovuti

Kiingereza

Kikabila

**UJUMBE**

#DefyHateNow ni mradi wa utafutaji wa amani unaodhoofisha hotuba za chuki na unataka kuimarisha matendo ya kuhamasisha vijana kuendeleza amani na kutotumia mabavu. Mradi unatumia mbinu za mtandaoni na nje ya mtandao na unakusudia kuwezesha uelewa na ujuzi wa zana za mitandao ya kijamii kwa vijana wa Sudan ya Kusini.

https://bit.ly/2K6T2JH

## JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



**KAMPENI YA VIJANA NA AMANI**

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla, Watafutaji, Hadhira ya Waislamu wachache na wengi

**MASHIRIKA HUSIKA** Global Peace Foundation

**MJUMBE**

Viongozi wa Jamii

**NJIA YA MAWASILISHO**

Tukio, Programu, Mitandao ya kijamii

Kiingereza Swahili

Kikabila Chanya/ mbadala

**UJUMBE**

Ujumbe huu ulikusudiwa kulenga utambulisho-kulingana na mgogoro na ufurutu ada nchini Tanzania, ambao ni asilimia 60 ya idadi ya watu. Kampeni ya Vijana Na Amani inataka kuhimiza elimu, uhamasishaji, uongozi na kujenga uwezo kupitia kampeni kwa ajili ya amani na vijana wenyewe.

https://bit.ly/2LnDYnK

https://bit.ly/2J2gciH

https://bit.ly/2KKZeTl



**ACHA VURUGU**

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla, Wathibitishaji, Wakusikika, Hadhira ya Waislamu wengi na wachache

**MASHIRIKA HUSIKA** Zanzibar Youth Forum

**MJUMBE**

Viongozi wa Jamii, Vijana

**NJIA YA MAWASILISHO**

Bango, Kipeperushi

Kiingereza Swahilia

Kijamii

**UJUMBE**

Haya mabango na vipeperushi kutoka Zanzibar Youth Forum yanalenga kukomesha mgogoro wa mabavu. Yanatoa mifano ya njia zenye afya za kusimamia migogoro ambazo hazisababishi vurugu. Pia yanatoa mapendekezo kwa utatuzi wa migogoro wenye mafanikio katika namna isiyo ya vurugu.




**WAAJIRIWA 11 WA AL-SHABAAB WAKAMATWA BAADA YA TAARIFA ZA MAFUNZO YA SIRI**

Kiingereza

Kihistoria, Ukweli wa kisiasa

| | |
|---|---|
| HADHIRA KUSUDIWA | Hadhira ya jumla, Watafutaji |
| MASHIRIKA HUSIKA | Abdallah Bakari |

**MJUMBE**

Serikali

**NJIA YA MAWASILISHO**

Makala za habari

**UJUMBE**

Makalaya habari kulingana na polisi kwenye mkoa wa Mtwara Tanzania. Polisi waliwakamata wanamafunzo 11 wa Al-Shabaab wakimilki diski video za kidigitali (DVD) 25 zikionyesha miongozo ya mafunzo ya Al-Shabaab. Makala hii inaweza kuwa njia muhimu ya kuzuia watu ambao huenda wavutiwa na propaganda za Al-Shabaab na inaonya juu ya hatari ya kusambaza propaganda nchini Tanzania.

https://bit.ly/2x6SKMt



**MLIPUKO KWENYE BAA KASKAZINI MWA TANZANIA UMEJERUHI WATU 15**

Kiingereza

Historical Political Factual

| | |
|---|---|
| HADHIRA KUSUDIWA | Hadhira ya jumla, Watafutaji |
| MASHIRIKA HUSIKA | Reuters |

**MJUMBE**

Vyombo vya Habari

**NJIA YA MAWASILISHO**

Makala za habari

**UJUMBE**

Ujumbe huu unaweka wazi hatari ya ugaidi kwa kuonyesha matokeo hasi kwenye utalii. Bomu lililipuka kwenye baa maarufu ikiwa na watalii mjini Arusha. Shambulio lilijeruhi watu 15. Lilitokea wakati mashabiki wa mpira wa miguu walikuwa wakiangalia mechi ya Ligi kuu ya Uingereza kwenye runinga ya baa.

https://reut.rs/2lCsMWy



MABINTI WAWILI WA KIZUNGU WASHMBULIWA KWA TINDIKALI NA WAISILAMU ZANZIBAR

| | |
|---|---|
| HADHIRA KUSUDIWA | Hadhira ya jumla, Watafutaji |
| MASHIRIKA HUSIKA | Katie Gee and Kirstie Trup |

**MJUMBE**

Mwathirika, Manusura, Kiongozi wa jamii

**NJIA YA MAWASILISHO**

Sinema, Makala za habari

Kiingereza

Kweli Kiuchumi

**UJUMBE**

Ujumbe huu unaonyesha matokeo hasi ya ugaidi. Katika ripoti hii, wasichana wawili wa kiingereza walimwagiwa tindikali kwenye nyuso zao mji mkongwe Zanzibar. Hadithi inaonyesha uzoefu wa wasichana wakiingereza kama waathirika wa shambulio la vurugu. Sinema ya YouTubepia inaonyesha matokeo yakiuchumi ya kufanya mashambulio dhidi ya watalii, ikieleza kuwa utalii ni sehemu muhimu ya uchumi wa Zanzibar.

https://bit.ly/2s21LRZ

https://bbc.in/2x3KLjr



SHAMBULIO LA MSIKITI TANZANIA

| | |
|---|---|
| HADHIRA KUSUDIWA | Hadhira ya jumla, Watafutaji |
| MASHIRIKA HUSIKA | BBC, CCTV |

**MJUMBE**

Vyombo vya Habari

**NJIA YA MAWASILISHO**

Makala za habari, Sinema fupi

Kiingereza

Ukweli

**UJUMBE**

Ujumbe huu unaonyesha matokeo hasi ya ugaidi. Watu watatu waliuawa kwenye msikiti mkoa wa Mwanza Tanzania baada ya kikundi cha vijana wenye mapanga kuvamia kwenye msikiti wakiwakata waliokuwemo ndani, ikiwa ni pamoja na imamu. Washambuliaji walikuwa kama watu 15 na walikuwa wamefunika nyuso zao kwa vinyago wakati wakivamia msikiti. Kwa mujibu wa masimulizi ya walionusurika, washukiwa walionyesha bendera nyeusi yenye maneno meupe yakisomeka 'Dola ya Kiislamu'.

https://bbc.in/2lGbVxX

https://bit.ly/2x6V8CV



MIGOGORO YA KIDINI TANZANIA

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla, Watafutaji

**MASHIRIKA HUSIKA** BBC, World Watch Monitor, EuroNews, Zephania Ubwani

**MJUMBE**
Vyombo vya habari

**NJIA YA MAWASILISHO**
Makala za habari, Sinema fupi

Kiingereza

Ukweli

**UJUMBE**

Watu waliuawa na zaidi ya 60 kujeruhiwa wakati wa mlipuko kwenye mkusanyiko kanisani kaskazini mwa Tanzania jijini Arusha, Mwanza na Zanzibar, Waislamu wenye msimamo mkali waliteketeza makanisa matatu kwenye mkoa wa Mwanza kwa sababu ya madai kwamba Wakristo wanne walichoma kuruani.

https://bbc.in/2GJKXnA

https://bit.ly/2s5RjZ2

https://bit.ly/2J0bbY9

https://bit.ly/2GIGiSA




MAFUNZO YA KIGAIDI TANZANIA

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla, Watafutaji

**MASHIRIKA HUSIKA** Warrior Security; CCTV

**MJUMBE**
Serikali

**NJIA YA MAWASILISHO**
Makala za habari, Sinema fupi

Kiingereza

Kihistoria, kisiasa, Ukweli

**UJUMBE**

Makala habari hii inaonyesha matokeo ya kujiunga na kundi la kigaidi kupitia kukamatwa na kufungwa jela. Wanawake nane na watoto wameshakamatwa kwa tuhuma ya kuwa sehemu ya Kambi ya mafunzo ya kigaidi kwenye viunga vya mji mkubwa wa Tanzania, Dar es Salaam. Ni idadi ya juu hivi karibuni ya ukamataji Afrika Mashariki ambayo imesababisha wasiwasi kwamba magaidi wanaweza kujaribu kueneza ushawishi wao nchini Tanzania.

https://bit.ly/2IFZJBx

https://bit.ly/2IE0QzX



FAMILIA MOJA CHINI YA MUNGU

HADHIRA KUSUDIWA Hadhira ya jumla

MASHIRIKA HUSIKA Global Peace Foundation

MJUMBE
Viongozi wa Jamii

NJIA YA MAWASILISHO
Ukurasa mitandao ya Kijamii, Vipande vya Sinema

Swahili
Kiingereza

Chanya/ mbadala

**UJUMBE**

Hivi karibuni, wafuasi wa ufurutu ada wameshaongeza hali ya wasiwasi kati ya jamii ya Kiislamu na Kikristo. Simulizi hili na Global Peace Foundation linalenga kudhoofisha mgogoro baina ya imani kwa kufundisha vijana wa Kitanzania kwamba wao ni sehemu ya familia moja chini ya Mungu.

https://bit.ly/2LvL4H0

https://bit.ly/2J9VPR3

https://bit.ly/2IMfjeU




AMANI KWANZA

HADHIRA KUSUDIWA Hadhira ya jumla

MASHIRIKA HUSIKA Global Peace Foundation

MJUMBE
Viongozi wa Jamii

NJIA YA MAWASILISHO
Tovuti

Kiingereza
Swahili

Chanya/ mbadala

**UJUMBE**

Amani Kwanza (Kipaumbele ni Amani) ni Simulizi Kinzani kabili ya Kiswahili inayosisitiza kuipa amani kipaumbele cha kwanza. Ujumbe huu unaipa jamii jukwaa la kupaza sauti zao juu ya namna wanavyopaswa kudumisha na kulinda amani wakati wa uchaguzi mkuu na baada ya kipindi cha uchaguzi. Ujumbe unataka kuhamasisha na kuhimiza Watanzania wote kuepuka ufurutu ada wa kisiasa na kudumisha amani, jamii inaelimishwa kuhakikisha kwamba inadumishaamani wakati na baada ya uchaguzi mkuu.

https://bit.ly/2saI5ec

https://bit.ly/2kqX9B0

https://bit.ly/2sa0vf9

https://bit.ly/2IJsD3K



## OKOA KITAA

| | |
|---|---|
| HADHIRA KUSUDIWA | Hadhira ya jumla |
| MASHIRIKA HUSIKA | Tandale Youth Development Centre |

**MJUMBE**

Viongozi wa Jamii

**NJIA YA MAWASILISHO**

Ukurasa mitamdao ya Kijamii, Blog

Kiingereza Swahili

Chanya/ mbadala

**UJUMBE**

Ujumbe huu ulitengenezwa kuhamasisha vijana kuacha ufurutu ada na kujihusisha na shughuli za kusaidia maendeleo ya jamii yao. Kundi kuu la walengwa ni vijana kutoka Tandale, moja ya maeneo yaliyoathirika zaidi na magenge jijini Dar Es Salaam. Eneo la kipato cha chini linasifika kwa mbanano wa watu wengi, ukosefu wa huduma za msingi za kuaminika za kijamii, na vijana wengi hawajaelimika. Simulizi inawahimiza vijana wazawa kuzisaidia jamii zao wenyewe na kufanya jitihada dhidi ya malalamiko haya.

http://bit.ly/2MlXkJt




## AMANI HUANZIA NYUMBANI

| | |
|---|---|
| HADHIRA KUSUDIWA | Hadhira ya jumla |
| MASHIRIKA HUSIKA | Global Peace Foundation |

**MJUMBE**

Viongozi wa Jamii, Vijana

**NJIA YA MAWASILISHO**

Mitamdao ya Kijamii

Kiingereza Swahili

Chanya/ mbadala

**UJUMBE**

Ujumbe huu hutumika kukuza amani kutoka ngazi ya familia ili kuzuia ufurutu ada katika jamii. Kampeni inakusudia kuhamasisha njia za kusaidia familia ili itikadi za ufurutu ada zisiote mizizi na wanafamilia kulindana dhidi ya ushawishi.

https://bit.ly/2xbgeAf



DINI MBALIMBALI UMOJA NA UPENDO

HADHIRA KUSUDIWA Hadhira ya jumla

MASHIRIKA HUSIKA Inter Religious Council For Peace Tanzania (ICPT)

MJUMBE
Viongozi wa Jamii

Kiingereza
Swahili

Chanya/mbadala
Kiitikadi
Kidini

UJUMBE

Ujumbe huu unakusudia kuhimiza Tanzania kuishi kama familia moja bila kujali tofauti zao za kidini. Zaidi ya hayo idadi ya matukio yametokea nchini Tanzania kwa miaka 10 iliyopita ambayo yamesababisha mvutano kati ya Waislamu na Wakristo kama vile mapambano dhidi ya uharibifu wa mabucha ya nyama ya nguruwe katika eneo la Mwembechai ya Dar es Salaam, mgogoro kama Zanzibar inaweza kujiunga katika OIC mwaka 1994, matukio ya polisi kuingia msikitini kukamata watu Mwembechai, mapigano juu ya matumizi ya maziko kwenye kitongoji cha Manzese jijini Dar es Salaam kati ya Waislamu na Wakristo, na kukamatwa kwa mhubiri wa Kiislamu kwa kutukana Dini ya Kikristo.



KIJANA BADILI MWENDO ACHANA NA TABIAHATARISHI

HADHIRA KUSUDIWA Hadhira ya jumla

MASHIRIKA HUSIKA Weep Group/Okoa Kitaa

MJUMBE
Viongozi wa Jamii, Vijana

NJIA YA MAWASILISHO
Vipande vya Sinema

Kiingereza
Swahili

Chanya/mbadala

UJUMBE

Ujumbesimulizi kinzani huu uliwasilishwa kwa vijana kupitia filamu fupi iliyotolewa na kundi la Weupe hasa kuhamasisha vijana wenzao ambao wanaishi kwenye jamii yenye mazingira magumu zaidi pale Tandale na Manzese, Dar Es Salaam, na ulisambazwa kwa YouTube ili kuhakikisha kwamba unawafikia vijana wengi iwezekanavyo na kubadili tabia zao mbaya ikiwa ni pamoja na kuacha kujihusisha na ufurutu ada na ushawishi.

https://bit.ly/2kolYgJ



**NAKUPENDA TANZANIA**

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla

**MASHIRIKA HUSIKA** Global Peace Foundation

**MJUMBE**
Viongozi wa Jamii

**MEDIUM**
Redio

Swahili

Chanya/ Mbadala

**UJUMBE**

"Nakupenda Tanzania" ni ujumbe kupitia wimbo kuhamasisha Watanzania kupenda nchi yao na kuwa waaminifu kwa nchi yao ili kukaa mbali na aina zote za ufurutu ada. Mtunzi wa wimbo huu ni Global Peace Foundation na ulirekodiwa na mmoja wa mwanamuziki maarufu nchini Tanzania, Barnaba Boy, wimbo ulichezwa kwenye redio nchini Tanzania na pia kiungo cha wimbo kusambazwa zaidi kupitia watumiaji wa WhatsApp.

## UGANDA



**UISILAMU NA MAENDELEO CHANYA YA VIJANA**

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla, Jumla ya Wengi-Hadhira ya Kiislamu

**MASHIRIKA HUSIKA** Allied Muslim Youth Uganda

**MJUMBE**
Viongozi wa Jamii, Vijana

**NJIA YA MAWASILISHO**
Vipande vya Sinema

Kiingereza

Chanya/ mbadala Maadili

**UJUMBE**

Imeandikwa na Muhsin Kaduyu, ujumbe huu wa video ni sehemu ya mfululizo wa 'Maisha kwenye Uislamu' ambayo yamelenga kuwaangaza Waganda, hasa Jamii ya Waislamu wa Uganda jinsi ya kuishi kwa amani na kuletea jamii zao matokeo mazuri. Hii hasa ni kuzingatia malezi bora ya watoto.

https://bit.ly/2KWQGsz



## WANAFUNZI VIUNGANISHI

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla, Wasikitikaji

**MASHIRIKA HUSIKA** Allied Muslim Youth Uganda

**MJUMBE**

Viongozi wa Jamii, Vijana

**NJIA YA MAWASILISHO**

Tukio

Kiingereza

Chanya/ mbadala

### UJUMBE

Student Connectors ni mtandao wa kitaifa wa wanafunzi wa Chuo kikuu wa jukwaa la imani mbalimbalinchini Uganda wakifanya kazi ya kuendeleza mazungumzo baina ya dini na ushirikiano. Ukianzishwa na Allied Muslim Youth Uganda kama sehemu ya mradi wa kuzuia/ kupambana na ufurutu ada, mpango unaongozwa na wanafunzi unatoa jukwaa kwa ajili ya vijana, hasa wanafunzi wa vyuo vikuu, kutoka jamii ya imani tofauti ambapo hujadili matatizo yanayojulikana na wote, kijamii na masuala ya kimaadili, thamani ya elimu, matumizi mabaya ya mafundisho ya haki za binadamu, utumiaji wa wasichana, ajira ya watoto, nk kama njia ya kukuza tabia isiyo ya vurugu na kuishi pamoja kwa amani miongoni mwa watu. Mtandao unaundwa na wanachama wa jumuiya ya wanafunzi wa Kiislamu, Muungano wa Maandiko ya Kikristo na vikundi vingine vya ushirika katika wote wanaohusika na vyuo vikuu vya kidini.

https://bit.ly/2GRuTAi




## MAFUNGO YA KIDINI YA VIJANA

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla

**MASHIRIKA HUSIKA** Allied Muslim Youth Uganda

**MJUMBE**

Viongozi wa Jamii, Vijana

**NJIA YA MAWASILISHO**

Tukio, Klipu Video

Kiingereza

Chanya/ mbadala Kiteknolojia Kihistoria Kisiasa Kijamii-maadili

### UJUMBE

Kila mwaka, Allied Muslim Youth Uganda (AMYU) hufanya mafungo ya vijana kidini ambapo vijana kutoka vyuo vikuu wanaowakilisha Imani mballimbali hushirikishana moja kwa moja kwa siku 3 kwenye vipindi vya majadiliaano kwenye vikundi vidogo. Kwa pamoja hushughulikia masuala machungu zaidi na masuala ya mgawanyiko yanayolenga mazingira yao, wakibadilishana uzoefu binafsi, wakjikita kwenye masimulizi shindani na kupeana changamoto za fikra za chuki.

https://bit.ly/2xeBF3g



## AMANI LEO

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla

**MASHIRIKA HUSIKA** Uganda Muslim Youth Development Forum

**MJUMBE**
Viongozi wa Jamii, Vijana

**NJIA YA MAWASILISHO**
Tukio, Mitandao ya Kijamii

Kiingereza

Chanya/ mbadala

**UJUMBE**

Video hii ni sehemu ya kampeni mtandaoni inayoitwa Amani Leo. Amani Leo ni juhudi ya Jukwaa la Maendeleo ya Vijana wa Waislamu Uganda (UMYDF) ambalo linalenga kukuza amani, kutokuhalalisha hotuba za chuki na kutoa njia mbadala za amani kwa matatizo ambayo huchochea vurugu nchini Uganda na dunia kwa ujumla.

https://bit.ly/2J6iNs6

https://bit.ly/2xcp0mt



## HADITHI ZA WAATHIRIKA WA UFURUTU ADA: UGANDA

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla, Watafutaji, Wathibitishaji

**MASHIRIKA HUSIKA** UNDP

**MJUMBE**
Tovuti

**NJIA YA MAWASILISHO**
Wahanga wa Ugaidi

Kiingereza

Kijamii

**UJUMBE**

Tovuti hii inaandika hadithi fupi ya waathirika wa mabomu ya 2010 Kampala nchini Uganda.Waathirika wanaelezea kiwewe walichokikabili na njia walizopitia kunusurika mashambulio. Pia wanazungumzia juu ya sababu za kwa nini wanafikiri mashambulio haya yalifanywa, na ufumbuzi kabambe wa jamii kuzuia mashambuliokama hayo katika siku zijazo.

https://bit.ly/2Lz9bV1




**MATEMBEZI YA KIDINI YAK-ILENGA AMANI KITAIFA YA MWAKA**

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla

**MASHIRIKA HUSIKA** AMYU

**MJUMBE**

Viongozi wa Jamii, Vijana

**NJIA YA MAWASILISHO**

Tukio, Vipande vya Sinema

Kiingereza

Kijamii

**UJUMBE**

Matembezi ya kitaifa kwa mwaka ya maelewano kidini ni tukio kubwa kidini lenyekuongozwa na vijana na kuandaliwa na Allied Muslim Youth Uganda kila mwezi wa pili wakati wa maadhimisho ya Umoja wa Mataifa ya wiki ya masikilizano ya kidini. Huleta mamia ya watu, hasa wanafunzi, bila kujali utaifa wao, jinsia, asili, dini, lugha, au hali yoyote nyingine, kushirikishana katika shughuli za kujenga imani, kukuza uelewano na ushirikiano kwa kufanya kazi pamoja kufikia lengo moja yaani utekelezaji kidini.

https://bit.ly/2LwJUe4




**KONY 2012 WATOTO WASIOONEKANA**

**HADHIRA KUSUDIWA** Hadhira ya jumla

**MASHIRIKA HUSIKA** Invisible Children

**MJUMBE**

Viongozi wa jamii

**NJIA YA MAWASILISHO**

Sinema, tovuti

Kiingereza

Siasa
Dini
Itikadi

**UJUMBE**

Invisible Children ni shirika linalo shirikiana na viongozi wa jamii kwenye programu kuwezesha jamii wazawa. Lengo ni kwa jamii wazawa kujifunza jinsi ya kujilinda kila mmoja kutokana na vurugu, kuponya kutoka kiwewe na kudai haki kutoka kwa viongozi wao katika Afrika ya kati. Invisible Children pia wanatoa simulizi kinzani mbalimbali kupitia filamu za hali halisi. Moja ya filamu ni maelezo mafupi ya mgogoro wa LRA. Filamu nyingine ni kuhusu dhamira ya shirika kupambana na Kony.

https://bit.ly/2KVxL0Q

https://bit.ly/2G05QeB

## KUHUSU HEDAYAH

Hedayah iliundwa kutokana na kuongezeka kwa hamu ya washirika wa jukwaa la kimataifa la kupambana na ugaidi GCTF na jamii pana ya kimataifa kwa ajili ya uanzishwaji wa kituo huru cha kimataifa chenye kujitolea kufanya mazungumzo na mawasiliano, mipango ya kujenga uwezo, utafiti na uchambuzi ili kukabiliana na ufurutu ada katika hali yoyote ile na muonekano wake.

Wakati wa uzinduzi wa GCTF ngazi ya wizara mjini New York mwezi Septemba 2011, UAE ilijitolea kwa ajili ya kutumika kama kituo mwenyeji cha Kimataifa cha ubora kwa ajili ya kukabiliana na ufurutu ada. Mwezi Desemba 2012 Hedayah ilizinduliwa na makao yake makuu yakawa Abu Dhabi, Falme za Kiarabu.

Hedayah inalenga kuwa kituo kikuu cha kimataifa kwa utaalamu na uzoefu ili kukabili ufurutu ada kwa kukuza uelewa na kushirikishana uzoefu kwa ufanisi kutumika kama kituo cha Kimataifachenye ubora kukabili ufurutu ada.

Hedayah
countering violent extremism